# UHALISIA NA UHALISIAJABU KATIKA RIWAYA MPYA: *BABU ALIPOFUFUKA* (SAID AHMED MOHAMED) NA *WATU WA GEHENNA* (TOM OLALI )

NA

MWANGI JEDIDAH WANJIRU

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA ISIMU NA LUGHA, CHUO KIKUU CHA NAIROBI

N0VEMBA 2013

University of NAIROBI Library
0389668 5

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote.

**Sahihi**.............................................. **Tarehe**...11-11-2013...

**Mwangi Jedidah Wanjiru**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia idara ya Isimu na Lugha.

**Sahihi**.............................................. **Tarehe**..12th Nov 201

**Dkt. Rayya Timammy**

**(Msimamizi)**

**Sahihi**.............................................. **Tarehe**...11/11/13...

**Prof. Kineene wa Mutiso**

**(Msimamizi)**

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu Bw. Morris Mwangi na Bi. Martha Mwangi walionilea na kunisomesha na kunifanya niwe na kiu ya masomo ili niweze kufaulu maishani.

Namtabarukia mpwa wangu Leemark, aliyeaga nilipokuwa nikifanya mtihani wangu wa mwaka wa kwanza. Nitaishi kukukumbuka daima. Vilevile, namtabarukia bwanangu mpenzi, John Gichohi, ambaye amekuwa mhimili mkubwa katika masomo yangu tangu shahada ya kwanza, watoto wetu watatu- Newton, Morris na Erick ambao wakati mwingi nimewanyima mahitaji muhimu kama mama ili kuyashughulikia masomo yangu.

## SHUKRANI

Kazi hii imefanikishwa kutokana na ukarimu na juhudi za watu kadhaa waliochangia kwa njia moja au nyingine. Naomba kuwataja baadhi yao kwa mawazo na ushauri walionipa mpaka nikafikia kiwango hiki. Kwanza nazitoa shukrani nyingi kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siha njema wakati wote niliokuwa nikiwania kusoma na kumaliza kazi hii na kunisaidia kuvuka changamoto nyingi nilizopatana nazo. Nawatolea shukrani zisizo na kifani wasimamizi wangu, Prof. Kineene wa Mutiso na Dkt. Rayya Timammy, kwa ushauri wao si haba na kwa kunielekeza tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Ninawashukuru sana kwa kuwajibika kwenu kila wakati nilipowahitaji. Mungu awabariki na kuwaongoza katika shughuli zenu zote. Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha ambao mihadhara yao yote ilikuwa nafasi ya kunishauri kwa njia za kiusomi. Shukrani maalum kwa wahadhiri wafuatao: Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. John Habwe, Prof. Wamitila, Prof. Abdulaziz, Prof. Mbatiah, Dkt. Zaja, Bw. Mungania, Dkt. Tom Olali, Dkt. Buregeya, na Dkt. Mukhwana.

Hakika si haki nikikosa kuwashukuru wahadhiri wafuatao ambao mchango wao katika usomi wangu hauwezi kupuuzwa; Dkt. Mogambi, Dkt. Mbuthia na Dkt. Iribe Mwangi. Shukrani pia kwa wanafunzi wenzangu tulioabiri jahazi hili la masomo pamoja. Hawa ni Alice Ochichi, Elizabeth Yego, Janepher Mulumba na Aziza Amara. Jamaa zangu pia wamechangia pakubwa katika kuhakikisha nimekamilisha masomo yangu. Inanibidi kuwataja baadhi yao kwa majina. Nawashukuru wazazi wangu Bw. Morris Mwangi na Bi Martha Mwangi, ndugu zangu; Macharia, Eng. Waithaka, Leah, Sarah, Nderitu, Wanjugu, Ndung'u, Susan na Jack pamoja na familia zao. Siwezi kusahau Tume ya Kuajiri Walimu (T.S.C) kwa kunipa likizo ya miaka miwili na kunilipa, na pia walimu na wanafunzi wa Crater ambao walibeba mzigo wangu wakati niliondoka. Asante Mary, msichana wangu wa kazi kwani, ulinisaidia kazi za kinyumbani na kuwa mwaminifu katika kazi yako, Mola akubariki.

# IKISIRI

Tasnifu hii inahusu uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya za Said Ahmed Mohammed (*Babu Alipofufuka)* na Tom Olali (*Watu wa Gehenna).* Katika utafiti huu tumechunguza uhalisiajabu katika kiwango cha wahusika na mandhari katika riwaya hizi teule tukiongozwa na nadharia ya uhalisiajabu. Ili kufikia malengo yetu, utafiti huu umegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza, tumetanguliza mada yetu, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, msingi wa nadharia, yalioyoandikwa kuhusu mada yetu, na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumechunguza hatua za mwanzo za uhalisiajabu ambazo ni uhalisia hakiki, uhalisia wa kijamaa hadi kufikia uhalisiajabu. Tumetambua ya kwamba waandishi waliotumia uhalisia kama vile Said A. Mohammed na K.W. Wamitila wamegeukia mtindo wa uhalisiajabu ili waweze kuyazungumzia mambo ambayo hawangeweza kuweka wazi kwa mtindo wa uhalisia.

Katika sura ya tatu, tumechunguza na kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika viwango vya wahusika na mandhari yenye matukio ya uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka.* Katika sura ya nne, tumebainisha wahusika na mandhari yenye matukio ya uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya ya *Watu wa Gehenna.*

Katika sura ya tano, tumetathmini matokeo ya uchunguzi wetu kwa kurejelea madhumuni na nadharia tete zetu. Tumetoa hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## YALIYOMO

UNGAMO ..... i

TABARUKU ..... ii

SHUKRANI ..... iii

IKISIRI ..... iv

YALIYOMO ..... v

**SURA YA KWANZA** ..... 1

1.1UTANGULIZI ..... 1

1.1.1Sifa Bainifu za Riwaya Mpya / za Kimajaribio ..... 2

1.2 TATIZO LA UTAFITI ..... 3

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI ..... 3

1.4 NADHARIA TETE ..... 4

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA ..... 4

1.6 UPEO NA MIPAKA ..... 6

1.7 MSINGI WA NADHARIA ..... 6

1.7.1 Mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu ..... 13

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA ..... 15

1.9 NJIA ZA UTAFITI ..... 20

**SURA YA PILI** ..... 22

2.0 UTANGULIZI ..... 22

2.1 VIPINDI VYA UANDISHI WA SAID AHMED MOHAMED ..... 22

2.2 VIPINDI VYA UANDISHI WA TOM OLALI ..... 23

2.3 HATUA YA MWANZO YA UHALISIAJABU ..... 24

2.3.1 Kipindi cha Uhalisia Hakiki ..... 24

2.3.2 Kipindi cha Uhalisia wa Kijamaa ..... 27

2.3.2.1 Mihimili ya Uhalisia wa Kijamaa ........ 27
2.3.3 Kipindi cha Uhalisiajabu ........ 29
2.4 HITIMISHO ........ 30
**SURA YA TATU: UHALISIA NA UHALISIAJABU KATIKA RIWAYA YA *BABU ALIPOFUFUKA*** ........ 31
3.0 UTANGULIZI ........ 31
3.1 MANDHARI NA MATUKIO YA UHALISIA NA UHALISIAJABU ........ 31
3.1.1 Maana ya mandhari ........ 31
3.1.2 Mandhari na Matukio ya Uhalisia na Uhalisiajabu ........ 32
3.2 WAHUSIKA WA UHALISIA NA UHALISIAJABU ........ 48
3.2.0 Utangulizi ........ 48
3.2.1 WAHUSIKA WAKUU ........ 49
3.2.1.1 Mhusika K ........ 50
3.2.1.2 Mzuka ........ 57
3.3.2 Wahusika Wadogo ........ 62
3.3.2.1 Delpiero ........ 62
3.3.2.2 Miyawaza ........ 62
3.2.2.3 Von Heim ........ 63
3.2.2.4 Di livio ........ 63
3.2.2.5 Mzula ........ 64
3.2.2.6 Maajuza ........ 64
3.2.2.7 Mahasimu wa K. ........ 65
3.2.2.8 Mahakimu Wakati ........ 65
3.3 HITIMISHO ........ 66

**SURA YA NNE:UHALISIA NA UHALISIAJABU KATIKA RIWAYA YA*WATU WA GEHENNA*** ... 67

4.0 UTANGULIZI ... 67

4.1 MANDHARI NA MATUKIO YA UHALISIA NA UHALISIAJABU ... 68

4.2 WAHUSIKA WAKUU ... 93

4.2.1 Mhusika Eks ... 94

4.2.2 Takosani binti Abdalla ... 97

4.3 WAHUSIKA WADOGO ... 102

4.3.1. Mishi ... 102

4.3.2 Shamsa Muhashamy (Baadayadhiki) ... 104

4.3.3. MKUU ... 105

4.3.4 Munkari ... 107

4.3.5 Hikmat ... 108

4.3.6 Watu wa Gehenna ... 109

4.4 HITIMISHO ... 111

**SURA YA TANO:HITIMISHO ... 112**

5.0 UTANGULIZI ... 112

5.1 KUHUSU MADHUMUNI YETU ... 112

5.2 UPIMAJI WA NADHARIA TETE ... 115

5.3 MAPENDEKEZO ... 118

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **TY** | - | Tafsiri Yangu |
| **NK** | - | Na Kadhalika |
| **UK** | - | Ukurasa |
| **FKK** | - | F= Florida K=1000 K = 1000 |
| **GSC** | - | Gehenna Systems Centre |
| **F.P.E.P-** | | Free Primary Education Programme |

# SURA YA KWANZA

## 1.1 **UTANGULIZI**

Katika utafiti huu, tunashughulikia uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya mpya ambazo ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Watu wa Gehenna* (2012). Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imeandikwa na mwandishi anayesifika Said Ahmed Mohamed na ambaye amechangia kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa. *Watu wa Gehenna ni riwaya* yenye muundo changamano na mwandishi wake ni Olali Tom. Waandishi hawa wameandika riwaya zingine.

Hata hivyo, katika utafiti huu tumejikita katika riwaya zao mbili *Babu Alipofufuka* (Said A. Mohamed) na *Watu wa Gehenna* (Tom Olali). Hizi ni riwaya mpya au riwaya za kimajaribio. Wamitila (2003:181) anasema kuwa, riwaya mpya hutumiwa kueleza riwaya ambayo inakiuka kaida za kawaida za utungaji na muundo wa riwaya. Anasema kuwa, riwaya za aina hii zina msuko, hadithi na wahusika wenye sifa zisizokuwa za kawaida. Kwa mfano, msuko huenda kuchanganya lugha ya msimulizi na mhusika, uakifishi huwa tofauti, wahusika hawana sifa zinazowabainisha waziwazi na hawana wasifu wa wahusika halisi.

Anaendelea kuelezea kuwa, riwaya mpya pia huitwa riwaya za kimajaribio ambayo ni dhana inayotumiwa kuirejelea riwaya iliyozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na kuakisi matumizi ya mbinu za kiubunifu za uandishi wa riwaya. Anafafanua kuwa, waandishi wa mkondo huu huwa na nia za kuziasi kaida za

kijadi za uandishi wa riwaya, pamoja na kuyapinga baadhi ya mawazo waliyonayo wasomaji kuhusu fasihi na hasa ya neno riwaya (2003:181).

Mifano ya riwaya mpya za Kiswahili ni kama vile *Bina- Adamu*! (2002) na *Musaleo! (2004)* za K.W Wamitila, *Nagona (1990) na Mzingile (1991)* za E. Kezilahabi, *Babu Alipofufuka (2002)* na *Dunia yao (2006)* za S. A. Mohamed, *Mafamba (2008)* na *Watu wa Gehenna (2012)* za Tom Olali miongoni mwa zingine. Mtindo huu wa utunzi umewezesha hali ya kukabiliana na mabadiliko kadha yanayozikumba jamii zetu za kisasa. Jambo hili linawapa waandishi wa riwaya mpya fursa ya kuyaeleza mambo ambayo hayangeweza kuelezeka kwa uwazi kwa mitindo ya kawaida.

### 1.1.1 Sifa Bainifu za Riwaya Mpya / za Kimajaribio

1. Kuna matumizi makubwa ya mitindo tofauti ya uakifishaji.
2. Msomaji wa kazi hizi aghalabu hujikuta amegumiwa na wingi wa marejeleo matini kwani urejeshi ni mwingi mno.
3. Uhalisiamazingaombwe hutumika yaani, uhalisia wa kiajabu. Kwa mfano, Mhusika 'K' katika *Babu Alipofufuka* anavyopanda Limousin.
4. Muundo ambao umevunjikavunjika.
5. Ndani ya riwaya hizi, msomaji anapambana na fikra za wanafilosofia na wanasiasa mashuhuri pamoja na vitimbi vyao.
6. Dhana ya mhusika kuwa tofauti na ilivyo katika riwaya ya jadi.
7. Mitindo ya usimulizi isiyo ya kawaida.

8. Muundo changamano unaokiuka baadhi ya taratibu na uzoefu wa uandishi wa riwaya, ambao humtumbukiza msomaji katika njia jarabati ya kumkomaza msomaji ashiriki kikamilifu na kufuatilia usimulizi kwa kina.
9. Kuna matumizi mengi ya ndoto.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Katika utafiti huu, tunachunguza jinsi vipengele vya uhalisia na uhalisiajabu vinavyodhihirika katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Tumeonyesha ni kwa nini uhalisiajabu ni njia mwafaka zaidi ya kusoma na kuzifahamu riwaya hizi mbili. Tatizo hili ni muhimu kushughulikiwa kwa vile waandishi Said Ahmed Mohamed na Olali wametumia lugha yenye ubunifu mwingi, uhusika usiozoeleka na mandhari ya kiajabu kusawiri kazi zao.Uandishi wa aina hii unahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubainisha mwelekeo wa waandishi hawa. Kuna pengo kati ya yale tunayoyajua katika uhalisia na yale ambayo hatuyaelewi katika ndoto lakini yanaonekana kama mambo halisi. Kutokana na jambo hili, tunadhamiria kuchunguza uhalisia na uhalisiajabu katika kiwango cha wahusika na uhusika, pamoja na mandhari ambamo matukio yanafanyika.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu ni:-

1. kuchunguza jinsi vipengele vya uhalisia na uhalisiajabu vinavyojitokeza katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna*.

2. kutathmini mtazamo wa waandishi hawa kuhusu suala la uhalisiajabu kama linavyojitokeza katika kazi hizi mbili.

## 1.4 NADHARIA TETE

1. Vipengele vya uhalisia na uhalisiajabu vinajitokeza katika uendelezaji wa riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.*
2. Dhana ya uhalisiajabu ndiyo mhimili mkuu wa dhamira katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.*

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Kazi ambazo tunashughulikia za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* zimewekwa katika tapo la riwaya mpya ambazo zinakiuka kaida za kawaida za utungaji na muundo wa riwaya unaozoeleka na kwa hivyo msukumo wetu wa kufanya utafiti kwa mtazamo na usomaji mpya.

Tumeamua kushughulikia mada hii kwa sababu, suala la uhalisiajabu ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Vilevile, ingawa dhana ya uhalisiajabu inahusishwa na waanzilishi wa kimagharibi, dhana hii imekuwepo katika fasihi simulizi za jamii nyingi ulimwenguni. Kwa hivyo, sababu kuu ya kuchagua mada hii ni kutaka kujua ni kwa nini waandishi hawa wameamua kutumia mtindo huu wa ukiushi wa kaida za uandishi katika kazi zao.

Kazi za waandishi hawa za hapo awali zimeshughulikiwa na wahakiki wengine katika viwango mbalimbali. Tumenuia kulipa suala la uhalisiajabu uzito unaostahili kama inavyodhihirika katika riwaya hizi mbili. Waandishi wa riwaya hizi wamethibitisha masuala ya uhalisiajabu ambayo hayatokei tu katika jamii zao, bali katika jamii nzima ya ulimwengu.

Sababu ya kuchagua mada hii pia inatokana na kuwa, tunaamini kuwa hakuna uhakiki unaoweza kudaiwa kwamba umekamilika kwa sababu wahakiki labda hutofautiana kwa mitazamo na misimamo. Pia, uhakiki hutegemea mabadiliko ya kijamii kulingana na wakati na katika maendeleo ya kihistoria ambayo kwa njia moja au nyingine huathiri maendeleo ya fasihi. Hii ndiyo sababu Hough (1962:6) anasema:

> Hakuna kazi yoyote ya uhakiki iliyokamilika wakati mmoja na ikawa ndio ukomo, kwani hutegemea historia na mazingira ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia. Fasihi ya wakati uliopita yafaa kufasiriwa upya jinsi tunavyofasili maandishi mapya, ndivyo fasihi zetu za yale ya zamani zinavyobadilika. (TY)

Tumechagua mada hii pia kutokana na pendekezo la mtafiti Nyabunga ( 2005) aliyehakiki riwaya za *Bina- Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) za K.W. Wamitila na kupendekeza riwaya mpya zihakikiwe kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu na uhakiki ushughulikie masuala mengine.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umejifunga katika kushughulikia riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001) na *Watu wa Gehenna* (2012). Waandishi hawa wameandika riwaya zingine lakini hizi mbili zinatoshea kwa mahitaji ya utafiti wetu, kwa sababu kutokana na utafiti wetu, riwaya hizi mbili zimeibuka na mwelekeo wa uhalisiajabu. Kuna kazi nyingi zilizoandikwa lakini tumeteua riwaya mbili tofauti za waandishi waliotengwa kitaifa ili kuchunguza kama kuna uhusiano wa riwaya japo wametengwa kiumri, wakati wa uandishi na pia kijiografia.

Tunatafiti kazi hizi kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu / uhalisia mazingaombwe ambayo inahusishwa na mwanzilishi wake mhakiki wa sanaa wa Kijerumani kwa jina Franz Roh (1925) na pia nadharia ya uhalisia inapohitajika. Riwaya hizi mbili zinashughulikiwa ili kutoa ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai yetu. Aidha, tunashughulikia vipengele viwili tu katika utafiti wetu. Tunachunguza wahusika na mandhari yenye matukio ya kiajabu.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Katika utafiti huu, tunaongozwa na nadharia ya uhalisiajabu/uhalisiamazingaombwe kwani tunaamini itaafiki utafiti wetu. Wamitila (2003:234) anaeleza kuwa, uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Franz Roh katika kitabu chake *Nach-expressionismus, magischer Realismus* na inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au

kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Anasema kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Walibora (2010:143) akimnukuu Abrams ( 1999) anasema:

> Istilahi ya 'uhalisiamazingaombwe' ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na hali kadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wanasukanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya.

Akielezea uhalisiajabu, Mbatiah (2001:60) anafafanua kuwa, istilahi ya uhalisiajabu inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo, mitindo ya uhalisiajabu inaelezwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa, ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokana na maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Anasema kuwa, uhalisia wa kimaajabu huhusishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka Bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia.

Kutokana na maelezo ya waandishi hawa, tunaona ya kuwa, wanauhalisiajabu hutumia sifa zinazobainisha kazi zao ingawa wana mitazamo na imani tofauti za kimsingi. Njogu na Wafula (2007:114) wanasema kuwa, uhalisiamazingaombwe ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelewa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa.

Huu ni ukweli unaobainika katika riwaya tunazoshughulikia za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* ambapo msomaji yeyote wa hadithi hizi anahisi kwamba, mambo yanayoelezwa kutokana na usawiri wa wahusika, mandhari, pamoja na usimulizi kama yasiyo ya kawaida lakini kwa hali halisi ni mambo yaliyowahi kutendeka katika jamii ila tu yanawasilishwa kwa mtindo mpya.

D'Haen (2005:191) anaeleza kwamba, uhalisiamazingaombwe ni tawi mahsusi la usasabaadaye (postmodernism), linaloonyesha sifa za usasabaadaye kama vile kujirejearejea, uziada uliopindukia uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi vilevile kumchanganya msomaji kwa makusudi na hali kadhalika kufuta mipaka kati ya dhana, vitu au hali tofauti.

Hoja kwamba Roh ndiye mwasisi wa uhalisiamazingaombwe inapingwa au kurekebishwa na wahakiki kama vile Christopher Warnes anayedai kwamba, matumizi ya awali kabisa ya istilahi ya 'uhalisiamazingaombwe' yanapatikana katika maandishi ya mshairi Fridrich Freiherr von Hardenberg, maarufu kwa lakabu ya kishairi Novalis. Warnes (2006:488) anasema kuwa, Novalis hakuikuza mno dhana ya uhalisiamazingaombwe pamoja na kwamba alikuwa wa kwanza kuitumia. Labda ndio sababu wengi humtaja Roh aliyeitumia kinadharia kauli ya uhalisiamazingaombwe mwaka 1925 kama mwasisi wa istilahi hii.

Green (2009:21) anasisitiza kwamba, mitindo na misingi ya uhalisiajabu katika fasihi kimatendo ilikuwa ya awali zaidi hasa katika kaida za Kiramsia (Romantism) ambapo masimulizi "yaliweka sambamba matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida".

Walibora (2010:146) anasema kuwa, uhalisiamazingaombwe unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama mkabala wa kuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka , kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha na ingawa ni mkabala wa kifasihi unaonasibishwa zaidi na waandishi wa Amerika Kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za janibu mbalimbali zikizungumzwa kwa dayalojia hii.

Waandishi katika Afrika Mashariki waliotumia uhalisia katika kazi zao za awali kama vile Ngugi wa Thiong'o mwishowe wameishia kusombwa na wimbi hili la

uhalisiamazingaombwe hasa katika riwaya yake ndefu ya '*Wizard of the Crow*' (2005). Katika riwaya yake ya Kikuyu: *Murogi wa Kagogo* (2004:212), tunapata uhalisiajabu ambapo mhusika mmoja anapoongea, sauti yake inasikika ikitoka ndani ya kioo. Vivyo hivyo, baadhi ya waandishi wa lugha ya Kiswahili kama vile; Said Ahmed Mohamed, E. Kezilahabi, K.W. Wamitila na Tom Olali wametekwa na 'mvuto wa ajabu' wa uhalisiamazingaombwe.

Wamitila (2003), katika '*Influence or Intertextuality*? A *comparative study of Kezilahabi's Nagona* and *Mzingile a*nd Juan Rulfo's *Pedro Paramo*; anabainisha jinsi fasihi ya Kiswahili inavyotoa mwangwi wa fasihi ya Amerika Kusini kwa kufumbata sifa za uhalisiamazingaombwe. Yamkini makala za Wamitila za miaka ya 1991 (*Nagona* and *Mzingile*: Kezilahabi's metaphysics) na 1999 (Unlocking Katana Mkangi's Walenisi) ni miongoni mwa makala za kwanza kabisa kugusia uhusiano huu wa kimtindo kati ya fasihi ya Afrika Mashariki ya tapo hili na kwingineko.

Walibora (2010:145) anasema kuwa, ingawa inaweza kudaiwa kwamba kazi za Shaaban bin Robert kama vile *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1961) zilikuwa na sifa fulani za uhalisimazingaombwe, Wamitila anasisitiza mchango mkubwa wa Euphrase Kezilahabi katika kuleta upya katika ulingo wa fasihi ya Kiswahili. Anaongeza kuwa, ulinganisho wa fasihi ya Kiswahili na fasihi ya janibu mbalimbali kama vile unaotekelezwa kwenye makala za Wamitila ndio njia mwafaka ya kuandamana ili kuuwezesha uhakiki kuwa na dayalojia ya

kilimwengu ambayo fasihi ya Kiswahili yenyewe tayari inashiriki kwa mapana na marefu.

Khamis (2005), anazungumzia dalili za riwaya ya Kiswahili kuchukua sura mpya kwenye makala yake '*Signs of New Features in the Swahili Novel'*. Khamis anataja mvuto wa mtindo wa kimajaribio kama unavyobainika katika riwaya kama vile *Nagona* na *Mzingile (Kezilahabi)* , *Babu Alipofufuka* (Said A Mohamed), na *Bina –Adamu*! (Wamitila) kama kielelezo cha kuibuka kwa mitindo mipya katika fasihi ya Kiswahili.

Walibora (2010:147) anasema kuwa, maoni ya Khamis (2005) na yale Williams katika kitabu chake *Marxism and literature* (1999) yanashabihiana ambapo Williams anasema kwamba mikakati ya kimajaribio katika sanaa hudhamiria kuakisi ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii. Aidha, kuibuka kwa riwaya za usasaleo kulibadili hali iliyokuweko hata zaidi (Williams 1995:1).

Marquez kama mwasisi wa uandishi wa kisasaleo anafikiriwa na wasomaji wengi wa kimagharibi kuwa mwandishi wa kifantasia. Kinyume na madai haya, yeye mwenyewe amedai mara nyingi kuwa ni mhalisia ambaye anajaribu kuelezea jinsi hali ilivyo nchini mwake Kolombia kwa njia ya kweli iwezekanavyo. Williams anasema kuwa, Marquez (1980) anaelezea kuhusu wafanyakazi wa Macondo ambao wanaandaa mgomo. Baadaye uvumi unaenezwa kwamba serikali imewaua mamia ya wafanyakazi. Kisa hiki kimetajwa kuwa cha kifantasia kuliko vingine

kwa sababu tukio la kihistoria linapuuzwa na kuwasilishwa kama uvumi tu. (Williams 1995:3).

Nchini Chile, Allende (1985) ndiye mwandishi aliyeandika kazi zake za kwanza kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu kuandika riwaya ya *The House of the Spirits*, inayohusu familia inayopitia mabadiliko ya kisiasa. Kama mtangulizi wake, anatumia uhalisiajabu kuyaangazia masuala ya nchi yake yakiwemo siasa. (Encarta Encyclopaedia: 2002).

Kulingana na Wamitila (2002:117), waandishi wanaohusishwa na mkondo huu katika hatua za mwanzo ni wa Marekani ya Kusini. Hawa ni waandishi kama Gabriel Garcia Marquez wa Colombia, Juan Rulfo na Carlos Fueres wa Mexico, Isabel Allende wa Chile, Alejo Carpenter wa Cuba, Miquel Asturias wa Guatemala na wengineo.

Wamitila anaendelea kuelezea kuwa, kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabu au maajabu. Anatoa mifano ya wahusika wanaopatikana kwenye riwaya ya Marquez, *One Hundred Years of Solitude* ambao wanaishi chumba na choo bila kutambua na pia kupaa angani na shuka ya jirani. Anasema kuwa, wahusika wengi wa Juan Rulfo katika *Pedro Paramo* ni wafu na msimulizi wa hadithi anaendelea kusimulia hata baada ya kufariki. Katika riwaya ya *The House of the Spirit*s ya Allende, kuna msichana

(Rosa) anayezaliwa akiwa na nywele za kijani na rangi ya uso wa manjano (Wamitila 2002:118).

Waandishi wa kazi hizi wanayakiuka matarajio ya uhalisia wa kisimulizi kimakusudi. Kwa mfano, katika riwaya ya S.A Mohamed ya *Babu Alipofufuka* , K anaposafiri kwenda ulimwengu wa pili anapitia kwenye mizizi ya mmea, magari yanapaa hewani, anapambana na babu asiyeonekana na dereva n.k. Mpaka uliopo kati ya yanayowezakana (mambo halisi) na yasiyowezekana unafutwa. Kazi hizi zinavunja muundo wa kikawaida wa utanzu kama njia ya kuzuka na istiara ya miundo ya mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya ulimwengu (Wamitila 2002:117).

1.7.1 **Mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu**

Kutokana na kazi za Danow (1995), Cooper (1998), Zamora (1995), (1993) na Encarta encyclopedia (2002), huu ndio muhtasari wa baadhi ya mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu.

1) Matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya.
2) Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

Ni muhimu kutaja kwamba, katika utafiti wetu, si mihimili yote ambayo itatumika. Itakayotumika ni ile tu, itakayofaa zaidi kufafanua riwaya tunazozichunguza ili kuweza kuangaza dhana ya uhalisiajabu.

Katika nadharia ya uhalisiajabu, ndoto huchukua nafasi muhimu sana kwani matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Malcolm, N. (1959:94) anaeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa ndoto huambatana na picha na mawazo na matukio kama kwamba yanatokea katika hali halisi.

## 1.8 **YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

Waandishi Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Juan Rulfo wa Meksiko, Gunter Grass wa Ujerumani, Said Ahmed Mohamed wa Zanzibar, Euphrase Kezilahabi wa Tanzania, Kyallo Wadi Wamitila na Tom Olali wa Kenya ni baadhi ya waandishi waliotengwa kitaifa na kilugha lakini wanaunganishwa na uamuzi wao wa kuandika riwaya yenye mtindo usiokuwa wa kawaida, mtindo wa uhalisiajabu.

Alexander, M. (1990:127), anaeleza kuwa, uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasaleo inavyotuhimiza kuwaza upya juu ya dhana ya kimapokeo

kuhusu riwaya ya uhalisia ya karne za kumi na nane na kumi na tisa. Uhalisiajabu unatuhimiza kufikiria ufaafu wa baadhi ya mitindo tofauti ya uandishi kuangazia mada tofauti tofauti. Baadhi ya waandishi wanajadili uhusiano kati ya historia na masimulizi ya ubunifu, huku wakitumia visaasili katika kazi zao.

Okri, B. (1991) anaingilia uwanja wa uhalisiajabu na kueleza kuhusu maisha nchini Nigeria. Anaeleza kuwa maisha ya uhalisi na ya ndoto hayatofautishwi katika nchi hii ya Abiku. Maisha nchini Nigeria ni kama ndoto na hayana mantiki. Anasema kuwa, kipengele hiki cha kifantasia kinafaa sana katika kufafanua hali mbaya katika taifa la Nigeria.

Gromov (2002:3-4) anaelezea kuwa, usasaleo ni njia ya kuufinyanga ukweli wa maisha kwa njia tofauti na jinsi ilivyozowewa. Kulingana naye, uhalisiajabu ni kitengo cha usasaleo ambacho kimefanikiwa kuzungumzia maswala ya kileo. Kutokana na maelezo haya, tunaonelea kuwa wasanii hawautumii uhalisiajabu kiajali, bali kwa lengo la kuangazia hali ya jamii wanamoishi.

Tasnifu hii itakuwa mojawapo ya kazi za kwanza kabisa kushughulikia riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imeshughulikiwa na Magaju *(2004)* katika tasnifu yake akiilinganisha na riwaya ya *Bina –Adamu!* akitumia nadharia ya uhalisiajabu.

Kuna waandishi watangulizi wa uwanja huu wa uandishi miongoni mwao ni Topan katika tamthilia ya *Aliyeonja Pepo* (1970) na Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Watunzi hawa wanakaribia kutumia mbinu uhalisiajabu. Hata hivyo, ingawa waliweza kubuni hali za kiajabuajabu walifanya hivyo kwa kuchota mitindo yao kutoka malighafi ya utamaduni wa kiamerika na kiafrika ambapo tunajua tangu kale dhana za miungu, mashetani, pepo na nyinginezo zimekuwepo (Nyabunga: 2005).

Katika uhakiki wao wa tamthilia ya *Mashetani*, Kimani na Chimerah (1999:200-201) wanatujulisha kwamba Juma na Kitaru wameamua kucheza mchezo wa shetani na binadamu ili waielewe barabara hali yao ya sasa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa jumla. Katika mchezo huu, kuna mgogoro uliopo baina ya shetani (Juma) na binadamu (Kitaru). Kitaru anafahamikiwa na migogoro, migongano na mikinzano ya kijamii katika ndoto. Kwa njia ya ndoto, anaifahamu mifumo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii na jinsi inavyomwathiri yeye na jamii nzima. Kutokana na mchezo huu, tunaona jinsi ndoto kama mhimili wa uhalisiajabu inavyotumika kufunulia binadamu mambo anayokumbana nayo.

Mkangi katika *Mafuta* (1984) ametumia uhalisiajabu mwingi katika kazi hii. Mtue anasema kuwa, ameshasikia visa vya majini, lakini alichopatana nacho kimeshinda vyote. Hii ni baada ya kujipata katika mandhari ya kushangaza na wala hakujua alivyofika pale. Ti anamweleza kuwa wakati mwingine huenda mtu akajikuta juu ya mbuyu, huku nguo zake zinaning'inia kitangaani. Mtue anamaka

na kumuuliza Ti kama yeye ni ibilisi au jini. Matukio ya kiajabuajabu na ambayo ni ya kushangaza na kuduwaza yanajitokeza riwayani.

Riwaya za *Nagona* na *Mzingile* za E. Kezilahabi pia zimeandikwa kuhusiana na uhalisiajabu. Wamitila anaziona riwaya hizi kama zinazopita ufahamu wetu wa ulimwengu na anapendekeza kwamba riwaya za aina hii zichunguzwe upya labda kwa mtazamo wa kifalsafa ili kuleta upya katika ulingo wa fasihi ya Kiswahili. (Wamitila 1991:66). Katika riwaya zake, *Bina–Adamu*! (2002) na *Musaleo!* (2004), Wamitila anatumia uhalisiajabu kimakusudi kwa kutaka kuyaangalia masuala ya kijamii kwa njia ya kiajabu na ya kipekee.

Walibora (2010:143-157) ameshughulikia uhalisia na uhalisiamazingaombwe kati ya The *Tin Drum na Dunia Yao.* Anasema kuwa lipo pengo la zaidi ya miongo minne kati ya kuchapishwa kwa *The Tin Drum* (1965) na *Dunia Yao* (2006), na kwa kujua au kwa kutojua waandishi hawa wawili wamo katika 'dayolojia' ambayo twaweza kuifasili kama mawasiliano au mazungumzo yanayowezesha kuigana na kuathiriana kimtindo na kimaudhui. Kimsingi, fasihi moja inasema au inajibizana na nyingine au kutoa mwangwi wa mambo yanayofanana au kulingana na yale ya fasihi nyingine.

Magaju, J (2004), katika tasnifu yake, ameshughulikia riwaya za *Babu Alipofufuka (2002)* ya S.A Mohamed na *Bina-Adamu*! ya K.W. Wamitila akitumia nadharia ya uhalisiajabu. Katika uhakiki wake, ameonelea kuwa,

uhalisiajabu unatokana na hali mbili zinazopingana lakini una misingi yake katika uhalisia.

Nyabunga (2005), katika tasnifu yake amehakiki riwaya za *Bina-Adamu* ! (2002) na *Musaleo!* (2004) za K.W. Wamitila. Nadharia iliyoongoza utafiti wake ni nadharia ya uhalisiajabu ambapo matukio yanasawiriwa kiajabuajabu, ya kuogofya na kutisha. Uhalisiajabu ni mtindo wa riwaya wa hivi majuzi unaopiku njia za kimapokeo za uandishi wa fasihi ya Kiswahili na usawiri wa jamii.

Mugwika (2012), katika tasnifu ya shahada yake ya uzamili ameshughulikia dhana ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* (2008). Katika tasnifu yake, anaelezea jinsi mwandishi ametumia uhalisiajabu kama njia mojawapo inayotumiwa katika uchimuzi.

Kuhusu riwaya ya kimajaribio, Olali (2010:82-98) anathibitisha kuwa, riwaya kadha za Kiswahili zilizoandikwa tangu miaka ya 1990 hadi leo zinadhihirisha muundo usio wa kawaida zikilinganishwa na muundo wa riwaya ya kihalisia. Anaonyesha kuwa, katika riwaya za Kiswahili kuna ukiushi wa kisarufi ambao husababisha tofauti katika utaratibu uliozoeleka hadi kwa ule usiozoeleka.

Olali (2010:83) anaonyesha muundo katika *Babu Alipofufuka* ambao ni mtindo katika riwaya za kimajaribio unaoingiliana na mambo ya kifantasia, kiajabu na kiubadausasa na wenye mitindo mipya ya uandishi wa kimajaribio ambao

unajaliza katika masuala nyeti ya kimaudhui kama ya utandawazi, dini, filosofia na siasa za kimataifa. Msisitizo wake wa sifa za riwaya hizi ni uandishi unaokiuka kaida za kiitikadi, utathmini wa ujumi kwa ndani na uvunjaji kaida za lugha kwa namna inayompa mwandishi uhuru zaidi.

Anakiri kuwa msuko wa riwaya hizi ni changamano na hudhihirisha mbinu rejeshi kwa kiwango kikubwa. Kulingana naye, msuko wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* upo katika vitengo viwili, yaani wa mhusika mkuu K na wa mzuka wa babu yake. Pindi mzuka wa babu yake uanzapo kufuata maisha ya K, mambo ya kiajabu yanaanza kutendeka kama vile kupotea kwa chakula cha mbwa wake 'Doggy', kuendesha na aidha kusumbuliwa na mzuka uliomtawala mara kwa mara. Licha ya hayo, mizuka ya watu ambao alitendea mabaya hapo awali ilimrudiarudia, hawa walikuwa watu halisi ambao yeye pekee ndiye aliyewaona. Kutokana na fasihi simulizi za jamii za Wakikuyu (na zinginezo) mizimu huwatokea waliohai hasa ndotoni ili kujaribu kuelekeza jamii inapokosa mwelekeo.

## 1.9 **NJIA ZA UTAFITI**

Utafiti wetu ni wa maktabani. Ili kufanikisha utafiti huu hatuna budi kujihusisha na mbinu mbalimbali ili kutimiza madhumuni yetu. Kwanza, tumesoma riwaya mpya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* ili kuzielewa kwa undani kwa lengo la kuzichanganua vilivyo. Tumesoma pia riwaya nyingine za kimajaribio

zilizoandikwa na waandishi mbalimbali ili kutathmini sifa za riwaya za kimajaribio.

Tatu, tumesoma kuhusu yaliyoandikwa kuhusu riwaya za kimajaribio (riwaya mpya), kuhusu uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya za Kiswahili ili kujua pengo lililoachwa. Uchunguzi wetu umetuwezesha kuchangia mada yetu kwani riwaya hizi zimeonyesha upeo wa juu wa dhana ya uhalisiajabu.

Nne, tumesoma yaliyoandikwa kuhusiana na mwelekeo wa kihakiki wa uhalisia mazingaombwe katika vitabu na makala mbalimbali na pia mtandao. Maelezo haya yametuwezesha kuelewa nadharia hii kwa kuangazia jinsi misingi ya madai yake inavyotumiwa katika uhakiki wa fasihi na kwa njia hiyo kufanikisha ufahamu wetu na utafiti wetu. Pia, tumetafuta ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu, wahadhiri mbalimbali wakiwemo wanafasihi na wanaisimu na pia wasomi wa isimu. Tajriba yetu na pia ya jamii zetu kuhusu uhalisiajabu zimetoa mchango mkubwa katika kubainisha uhalisiajabu. Tumeweza kuwahoji baadhi ya waandishi wanaotumia uhalisiajabu na kupata maoni yao kuhusu msukumo uliowafanya kutumia mwelekeo huu.

# SURA YA PILI

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ya pili, tunashughulikia vipindi vya uandishi wa waandishi Mohammed Said Ahmed na Olali Tom, na vilevile kuangazia hatua zilizopigwa na waandishi kutoka uhalisia na kufikia uhalisiajabu. Katika kuangazia hatua hizi, tunaweza kuelewa ni kwa nini waandishi waliokuwa wakitumia mtindo wa uhalisia hakika wamegeukia uandishi wa uhalisiajabu.

## 2.1 VIPINDI VYA UANDISHI WA SAID AHMED MOHAMED

Said A. Mohamed alizaliwa mwaka wa 1947. Alizuka kwenye ulingo wa fasihi kwa hadithi fupi zake zilizotangazwa kwenye idhaa ya Kiswahili ya BBC kuanzia miaka ya sabini na kuchapishwa baadaye. Aliwahi kufunza vyuo vingi katika Afrika Mashariki vikiwemo Chuo Kikuu cha Moi (Eldoret) na Chuo Kikuu cha Nairobi kabla ya kuteuliwa Profesa katika Chuo Kikuu cha Osaka, Japan. Baadaye alienda kufunza katika Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani.

Kama mwandishi anayesifika, ameandika riwaya, hadithi fupi, tamthilia na mashairi. Baadhi ya kazi zake za mashairi ni; *Sikate Tamaa* (1980), *Kina Cha Maisha (*1984) na *Jicho la Ndani* (2002). Tamthilia zake ni pamoja na; *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) *na Posa za Bi Kisiwa* (pamoja na Kitula Kingei) (2007). Pia, aliandika riwaya ambazo zilizingatia mtindo wa kiuhalisia na zilizomfanya kuwa msanii maarufu zaidi katika mandhari ya fasihi ya Kiswahili. Riwaya hizi ni pamoja na

*Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988) na *Tata za Asumini* (1990).

Hata hivyo riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia yao* (2006) ni sehemu ya mabadiliko makubwa katika mkabala na mkondo wa kisanii unaokiuka kaida za uandishi zilizozoeleka. Alijiunga katika jitihada za kubuni riwaya za Kiswahili katika usasabaadaye akichanganya mitindo tofauti kama vile uhalisiajabu, kuhoji katika kupinga ukoloni mamboleo na utandaridhi kutokana na matatizo ya ndani kwa ndani na pia kutokana na kani zinazotoka nje katika mtazamo wa Afrika Mashariki. Katika riwaya yake ya hivi karibuni ya *Nyuso za mwanamke* (2010), alirudia uandishi wake wa uhalisia akiangazia wanawake waliofanikiwa hata ikiwa wanakumbana na changamoto nyingi zikiwemo masuala ibuka, yenye migogoro mingi ya kumdunisha mwanamke. Pia ameandika *Arusi ya Buldoza* (2005) na hadithi nyingi fupi.

## 2.2 VIPINDI VYA UANDISHI WA TOM OLALI

Mwandishi Tom Olali alipata shahada yake ya kwanza (1994) na ile ya MA katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi (1997) na shahada ya PhD huko London (2004). Mwandishi Olali ameandika riwaya za *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* (2012) akizingatia uandishi wa riwaya ya kimajaribio.

## 2.3 HATUA YA MWANZO YA UHALISIAJABU

Katika sehemu hii, tunadhamiria kuangalia kipindi cha uhalisia hakiki, kipindi cha uhalisia wa kijamaa na pia kipindi cha uhalisiajabu ili tujue ni kwa nini waandishi tuliochagua kazi zao wakaamua kutumia mtindo wa uhalisiajabu na kuasi mitindo iliyozowewa.

### 2.3.1 Kipindi cha Uhalisia Hakiki

Wanauhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wanaotumia uhalisia, wanapendelea wahusika, mandhari na matukio ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii. Kulingana na Wafula na Njogu (2007:62), uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Waandishi hawa wanaelezea kuwa, huko Ufaransa kuna waandishi kama vile Flaubert (1850), waliotumia dhana ya uhalisia kuelezea kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo na uigaji wa mazingira wanapopatikana wanadamu. Wanafafanua kuwa mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetik* (Ujumi) alitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka.

Wamitila (2002:114) anasema kuwa, kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisia, zinatarajiwa kuwa kama akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika kwa kiasi kikubwa. Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa

kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao na kusawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Anasisitiza kuwa, uhalisia unapinga au kukataa aina yoyote ya majaribio. Katika hali hii, tapo hili linaweza kulinganuliwa na ulimbwende ambao unampa mwandishi nafasi ya kuyasawiri matukio, mandhari na wahusika ambao huenda wasiafikiane ki-uaminifu na uhalisi wa jamii yake.

Kwa kuchukua mtazamo huu, kazi nyingi za kiuhalisia zinaishia kuyakwepa matukio, wahusika na mandhari yasiyo ya kawaida. Muundo wa sentensi za kazi ya kiuhalisia pamoja na uteuzi wa msamiati ni sahili na uteuzi wa mkabala wa kisimulizi hutiliwa maanani sana.

Wamitila (2002:114) anaonelea kuwa, waandishi wa kihalisia huchukulia kuwa picha zinazopatikana kwenye kazi zao pamoja na yaliyomo huwiana na ukweli wa jamii zinazohusika. Msimamo huu unaelekea kuamini kuwa *'ukweli'* na *'uhalisi'* ni vitu vinavyoweza kuelezeka kwa urahisi jambo ambalo si kweli.

Kwa kiasi kikubwa tunaweza kusema kuwa jinsi za kuusawiri na kuuelewa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Katika msingi huu, inawezekana kusema kuwa kila kizazi huwa na uhalisia wake. Watu mbalimbali na wasomaji hawawezi kuungalia uhalisia kwa njia sawa. Anachokiona msomaji mmoja kama uhalisia huenda mwingine asikione kama uhalisia.

Akitoa mfano kutoka riwaya ya E. Kezilahabi ya *Rosa Mistika,* Wamitila (2002:117) anaeleza kuwa riwaya hii imeandikwa kwa kiasi kikubwa kwenye misingi ya uhalisia lakini kuna tukio ambalo linazua maswali. Rosa anapoletewa maji ya sumu, anayamwaga nje ya nyumba na asubuhi anakuta kichuguu kikubwa. Jambo hili kwa msomaji mmoja laweza kuwa la kihalisia lakini kwa mwingine liwe la kiajabu.

Katika tamaduni za jamii ya Wakikuyu, mtu anapopatwa na maafa yanayofuatana huaminika kuwa, amelaaniwa na lazima 'kafara' itolewe ili aondolewe laana hiyo. Tamaduni za jamii nyingi zina mila na itikadi tofautitofauti na wenye imani hizo ni wao tu wanaozielewa. Kwa mfano, maafa ni matukio ya kimaumbile kwa jamii ya kikristo na wakati mwingine hutokana na adhabu ya Mungu binadamu anatenda dhambi. Kizazi kilichoko pia hakielewi baadhi ya mila na itikadi za jamii zao. Kwa hivyo, kinachoonekana kama uhalisiajabu kwa jamii moja huenda kikaonekana jambo la kawaida katika jamii nyingine.

Akieleza upungufu wa nadharia ya uhalisia hakiki, Khaemba (1999:14) anaonelea kuwa, uhalisia hakiki ni muhimu tu kwa kadri unavyoangazia kujimudu katika harakati za mwanajamii kupambana dhidi ya hali dhahiri. Ni wazi kuwa nadharia ya uhalisia hakiki ina upungufu kwani haielezi jinsi binadamu anavyopambana na nguvu za ajabu dhidi ya uwezo wake. Pengine ndipo waandishi Said A. Mohamed na Tom Olali waliamua kuandika kazi tulizoziteua kwa mtazamo wa

kiuhalisiajabu, ili waweze kueleza mambo ambayo hayangeweza kuelezeka kwa kutumia uhalisia.

### 2.3.2 **Kipindi cha Uhalisia wa Kijamaa**

Kwa mujibu wa Suchkov katika Khaemba (1999), nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilizuka pale wanajamii waling'amua kwamba mahitaji ya jamii yanatawaliwa na mahitaji ya kiuchumi na wala si fikra za watu au majaaliwa. Wakielezea nadharia ya uhalisia wa kijamaa, Wafula na Njogu (2007:61) wanasema:

> Ni mbinu ya utunzi na uhakiki inayomzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa kuwepo kwa ulimwengu na maana ya ulimwengu ule. Waundaji wa nadharia hii wameathiriwa na mtazamo wa Kimarx kuhusu ulimwengu na historia. Maxim Gorky, mmojawapo wa waasisi wa uhakiki wa kijamaa, anasema kwamba mambo yote mazuri yanayotamanika ulimwenguni yameumbwa au kuelezwa na binadamu.

#### 2.3.2.1 **Mihimili ya Uhalisia wa Kijamaa**

Wafula na Njogu (2007:68) wanasema kuwa, katika tungo zinazoongozwa na uhalisia wa kijamaa, mwandishi huongozwa na mihimili ifuatayo:

i) Wahusika wa kimaendeleo. Hawa ni wahusika wanaonuia kupindua na kuibadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika wenye nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao.

ii) Pamoja na kusawiri matukio ya kihistoria, wahusika hutekeleza matendo ya kitabaka. Hufanya hivi kimakusudi au bila kufahamu.

iii) Uhalisia wa kijamaa huzingatia maslahi ya makabwela.

iv) Binadamu huonyesha kiuyakinifu wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi, hupuliziwa uhai mfano wa wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao.

v) Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu. Hii inamaanisha kwamba mtu atakuwa mshindi au ni mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote.

v) Lugha inayotumiwa katika uhalisia wa kijamaa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii.

Kutokana na maelezo haya, nadharia ya uhalisia wa kijamaa inapatikana na upungufu wa kuwa imekolea itikadi sana hivi kwamba masuala ya kisanaa yanaweza kupuuzwa. Lugha inayotumiwa inaweza kuwa kavu ikakosa matumizi ya kunga za kifasihi kama vile sadfa, taharuki na tamathali za usemi.

Kutokana na maelezo haya, pengine ndipo waandishi tuliochagua kazi zao wakapata msukumo. Sanaa ya kijamaa ni sanaa ya kitaifa kwa kuwa haiangazii mazingira mahsusi ya kihistoria ambamo jamii imepitia.

Nadharia hii inapendekeza namna ya kutatua matatizo ya kijamii ili kuunda jamii mpya itakayokuwa bora zaidi na ikawa sharti kanuni za nadharia hii zizingatiwe na waandishi na wahakiki. Tunaweza kusema kuwa kipindi hiki kiliwaathiri waandishi Said A. Mohamed na Tom Olali katika uamuzi wa uandishi wao

wakitumia usanii unaokiuka kaida za uandishi wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

### 2.3.3 Kipindi cha Uhalisiajabu

Said A. Mohamed alianza uandishi wa uhalisiajabu baada ya kuandika vitabu vingi katika mtazamo wa uhalisia. Naye mwandishi Olali katika riwaya zake (*Mafamba* na *Watu wa Gehenna*) amefuata mtindo huu wa uhalisiajabu na kuna uhusiano mkubwa wa kazi zake na zile za Said A Mohamed (*Babu Alipofufuka* na *Dunia Yao*). Wamitila (2003:274) kuhusu uhalisiajabu anasema:

> Sifa hizi ni za kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane kama ya kawaida tu. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo mno.

Said A. Mohamed (2006:71) anasema kuwa, alijua wakati wa sanaa ya uhalisia imepita na alipoanza uandishi, hangeandika vingine nje ya uhalisia, kwani kanuni za uhalisiajabu hazingekubalika. Zamora na Faris (1995:3) wanasema kuwa,waandishi wa kiuhalisiamazingaombwe wanasomeana kazi zao na kuitikiana wenyewe kwa wenyewe nje ya mipaka yao ya kitaifa na kilugha katika njia ambazo zimeathiri kazi zao na matukio ya hivi karibuni katika mada na mikakati ya kiuhalisiamazingaombwe.

Waandishi wanaotumia mtindo huu wa uhalisiajabu wanafanya hivi ili waweze kuzungumzia masuala ambayo hayangeweza kuzungumziwa kwa uwazi kwa njia

ya kawaida au kwa mtindo wa kiuhalisia. Waandishi Said A. Mohamed na Tom Olali wamezingatia mtindo wa kiuhalisiajabu kwani waliona kuwa mitindo ya uhalisia hakiki na uhalisia wa kijamaa haikuweza tena kuyaakisi masuala ya jamii na hivyo wakataka kuziba pengo kwa kutumia mtazamo huu katika kuangazia masuala ibuka yanayokabili mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa mtindo wa kipekee unaosheheni ugothi, uhalisia wa kiajabu na nguvu za giza, ili kuwezesha msomaji kuelewa dunia tunamoishi leo. Mihimili ya uhalisiajabu ni kama ilivyoorodheshwa katika sura ya kwanza.

## 2.4 **HITIMISHO**

Katika sura hii, tumezungumzia vipindi vya uandishi wa waandishi Said A. Mohamed na Olali Tom. Tumezungumzia vipindi vya uhalisia hakiki, uhalisia wa kijamaa na kutokana na mihimili yake, tumepata upungufu ulio wafanya baadhi ya waandishi waliozoea mtindo wa uhalisia kuingilia mtindo wa kiuhalisiajabu.

# SURA YA TATU

# UHALISIA NA UHALISIAJABU KATIKA RIWAYA YA *BABU ALIPOFUFUKA*

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumedhamiria kuuwekea msingi mjadala wa utafiti wetu. Tumebainisha mandhari yenye matukio na wahusika wa kiajabu tukitumia mihimili husika ya nadharia ya uhalisiajabu. Fauka ya hayo, tumeangazia uozo katika jamii huku tukitoa mifano ili tuchunguze kama uhalisiajabu umefanikiwa pale uhalisia umelemewa.

## 3.1 MANDHARI NA MATUKIO YA UHALISIA NA UHALISIAJABU

### 3.1.1 Maana ya mandhari

Mandhari ni sehemu muhimu sana katika fasihi ya aina hii. Katika mandhari ya uhalisiajabu, matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Njogu na Chimerah (1999:46) wanasema kuwa mandhari ni mahali au makazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi. Ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio, na yanahusu mahali wanamokaa wahusika hao; mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao; na nafasi zao za kitabaka.

Kulingana na Wamitila (2003:108), dhana hii hutumiwa kurejelea wakati wa kihistoria na mahali pa hadithi, yaani mazingira ya kijamii au kijiografia

wanamojikuta wahusika wa kifasihi. Huwa ni nguzo au msingi muhimu katika uandishi wa kazi ya kifasihi.

Kutokana na fasiri hizi, tunaonelea kuwa mandhari ni nguzo muhimu ya uhusika (ya kuimarisha matendo ya wahusika) kwa kuwa matendo yao yanafungamana na mazingira wanamojikuta. Kufahamu mandhari hutusaidia kuwaelewa wahusika, tabia zao, hisia zao, imani, misukumo yao, lugha zao na hata maumbile yao.

Mandhari pia hufungamana kwa kiasi kikubwa na maudhui na dhamira inayohusika. Kwa mfano, katika mandhari ya kitajiri ndimo tunamowaona wahusika wa tabaka la kibepari na kimwinyi na katika mandhari ya kimaskini tunawakuta wafanyikazi, wakulima, watamba-na-njia na wengine. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* tunachunguza mandhari ya kiuhalisia na mandhari ya kiuhalisiajabu.

### 3.1.2 **Mandhari na Matukio ya Uhalisia na Uhalisiajabu**

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* tunapata mandhari yaliyochanganyika hivi kwamba kuna mandhari ya kiuhalisia na ya kimazingaombwe, ambapo wakati mwingine inakuwa vigumu kutambua au kubainisha mipaka ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa kinjozi au ndoto. Mandhari ya uhalisiajabu hutokea ili kuwakilisha uhalisiajabu fulani katika ulimwengu wa kawaida. Mandhari yenye uhalisia yanapatikana mwanzoni mwa riwaya ambapo mhusika K anaanza katika ulimwengu halisi na kisha anaingia katika ulimwengu wa kimawazo, na kurejea

tena katika ulimwengu halisi. Mandhari haya yanabadilika hivyo hivyo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Katika riwaya nzima, uhalisiajabu umetokea mara nyingi kuanzia wakati maisha ya mhusika K yameingiliwa na mzuka wa babu yake.

Katika Kasri lake, K amefuga jibwa kwa jina Doggy, ana watumishi wengi akiwemo Biye na Walinzi. Katika mandhari haya ya uhalisia, matukio ya kiuhalisiajabu yanatokea. Kwa mwezi mzima, sahani na chakula cha Doggy vimekuwa vikitoweka kila mara anapoletewa Doggy na watumishi. Katika ulimwengu wa mazingaombwe, babu Mzuka ndiye anayeondoa chakula anachowekewa Doggy na kuwapa majirani wanaolala njaa, kwani wakati wa akina babu, mbwa walipewa chakula baada ya watu wote kushiba (uk.2).

Katika ulimwengu halisi, K anawalaumu watumishi wake kwa kumuondolea mbwa chakula. Kwa sababu hii, anawafuta kazi watumishi kila wakati na kuajiri wengine. Said A. Mohamed ametumia tukio hili la kiajabu ili kukashifu vitendo vya ubadhirifu na kutojali kwa viongozi katika nchi za ulimwengu wa tatu. Viongozi wa serikali na matajiri kama vile K huwajali wanyama hata kuliko binadamu wanaowahudumia. Wananchi hulala njaa na wengine hufa kutokana na njaa.

Matukio ya kiajabu yanaendelea kumtokea K katika kasri lake. K anashikwa na kikohozi yabisi, kichefuchefu kinafuata na kisha tumbo linamchiririka kwa sauti

ya mnung'uniko. Baada ya K kujizoazoa msalani, anajikuta ameenea uchafu msambani, makalioni, mapajani na miguuni na ghafla masikio yake yanazibukia kicheko kizito cha tashtiti kinachokuja kwa sauti yake yeye mwenyewe na kujaa ndani mote. Mambo mageni yanakuwa yakimwandama kila siku hasa anapokuwa na wasiwasi au hamaki. Kicheko anachokisikia kina sauti inayofanana na yake mwenyewe lakini hajui kinatoka wapi (uk.8).

Mwandishi katika riwaya hii ya *Babu Alipofufuka* anakashifu ubinafsi na uozo katika jamii unaoletwa na watu kama vile K wanapopata cheo au uongozi. K anaingilia utamaduni mpya; lazima aende maskanini na saa tatu ya usiku aende Neo-Casino kila siku. Babu Mzuka anaeleza:

> Siku hizi K, kinying'inya changu, anaweza kuketi meza moja na watu ambao miaka michache iliyopita ilikuwa miko kukaa nao. Mazimwi, aliwaita. Akatangaza vita nao akisaidiwa na nyuki.. Aaaa, lakini ule ulikuwa wakati mwingine... (uk.10).

Mwandishi anamulika yanayopatikana ulimwenguni, hasa katika nchi za Afrika. Wakati viongozi wanatafuta kura ili waingie mamlakani, wanakashifu viongozi walioko mamlakani lakini pindi tu wapatapo mamlaka wanakuwa wabaya zaidi.

Ingawa kasri la K linapatikana katika mandhari halisi, ni la ndotoni tu. Muundo wa umbo lake ni wa kifantasia tu. Kasri hili lina mabawa kama eropleni na hata mkewe Kikuba anaishi katika bawa mojawapo. Ni kasri kubwa mno lenye vyumba vingi sana; hata babu Mzuka anamwuliza K ni kwa nini mtu anayeishi

miaka themanini tu (akijaaliwa) awe na majumba mia moja yenye vyumba mamilioni (uk. 15). Katika ulimwengu halisi, baadhi ya marafiki zake hasa Delpiero, Von Heim, Di Livio na Miyawaza wanalikejeli jumba hilo na kumwambia ni Kasri kama la Dracula. Mtunzi anawakashifu viongozi kama K kujijengea majengo ya kifahari huku wananchi wanyonge wakiishi katika makazi duni, mitaa ya mabanda na yenye umaskini mwingi. Mwandishi anasema kuwa hamu ya K siku hizi ni kuwa na kitu cha kiyeyeyeye. Kitu cha kipekee (uk. 15).

Katika mandhari haya ya kitajiri, kasri lake limejaa watu kama utitiri, walinzi wa siri, walinzi wa dhahiri, makarani, wapishi, wasafishaji, wahudumubustani, waduhushi-mbwa-na-farasi, madereva, mayaya na madobi. Ukweli ni kwamba watu hawa wote hupotelea mbele ya jicho la K mpaka pale anapomhitajia mmojawao na kufumbua akili ya kompyuta kuweza kumwita na kumtuma haja yake (uk.16). Katika mandhari haya, tunaona athari za utandawazi. Mhusika K anatumia mtandao kufanya karibu kila kitu, haoni hata umuhimu wa kuongea na kushirikiana na watumishi wake katika kasri hili. Yeye huzungumza na kompyuta yake.

Mandhari ya kiuhalisiajabu yanajitokeza pale K anapojiandaa kupelekwa Neo-Casino katika Limonsin yake. Mandhari ya Neo-Casino ni ya kihalisia, kuna pia Limonsin na dereva wake Mzula. Tukio la ajabu linatokea pale dereva huyu Mzula, anaibuka ghafla na kumfungulia mlango wa nyuma. Vilevile, walinzi wa

K wawili wanachimbuka ardhini walikokuwa wamefukilika na kuja juu haraka wanaposikia **Limonsin** ikinguruma (uk.17).

Katika Limonsin lake, K anaziona nyuso za watu zenye matuta kudhihirisha ghadhabu kwake. Mwanzoni zilikuwa nyuso mbili badala ya moja, kisha zikawa nne na hatimaye zikawa elfu (uk.18, 27, 55). Said A. Mohamed ametumia mawazo ya K kama mandhari ya uhalisiajabu. Kutokana na kule kutowahudumia wananchi vilivyo, mawazoni mwa K anawaona mahasimu wake wakimfuata. Hawa ni wale wanaopinga uozo wa viongozi; wanaendelea kuongezeka maradufu na hivyo linakuwa onyo kwa K kuwa hawezi kamwe kuukimbia ukweli.

Katika Limonsin lake, dereva Mzula anamwendesha K kuelekea Neo-Casino. Mandhari haya ya kihalisia ghafla yanabadilika na kuwa ya ndotoni au ya kiuhalisiajabu, pale ambapo kioo kinachomtenganisha dereva na K kinafunguliwa kinyume cha kanuni. K anaingia katika ulimwengu wa ndoto na kutanabahi kuwa dereva anayeendesha gari sasa hakuwa dereva wake Mzula. K anafikiria ni kiinimacho (uk.19).

Tangu babu Mzuka aingilie maisha ya K, hajawahi kumtoka na anamwandama kila mahali. Mzuka anamwambia K ameingilia dunia yao na amekuja kumtatulia mambo na ndiyo maana sura yake si muhimu kuliko kauli yake (uk. 22). Katika mandhari ya ndotoni, babu Mzuka anamweleza K ukweli kuhusu uozo wake na jinsi alivyomtafuta sana. Katika safari halisi ya kwenda Neo-Casino, kuna

mandhari ya ulimwengu halisi pale Limonsin linapita katika janibu za wakwasi na mabanda yenye umaskini mwingi. Barabara yenyewe ina sehemu kubwa mbovu na sehemu nyingine nzuri (uk. 27). Wakiwa safarini babu Mzuka anamfanya K atambue mabaya anayoyafanya. Mzuka anamwambia kuwa hata kama anakoga katika mabafu ya maziwa na asali, dunia inayomzunguka imejaa udhia. Barabara ni mbovu lakini gari la K lina vioo vya giza visivyopenya mwangaza wala risasi. Yeye K anajikinga na hataki kuona mazingira yalivyoharibika, badala yake anavaa miwani asione hata maskini wakiombaomba. Babu Mzuka anamfunulia kuwa ni yeye anayesababisha tabia mpya ya tumbo kuendesha na maajabu yote anayoyaona. K hakujua kama yu ndotoni au yu macho, kama yu duniani au ahera (uk.23).

Safarini, tunapatana na mandhari ya uhalisia; magari mfululizo yanapishana, mapikipiki, vitutu, baiskeli na wenda-kwa-miguu. Pembeni mwa njia vibanda na vijumba vimejifunika gubigubi guo la giza. Kuna umaskini mwingi na watoto ndio wanaouza samaki, vitumbua na kusujudia vumbi ardhini kwa kusinzia (uk.26). Wanapozuiwa kupita kutokana na wingi wa magari, tukio la kiajabu linatokea katika mazingira haya ambapo K na dereva wake Mzula wanazungukwa na watoto viditia wanaogonga vioo na kunyoosha mikono kuomba pesa. Vijana nao wameghadhibika na kufinyanga ngumi ambazo kila baada ya muda zinaishia kupiga bodi la Limonsin. Wote wamejaa mori na macho yao yakiwaka moto wa kisasi. Vimada nao wanavalia mini na vitopu na kujipodoa huku wakipita wakitoa ishara za mapenzi na K anatambua baadhi ya sura zao (uk 27). Mtunzi anatumia

uhalisia kudhihirisha uozo na umaskini unavyokita mizizi mitaani na wakati huo huo matajiri wanakaa kwenye makasri na kuendesha magari ya kifahari na maisha yenye starehe nyingi. Hii ndiyo maana wananchi wanajawa na hasira na wamo tayari kulipiza kisasi.

Uhalisiajabu unadhihirika wakati K anapobonyeza chombo fulani cha kisasa kinachosababisha mapikipiki yaruke angani kufika, na Limonsin nalo linaruka likiongozwa na kulindwa na mapikipiki ya polisi nyuma, mbele na ubavu huu na huu. Gari linaruka na kutua langoni mwa Neo-Casino (uk. 27). Mtunzi anatumia uhalisiajabu huu kudhihirisha jinsi hali ilivyo katika mataifa ya ulimwengu wa tatu. Kuna umaskini na uhitaji mkubwa miongoni mwa wananchi walio wengi kutokana na uongozi mbaya unaoongozwa na ubinafsi na ufisadi. Vilevile mtunzi anakashifu uozo katika jamii hasa uasherati ambao hata viongozi kama vile K wanauendeleza. Kwa sababu ya uongozi mbaya na ugavi mbaya wa mali, kuna chuki dhidi ya viongozi na uozo katika jamii. Viongozi hupewa ulinzi mkali dhidi ya raia wanaopigania haki zao.

Mtunzi anaturudisha katika ulimwengu halisi katika jengo la Neo-Casino. Jengo hili ni la kifahari na la kisasa. K anafurahi kuwa angalau wageni wakija, sasa watakuwa na cha kuwaonyesha badala ya magofu, vibanda, vumbi na uvundo (uk 29). Kuna marafiki wa K katika jengo hili wanaomsubiri. Hawa ni pamoja na Delpiero, Di Livio, Von Heim, Miyawaza na watukufu wengine. Kupitia kwa kompyuta, walikuwa wamepata habari kuwa alikuwa amezungukwa na wahuni

kule njiani na hivyo ikabidi waje kumlaki huku wamevaa hofu, wasiwasi na kujali. Tunaona athari za utandawazi ambapo viongozi hujikinga na mabaya yanayoweza kuwapata lakini raia hawana ulinzi wowote.

Kule Neo-Casino uhalisi na ndoto vinachanganyika. K anapeperuka kwa mapozi na fahari huku akilazimisha kicheko cha ukubwa. Anafurahia kupanda juu zaidi na kupata raha aliyotafuta kwa miaka mingi. Aina za vyakula vinavyoliwa Neo-Casino ni vya kiajabu sana. Ni vyakula vya utamaduni wa kigeni usio wa asilia ya utamaduni wa K. Vyakula hivi vyaweza kupatikana tu katika mawazo ya mhusika. Kuna chatu wa kutokosa, kijibwa kichanga kilichochomwa na kupambwa majani na maua, nyama ya nyangumi aliyekaangwa, mende waliochemshwa na pilipili manga, makombe ya samaki wabichi na vinginevyo. Hii ni ajabu kwa sababu vyakula hivi havina asili katika Afrika kama tunavyotarajia katika mazingira ya K ya kiafrika. Mtunzi anatumia mhusika wa kiajabu (Mzuka) kukashifu vitendo vya kuiga vya K hata kwa vyakula visivyo vya utamaduni wake. Mzuka anauliza kwani kuna siri gani kwenye kina cha chini kabisa cha akili za watu wenye utamaduni huu (uk.36). Akimjibu babu Mzuka, K anasema hakuna siri, ila tasnifu ya mwanadamu kutafuta starehe katika sanaa ya vyakula na kufazaishwa na uzuri wa ladha. (uk.30). Majibizano haya ya K na babu Mzuka katika mandhari haya yanawashtua wenzake kwani hawaoni anayejibizana na K. Kutokana na majibizano haya mpaka kati ya roho na mwili, mpaka kati ya kuwepo na kutokuwepo, mpaka kati ya kuonekana na kutoonekana,

na vilevile mpaka kati ya Afrika na Ulaya unavunjwa au umeondolewa. Hii ni kwa sababu K amekumbatia utamaduni wa kigeni na kuiga kila kitu ( uk.38).

Mandhari ya FKK ni ya kihalisia na K na wenzake wanaenda kustarehe huko ingawa babu Mzuka anamuonya K kutohudhuria. Mzuka anamwambia K waite klabu hiki Giningi au Uchawini badala ya FKK. Uasherati na uozo wa aina zote unapatikana hapa kinyume na utamaduni wa Kiafrika (uk. 39-45).

Katika riwaya hii ya *Babu alipofufuka,* tunaona mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa ikivunjwa. Hii ni kwa sababu wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja. Kwa mfano, Von Heim anauliza ni mpaka lini Waafrika watafumbua macho. Anadai kuwa:

> mambo mengine ni mageni ndiyo lakini ni kawaida tu... FKK ni upeo wa utamaduni. Hivi leo ukitaka kuuangalia upeo wa sanaa tazama mwili wa mwanadamu katika utupu wake. Ukitaka kuona hivyo nenda FKK.... Ili muweze kutambulikana, kukubalika na kuheshimika, mkubali mambo yatakayokuwa yanakuja hatua kwa hatua. Mkubali biashara kwa upana wake na utamaduni wa msingi wa kufungua milango. Msingi wa haki. Na haki si haki za kawaida tu, bali pia haki za maarifa, haki za watu kufanya wapendavyo... haki ya kuvaa wapendavyo, haki ya kuzaa na mume maiti, haki ya kuzalishwa kwa sindano... haki na haki na haki... (uk.44).

Kutokana na madai haya, K, anamuunga mkono Von Heim kuendelezwa kwa mradi wa FKK, jambo ambalo linamkera babu Mzuka. Mtunzi ametumia uhalisiajabu huu kumulika jinsi viongozi wanavyounga na kutengea miradi kama FKK ambayo haileti manufaa yoyote kwa nchi pesa nyingi. K pia anafuja pesa za umma anapompatia mpenzi wake Zuhura Mapozi shilingi milioni sabini kuanzisha duka la peremende. Mzuka anamuonya K kuwa kesho vitukuu na vinying'inya vyao vitazama katika mashakili makubwa kuliko FKK. Kutakuja tupwa takataka za sumu, ardhi na viwanja vyao kuuzwa na haya yataleta matatizo makubwa (uk.47).

Wakati K anafika ofisini, tukio la kiajabu linatokea asijue kama ni uhalisia au ni ndoto. Ofisi inapofunguliwa K anaona kikundi cha watu wenye mapanga na kinapasua kuta za ghorofa. Walinzi wanapojaribu kukizuia kinageuka mvuke na kutoweka. K anapatwa na wasiwasi mwingi kwani anazingirwa na walinzi na kuta za ghorofa na hivyo kudhani yuko salama. Ajabu ni kuwa hata sekretari wake Mashavu hakuwaona mahasimu hao badala yake aliwaona walinzi tu (uk.68-69).

Kwa kutumia uhalisiajabu, mtunzi anadhihirisha kuwa, mahasimu wa viongozi huongezeka kila uchao na wana nia ya kulipiza kisasi kutokana na uongozi mbaya na kuwaacha wananchi watawaliwe na umaskini mkubwa. Hivyo, harakati za wanyonge kutafuta haki haziwezi kuzuiliwa kamwe.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, kuna mandhari ya mahakama ya ndotoni ambapo Mzuka anamsomea K mashtaka yake (uk.74). Baadhi ya mashtaka ni:

- Kuwageuza watu panya wa majaribio katika maisha yao.
- Ukatili wa kuwanyang'anya watu mashamba yao.
- Uharibifu wa kuvunja nyumba za wananchi mijini na vijijini bila kuwalipa fidia.
- Ufisadi wa maofisa watendakazi waliopokea hongo.
- Mfumo makini wa kilimo uliofisidiwa kwa ajili ya watu fulani kujipatia sifa.
- Watoto kupewa elimu ya jembe miaka yote.
- Uozo wa maadili ambapo picha za wasichana uchi '*nudist*' zimetundikwa kutani na kuwafurahisha kina K.
- Kesi ya Bw. Sururu aliyechukuliwa Bi Zuhura mapozi na K.

Akiwa ndotoni, babu Mzuka anamchukua K na kumpeleka katika safari ya kumrejesha nyuma katika maisha yake ya awali. Mzuka anampeleka K dunia nyingine ili aweze kusoma. Baadhi ya matukio ya uhalisiajabu yanajitokeza. K anavua miwani na kuvaa figu la sura ya mchwa, kisha anajiua kwa kujikaba roho; halafu anasimama tena mwenyewe kama anavyoagizwa. Kisha, Mzuka anamgusa K kichwani na anageuka mchwa, huku naye Mzuka akigeuka mchwa. Wote wanatumbukia ardhini kupitia kwenye mizizi ya gugu la ukoko; kisha K ananyanyua mkono na kuruka juu na kupaa nje hewani na kutua chini kama ndege. Wote wanaanguka karibu na kisima cha Makalbi (uk. 82-86).

Mtunzi anatumia uhalisiajabu kwa kumbadilisha K ili apate nafsi nyingine ya kuweza kuingia dunia tofauti na kuweza kusoma. Kulingana na nadharia ya uhalisiajabu, uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na uwenyeji huonekana zikiingiliana. Wakati binadamu yumo ndotoni, anayaona na kuyapitia mengi yanayomfanya achunguze matendo yake.

Katika safari hii, K anapitishwa kwenye mazingira halisi alimokulia. Anapatana na raia ambao kawaida wanasema kina K hawawasikilizi.Wanapita lakini hawawaoni wanaopaswa kuwahudumia. K anaona kama wamechukua miaka elfu moja katika safari hii (uk.88). Anakutana na Mussa lakini Mussa hamtambui kwa sababu amevaa figu. Kwa kutumia uhalisiajabu, mtunzi anamulika viongozi na jinsi wanavyopuuza maendeleo vijijini na kutorokea mijini. Vijijini kuna umaskini mwingi na wanakijiji wanamkagua K kutoka kichwa hadi miguuni na kutoweka huku wakimwita *"Protausi."* K anaona lile jina kama kejeli (uk.96). Said A. Mohamed anatumia mbinu rejeshi kumkumbusha K alikotoka na kuyapitia.

K anakumbuka jinsi Bw. Sururu alivyomsaidia alipokuwa amekwama matopeni na Limonsin yake. Badala ya amlipe kwa wema anamnyang'anya bibi yake Zuhura Mapozi na kumnunulia nyumba jijini awe karibu naye. Kisa hiki kinatupeleka kwenye hadithi ya ngamia na msafiri jangwani aliyekuwa kalala ndani ya hema. Mtunzi anaeleza alivyosema ngamia:

> Nipishe nitie kichwa tu, haya! Nipishe nitie shingo tu, vyema!
> Nipishe nitie kifua tu, sawa! Nipishe nitie miguu tu, hewalla!

> Nipishe nitie mkia tu, ndiyo! Kutahamaki mwenye hema kapigwa teke kabaki kutafunwa na baridi nje (uk 99).

Kutokana na kisa hiki tunaona jinsi uhalisiajabu unavyofungamana na sanaajadi kama vile visasili. Mtunzi anatumia hadithi hii kuonyesha jinsi baadhi ya binadamu hawana shukrani. Baada ya kusaidiwa na kufanikiwa, huwasahau waliowasaidia na wakati mwingine kuwadharau wakisahau kuwa wanaweza kuwahitaji tena. Viongozi hutoa ahadi za uwongo lakini wakipata vyeo, wanawasahau waliowachagua.

K anarudishwa katika mazingira alimokulia. Hapa anakutana na Maajuza mhusika wa kihalisia nyanya yake. Maajuza anawasimulia wajukuu wake, K akiwemo, simulizi za zamani. Anawaeleza kuwa, simulizi za zamani zinasema kuwa roho zinapokwisha toka ndani ya miili ya watu hugeuka vivuli vinavyoishi, ambavyo havionekani kwa urahisi lakini huathiri maisha ya binadamu wote, matajiri na maskini. Anasimulia kuwa mizuka inaweza kuwasiliana na walio hai katika ndoto ndoto au ndoto macho na inaweza kuleta balaa kwa mtu binafsi, ukoo, au hata jamii nzima iwapo imepoteza mizani ya mwenendo wake.

Maajuza anasisitiza kuwa makungu huja katika maumbo mengi kama vile paka, nyoka, mijusi, vinyonga na kadhalika, na katika miji yao kuna giza ambalo huwafanya waghadhibike na huamsha taharuki katika mioyo ya binadamu. Taharuki hizi huogopesha na hivyo huwafanya walio hai kushirikiana nao kusafisha dhambi na dhambi zikiondoka, vijiji vyao huangazwa kwa mwanga wa

ajabu ambao huangaa hata kwa walio hai. Wakati anaposema kuwa wanaotenda maovu huandamwa na wasioonekana wakitaka kulipiza kisasi, K anachukuliwa mzimamzima na kudidimizwa ardhi ya saba na ukweli wa hadithi hii ya Maajuza. Sababu ni kuwa haya ndiyo matukio ya ajabu anayokutana nayo kila siku (uk. 118-120).

Kutokana na simulizi hii, tunaona matukio ambayo hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Kawaida aliyekufa hawi hai tena na haingilii maisha ya waliohai. Kwa kutumia mtindo huu wa uhalisiajabu, tanzu za fasihi simulizi huweza kutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Mtunzi anajenga wahusika wenye nafsi mbili. Katika nafsi halisi, K haamini mizuka lakini alipobadilishwa nafsi yake na kuwa mzuka anayaelewa matukio haya kabisa kwani yanamjia kila wakati.
Akiwa safarini anapitia nchi za Kata, Amani, Ncha, Nusunjia na nyinginezo. Baadaye anaona umati wa watu wakiabudu masanamu makubwa. Katika mandhari haya ya kuabudia, kuna sanamu la paka wa Kijapani anayeitwa Manekineko, tai la Kimarekani na Gwaru kubwa ajabu la Euro. Sauti ya Mzuka inasikika ikisema:

> wacheni nyinyi watu, wacheni... Manekineko kila siku linaita halikimbizi pesa...Gwaru la tai hunyakua tu, halitoi sadaka. Na Euro ni ufupisho wa uroho... (uk. 131).

Mtunzi ametumia matukio haya ya kiajabu kuonyesha athari za utandawazi. Waafrika wanaiga kila kitu kutoka Ulaya na pia wameanza kuabudu miungu kutoka mataifa yaliyoendelea. Hawathamini vitu vyao vya kiasili.

Akirejeshwa katika dunia yao, K anapitishwa baharini kwenye mahakimu wakati. Hapa tunaona mandhari ya kiuhalisiajabu ya mahakama, kwani lazima ahukumiwe. Mzuka anamwambia kuwa, hana uchaguzi wa kuamua, lakini K anaendelea kukataa mashtaka. K anawaona watu watano wakongwe wenye madevu na hawakuonekana binadamu wa kawaida.

Mtunzi kwa kutumia mahakama na mahakimu wa kiuhalisiajabu anadhihirisha kuwa lazima mwishowe kutakuwa na hukumu kali kwa viongozi wanaokosa kuwahudumia raia kwa njia ipasavyo kwa kuongozwa na ubinafsi. Babu Mzuka anasema hata wakifa, watoto wao, jamaa zao na hata vivuli vyao vitahukumiwa kwani hiyo ndiyo kanuni ya wakati. Babu Mzuka anamwambia K kuwa, sasa amemaliza kazi yake (uk.144).

Mahakimu wanamlisha K kiapo cha Kimasai na Kikamba; kiapo cha Kithitu au Ndundu. Kiapo cha mchanganyiko wa vitu vya ajabuajabu kama vile karafuu maiti, vipande vya unyoya na mangisi, mizizi ya mimea ya makaburini, majani ya miti ya mwarubaini, unyoya wa korongo wa Uganda na magamba ya samaki ya telapia wa ziwa Nyasa na ziwa Rudolf la Kenya na ziwa Tanganyika na nduaro wa Bahari ya Hindi ya Zanzibar (uk.133-145).

Mtunzi anatumia kiapo cha aina hii kuonyesha kuwa tayari K ameikosea jamii na nchi nyingi kwa maovu aliyotenda. Kwa mfano, wakati misitu inakatwa ovyo, watu pamoja na wanyama na mazingira hata ya nchi jirani huathirika.

Baada ya kula kiapo, K anafunguka macho na anaona jinsi barabara zilivyoharibika, watu wakongwe na waliokonda, na vijana wamekimbilia Uingereza na Amerika kubadilisha jinsi zao na kuuza misuli yao katika utumwa mpya. Wengine wamekuwa Wasomali, Warwanda au Waburundi. Wanaonekana wakitafuta kitu kisichoonekana na nyuso zao zinaonyesha kukata tamaa. Hakuna anayewapa sadaka hata wakiomba. Dunia yote imejumuika kuwadharau (uk. 146-147).

Hatimaye, K anarudi katika ulimwengu halisi katika kasri lake na anakuta Doggy wake na wanakumbatiana. Anashtukia amenyang'anywa mamlaka, hana walinzi na watumishi wote wameondoka. Huko Neo-Casino hakaribishwi tena na mwishowe anatolewa kutoka kwa kasri lake na vitu vyote kuuzwa. Anawakumbuka wanawe (Kidawa na Bamkubwa) na mkewe Kikuba ambaye ameshageuka kuwa mwendawazimu. Mwishowe K anajinyonga na kufa. Akiwa pepo, anajaribu kuwafikia watoto wake ila inakuwa vigumu (uk. 165-168).

## 3.2 **WAHUSIKA WA UHALISIA NA UHALISIAJABU**

### 3.2.0 **Utangulizi**

Kulingana na Baldic (2001:70), neno wahusika linatokana na kazi ya Theophratus; *The Characters;* katika karne ya tatu kabla ya Kristo. Akielezea mhusika, Wamitila (2003:123) anasema:

> Ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:45), wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii ambayo yaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, wanaotambulishwa na mhusika au msimulizi na huwakilisha sifa tofauti zinazobainika kupitia kwa matendo yao. Dhima kuu ya wahusika katika kazi ya kifasihi ni kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa kushirikisha matendo yao, hisia, mazungumzo na mawazo yao. Wahusika hudhihirisha wasifu wa binadamu katika hali halisi kwa kuwa wanawakilisha binadamu wa kawaida. Wahusika pia huwa nguzo kuu ya kusukuma hadithi mbele. Wanaendelea kusema kuwa, uhusika ni umithilishaji wa vitendo vya viumbe wa hadithini na vile vya viumbe katika ulimwengu razini. Vitendo vya viumbe hao husababishwa na kuingiliana kwao na mazingira ya ubunifu, kama ambavyo vitendo vya viumbe razini huwa vinasababishwa na

maingiliano baina yao wao wenyewe na mazingira yao, ambayo ni razini. Ili kuelewa uhusika wa wahusika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kama ilivyodhamiriwa na mwandishi Said Ahmed Mohamed, tutategemea usimulizi wenyewe.

Katika riwaya hii ya *Babu Alipofufuka,* mtunzi amechanganya wahusika halisi na wale wa kimazingaombwe. Wahusika wengine wanabadilika kutoka wahusika halisi na kuwa wa kiuhalisiajabu. Matukio mengi ya kiuhalisiajabu yanatendeka wakati mhusika anapolala na yumo ndotoni. Nadharia hii ya uhalisiajabu ina mhimili kuwa labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndimo yumo ndotoni. Uhusika wa jadi unajengeka kwenye misingi ya uhalisi wa kijamii ambapo wahusika wanawakilisha binadamu katika ulimwengu halisi. Aidha, wahusika majagina wana maumbile na nguvu za kiajabu na wanatambuliwa kwa urahisi kutokana na sifa zao. Wengine wamo na nguvu za kiungu kama vile Lwanda Magere na Fumo Liyongo.

### 3.2.1 **WAHUSIKA WAKUU**

Wahusika wakuu hutawala kazi ya kifasihi kwani wanahusika katika utendaji wa matukio muhimu na wanawakilisha dhamira na maudhui ya kazi husika, wakieleza wahusika wakuu, Njogu na Chimerah (1999:41) wanasema:

> Hawa ndio nguzo za riwaya na ndio wanaosheheni hadithi nzima. Ndio wanaoisukuma riwaya mbele, kwa sababu matendo na migogoro yote muhimu inawahusu. Dhamira kuu ya mwandishi hujitokeza kupitia kwao, na msimamo

> wa mwandishi kuhusu dhamira, matukio na vitushi vya hadithi hujibainisha kupitia kwa matendo na maneno yao. Mwingiliano wao na wahusika wengine ndiyo mbinu ya kufafanua dhamira kuu.

Katika kipengele hiki, mtunzi ametumia wahusika wakuu wawili wa kiajabu sana kwani mhusika ana uwezo wa kuwa na nafsi mbili. Mhusika wa kihalisia anabadilika na kuwa wa kimazingaombwe. Katika riwaya hii kuna mhusika mkuu K katika uhalisia na mhusika Mzuka wa babu yake mawazoni mwa K akiwa ndotoni. Mwandishi amewaumba wahusika hawa ili kudhihirisha ukweli kwa wasomaji kuhusu nafasi zao katika jamii.

3.2.1.1 **Mhusika K**

Kuanzia mwanzo wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* kuna nafasi ya mhusika wa kihalisia K anayeingiliwa maisha yake na pepo au mzuka wa babu yake. Mzuka anaingilia maisha ya K na mara matukio ya kiajabu yanaanza kutokea. Kwa mfano; kwa mwezi mzima sahani na vyakula vya Doggy vinatoweka kiajabu kila mara Doggy anapoletewa chakula na watumishi. Pia K anaanza kupatwa na kikohozi yabisi, kichefuchefu na kutibukwa na tumbo. Masikio yake pia yanazibukia kicheko kizito cha tashtiti, kinachokuja kwa sauti yake yeye mwenyewe na kujaa ndani mote. K anaudhika na matukio haya (uk 6-9).

K anaonyesha kutopendezwa na viongozi wabinafsi na wafisadi wanaonyanyasa wananchi hapo mwanzoni. Anawaita mazimwi na kukashifu vitendo vyao. Hata

hivyo anaota ndoto akiwa mdogo kuwa, siku moja atafanikiwa apate cheo na awe na Limonsin. Ni msahaulifu kwani anapopata cheo, anasahau ahadi yake na kuona huo ni wakati mwengine. Kwake anaona fahari kuendelea kukwea miti na kutaka kuruka juu kugusa mbingu bila ya mbawa. Hakumbuki wanyonge na maskini. Anaamini kwamba watu wote lazima waamini kama anavyoamini yeye, kuwa hakuna mbora mwengine zaidi ya PROTEUS. Proteus ni mhusika kama K, ambaye ni kiongozi ambaye amepewa jukumu la kuwalinda na kuwahudumia watu hivyo "Protect us." K anaamini yeye ni Proteus wa pili. Anasema kuwa hata Proteus akiingia gizani kujificha, lazima akatafutwe kuombwa kuja kuleta wokovu katika kila jambo (uk. 11)

K ni mwenye kiburi na anajiona yeye ni Proteus wa kutegemewa na hajui akifa watu watafanyaje. K anajibidiisha awe Proteus, mhusika wa kiajabu, ambaye ana uwezo na nguvu zaidi. Mtunzi anasema:

> Porteus hawezi kufa. Anaweza kujigeuzageuza tu. Kwa kweli, mara ngapi mwenyewe PROtEUS anasema hafi? Anaweza kuwa mti mkubwa badala ya Bahari ya Hindi. Anaweza kuvua ngozi ya nyoka na kuvaa ya panya au ya fisi na kinyume chake. Aaah... kazi kubwa wamefanya akina K! Kazi ya kumhasi kila mwanamme.... Leo, kwa hivyo katika msitu mpya na komba wapya, imekuwa rahisi kwa kugeuza uso kutazama upande mwengine bila pingamizi yoyote. Leo wanaweza kukaa meza moja na mazimwi (uk. 11).

Mtunzi ameandika jina la mhusika Proteus kwa njia tofauti; PROTEUS, Proteus, pRoteus, PROtEus, PrOtTeus na porteus. Mabadiliko katika uandishi wa jina hili yanadhihirisha uwezo wa binadamu wa kubadilikabadilika au kujigeuzageuza na kuwa mhusika tofauti kabisa. K amebadilika kitabia, kihadhi na kimawazo. K ni msahaulifu kwani, anawasahau watu na utamaduni wake na kuiga mambo ya kigeni. Akiwatazama aliowaita mazimwi awali, anaona kumbe sura zao zinafanana na yake.

Anafurahia marafiki wake wapya Delpiero, Miyawaza, Von Heim na Di Livio. Anashirikiana nao kuitendea maovu jamii anayoiwakilisha, wanashiriki katika unyakuzi wa ardhi, kuuza bidhaa duni kwa bei ya juu, kuchimba dhahabu na almasi, kutisha watoto weusi na kutumia mili yao kufanya majaribio katika maabara, kucheza kamari, kufurahia mchezo wa mbwa na wasichana na pia kunajisi wavulana na kueneza virusi vya unajisi wake katika miili ya vijana hawa. Anawalinda wageni hawa watende maovu haya na kwa hivyo hata wakifumaniwa si chochote (uk. 13-14).

K ni mpenda raha na kila usiku saa tatu lazima aende Neo-Casino kufurahi na wenzake. Anaishi katika kasri kubwa lenye mabawa kama eropleni. Kasri hili mnaishi mkewe Kikuba na limejaa watu kama utitiri, walinzi wa siri, walinzi wa dhahiri, makarani, wapishi, wasafishaji, wahudumu bustani, waduhushi-mbwa-na-farasi, madereva, mayaya na madobi. Watu hawa wote hupotelea mbele ya jicho la K mpaka pale anapomhitajia mmojawao na kufumbua akili ya kompyuta

kuweza kumwita na kumtuma haja zake. Kupitia kwake, tunaona athari za utandawazi kwani, rafiki wa karibu wa K ni kompyuta.

Anapoingiliwa na Mzuka, anaanza kuona mambo ya kiajabu. Anaona dereva wake Mzula akibadilika na kuwa Mzuka. Anaona walinzi wakichimbuka kutoka ardhini na pia anaziona nyuso za watu zenye matuta kudhihirisha ghadhabu kwake.Nyuso hizi zinaendelea kuongezeka. Hawa ni mahasimu wake wanaopinga uozo wa viongozi na ni onyo kwa K kuwa hawezi kamwe kuukimbia ukweli. Anapoendeshwa na dereva Mzula, anapitia kwenye barabara zilizoharibika lakini hajali. Anaona Mzula akiwa na mgongo wa ajabu, kisogo kama sura ya fuvu, nyuma fuvu na mbele mgandamo wa nyama, na ngozi ambayo imekunyaakunyaa na mwili ukiwa upongoo kamili. Maajabu anayoyaona yamo mawazoni tu, kwani dereva wake Mzula haoni maajabu haya. Ana mazoea ya kuingia katika majadiliano na babu yake Mzuka. Aliwahi kumwambia asimzonge kwa mazingaombwe na kuwa aliyekufa hafufuki kwani babu yake alikufa zamani. Anaendelea kushtuka kwani anaihisi na kutambua sauti ile na kuwa inafanana na yake. Amejikinga na kujizungushia walinzi, gari lake la kifahari lina vioo vya giza visivyopenyeza mwangaza wala risasi. Anatambua kuwa ana mahasimu wengi wanaotaka kulipiza kisasi na hivyo anavaa miwani asiwaone na pia asione mazingira yalivyoharibika (uk. 23-27).

K ana tabia ya kuwaona watu wasiyoonekana na wengine. Wakiwa safarini na Mzuka, anaona mtu wa kiajabu; mwenye kifua wazi na anayevaa chupi iliyoroa

damu chapachapa; damu yenyewe inafufurika kutoka pahala fulani kichwani mtu huyu anasimama katikati mwa njia (uk. 25). Ni mwenye hasira hasa anapowaona maskini wakikaribia Limonsin yake kuomba pesa. K ni mwenye hasira na anapozuiwa kupita kwa sababu ya msongamano wa magari, anamkemea dereva wake na kumwambia aote mbawa na aruke. Anasikia kicheko cha yule mfu na mara gari lake linazungukwa na watu lakini dereva wake hasikii kicheko wala kuona mtu yeyote. K sasa kama mhusika wa kiuhalisiajabu anabonyeza chombo fulani cha kisasa kinachosababisha mapikipiki kuruka angani na Limonsin kuruka likiongozwa na kulindwa na mapikipiki ya polisi pande zote (uk.27). Hizi ndizo athari za utandawazi. K ni mmojawapo wa viongozi katika ulimwengu wa tatu ambako, wachache ndio wenye mali lakini maskini ni wengi, na hivyo chuki dhidi ya viongozi hawa inadhihirika nyusoni mwa wanyonge.

K ni kiongozi anayewathamini wageni kuliko wenyeji. K mhusika halisi katika jengo la kifahari na la kisasa la Neo-Casino anafurahi kuwa wageni wakija sasa watakuwa na cha kuwaonyesha badala ya magofu, vibanda, vumbi na uvundo. K anajali na kuwatambua wageni kuliko raia. Ghafla anaingiliwa na Mzuka; na kwa sauti ya chura, anakashifu kitendo cha kiu ya ukubwa. Inasemekana kuwa K anafurahia kuendelea kupanda juu zaidi na kupata raha aliyoitafuta miaka mingi. Akiwa mdogo aliota ndoto iliyomfanya aamini kwamba siku moja angeweza kugusa mbingu kwa mikono yake.

K pia ni mwacha mila na mwacha mila ni mtumwa. Anaiga utamaduni wote wa kigeni. Chakula anachokula sasa sio cha asili ya Kiafrika. Anakula chatu wa kutokosa, kijibwa kichanga cha kuchomwa, nyama ya nyangumi aliyekaangwa, kombe la mende waliochemshwa, makombe ya samaki wabichi na vyakula vingine vya kiajabu sana. Vyakula hivi vinamghadhibisha babu Mzuka (uk. 36).

K ni kiongozi fisadi. Anafuja pesa za umma kwa kuanzisha miradi isiyo na manufaa kwa raia. Akishirikiana na wageni, wanaanzisha klabu kwa jina FKK, ambapo watu watakuwa wakijifurahisha katika uasherati. Anapounga mkono mradi huu, hafikiri kama watoto wake wanaweza kunaswa hapa. Tunamwona bintiye Kidawa akifanya uasherati katika klabu hii. Mzuka anamuonya kuwa hata wakivaa miwani, vitukuu na vinying'inya vyao vitaathirika baadaye, na ni lazima hukumu itawaangukia (uk 42-45). Akiwa ndotoni, anaona viwiliwili vizima na anamkumbuka Sururu. K ni mhusika mkatili anayewanyanyasa wanyonge, anamnyang'anya Sururu bibi yake Zuhura Mapozi huku akimpeleka mjini awe akijistarehesha naye (uk. 61).

Katika safari yake na babu Mzuka, K anahisi kwamba wamechukua miaka elfu moja ilhali safari yenyewe imekuwa ya mawazoni na ni fupi sana. Katika uhalisiajabu, huu ni mvunjiko wa mahali na wakati (uk. 94). Kuondolewa raha zake na kupelekwa safari isiyo na maana kwake ni jambo linalomuudhi. Anataka aishi miaka mia nne na hivyo anaanza mazoezi ya kuimarisha siha yake. K anawakejeli maskini na hana utu. Ananing'iniza mfuko wa plastiki wenye shilingi milioni tatu

kufanyia mazoezi na anampatia Doggy wake 'cornflakes' wakati maskini wanalala njaa. Anawatelekeza mkewe Kikuba na watoto wake (uk. 64-66).

K ni mhusika mwenye nafsi mbili. Anabadilishwa kutoka nafsi ya uhalisia na kuingizwa ulimwengu wa uhalisiajabu ili aweze kusoma. Hii ni kwa sababu anakataa kusoma haraka. Analazimishwa kuvaa figu la sura ya mchwa, kisha kujiua kwa kujikaba roho, kuanguka chini na kufa. Anaguswa na Mzuka na kugeuka mchwa na anapata uwezo wa kupitia chini kwenye mizizi ya gugu la ukoko. Baadaye anapata uwezo wa kupaa hewani na kutua kama ndege (uk. 82-86).

K ni mbinafsi na hapendi kuhusishwa na umaskini na hivyo anavaa figu hivi kwamba hata Mussa rafiki wa utotoni hamtambui. Wananchi kutoka mazingira alimolelewa wanambandika jina la '*Protausi*' kumaanisha kuwa anapaswa kuwalinda na kuwahudumia raia lakini amejitwika uwezo wa mali ya kujinufaisha yeye binafsi.

Ni kiongozi katili kwani anawageuza watu panya wa majaribio na kuharibu nyumba za maskini mjini na vijijini ili apate ardhi. Tunamwona pia akimnyang'anya Bwana Sururu mkewe.

K ni kiongozi anayekataa mabadiliko na ndivyo maana analishwa kiapo cha Wakamba na Wamaasai ili afunguke macho na kuona maovu aliyoyatenda. Anapolishwa kulishwa kiapo, anafunguka macho. Anarudi ofisini na kupata amenyang'anywa mamlaka na pia kasri lake limeuzwa kulipia madeni.

Ananyang'anywa kila kitu na kubaki na Doggy peke yake.K anapitia mabadiliko mengi sana kabla ya kubadilika.

3.2.1.2 **Mzuka**

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* babu yake K ni mhusika mkuu akiwa katika nafsi ya mzuka au pepo. Mtunzi ametumia sauti ya Mzuka kutanguliza usimulizi na msomaji anatambua baadaye kuwa msimulizi mwenyewe ni babu ya mhusika mkuu K, anayejaribu maisha ya mjukuu wake. Mzuka kama msimulizi anasema:

> Baina yangu na K, nafasi nyembamba kama unyuzi. Bahati mbaya kwelikweli.Nilidhani pumzi zangu zingetosha kuniunganisha naye. Labda zingeweza kuanzisha mawasiliano yoyote, lau madogo, lakini wapi! Kwenye mwanya wetu mwembamba hajawahi kujipenyeza shetani seuze malaika. N'namkodolea macho K. N'nampungia mkono. N'namkodolea macho K. N'nampungia mkono. N'najikaza kumshika kichwa hata n'nampigia kelele kumwita- mawe! (uk 1).

Mzuka ni sauti ya mtunzi ambaye anajaribu kumulika athari za utandawazi katika uchumi, athari ya mienendo mipya ya kuiga chochote kutoka Ulaya na kusahau utamaduni wa jamii. Anawashawishi waafrika wajikubali walivyo badala ya kuiga watu wengine. Anawaonya dhidi ya ubinafsi, uchoyo, ufisadi na uchu wa kutaka kukwea juu wafike kiwango cha marafiki wao kutoka Ulaya bila kuwajali waafrika wenzao. Anamaka:

> Kukuruhusu... kujiachia na kukubali kupandwa juu ya mabega... kukubali kufunguliwa kichwa na kuchotwa akili

zote; kuchotwa na kunyang'anywa hata mazinduzi ya kuishi... hili ni kosa la dunia mlio nayo (uk. 79).

Mzuka ni mhusika wa kiajabu sana na mtunzi anatumia fikra zake pamoja na za K kudhihirisha jinsi mtunzi ana uwezo wa kutawala fikra za wahusika. Mtunzi kwa kutumia utunzi huu wa kiajabu, anadhihirisha uwezo wa binadamu wa kuwaza katika uhalisia na katika ndoto. Babu Mzuka anaamini falsafa ya ufufuzi kwani wakati wao waliwaona hata wafu na vivuli vyao katika ndotomacho. Walisema na mizimu na mizuka, kuomba msamaha kwa makosa yao na roho ya mfu kufufuka haikuwa uchawi wa aina yoyote.Anachoamini ni kinyume na kile K anachokiamini. K anaamini kuwa aliyekufa hafufuki na sio vibaya kujitenga na mfu (uk.19-21).

Mzuka ni mhusika wa kiuhalisiajabu ambaye ana uwezo wa kuingilia maisha ya walio hai ili kuwaonya, kuwaelekeza na kuwaelimisha. Anamkumbusha K alivyobadilika kitabia, kihadhi na kifalsafa, kwani zamani aliwachukia matajiri na kuwaita mazimwi. Mzuka anamkumbusha K alivyoahidi kutumikia raia lakini ni msahaulifu na amebadilika hivi kwamba leo ni 'msitu mpya na komba wapya ' (uk.120.) Mzuka anakashifu maovu yanayotekelezwa na viongozi kama K. Mzuka haoni ni kwa nini mtu mmoja awe na majumba mia moja yenye vyumba milioni na akijaliwa maisha yake ni miaka themanini tu. Mzuka anawashawishi viongozi wasiwe wabinafsi na wajali maskini wanaoishi katika makazi duni na yenye umaskini mwingi.

Mzuka ni mwenye uwezo mkubwa. Anapenyeza na kuingia ndani ya dereva Mzula ili aweze kuwa karibu na K na kumwandama popote aendapo. Dereva Mzula anabadilika na kuwa Mzuka. K anaona kisogo cha dereva wake Mzula kimebadilika na kuwa sura ya fuvu, nyuma fuvu na mbele mgandamo wa nyama. Mzuka anamfanya K aone kama ameingiwa na kichaa (uk.19). Tangu Mzuka aingilie maisha ya mjukuu wake K, matukio ya kiajabu yanatendeka maishani mwa K. Babu Mzuka anamwambia kuwa ni yeye anayeondoa chakula na sahani ya Doggy kwa sababu anawajali wanyama kuliko binadamu. Maskini jirani wa K wanalala njaa ilhali K anampatia mbwa wake hata *'cornflakes'*. Mzuka anasababisha K ashikwe na kikohozi yabisi, kichefuchefu na kutibukwa na tumbo, kusikia kicheko kizito kinachokuja kwa sauti yake mwenyewe na kuwaona mahasimu wakimfuata. Hali hii inatokea mawazoni mwa K kwani, maisha yake sasa yanatawaliwa na Mzuka. Mzuka anampa onyo kuhusu uozo wake anapowahudumia wananchi (uk 8).

Mzuka anapenda mila na utamaduni wa jamii yake ya kiafrika.Anapendekeza chakula chenye utamaduni wa kiasili na kukashifu waafrika wanaoiga chakula ambacho hawajui chanzo na athari zake. Tunamuona akiwa kinyume cha K. Mzuka anamuuliza K kwa hamaki:

> Kuna siri gani kwenye kina cha chini kabisa cha akili za
> watu wenye utamaduni huu? (uk. 36).

Mzuka ana uwezo wa kujibadilisha kiajabuajabu, mara anageuka na kuwa moshi au mvuke, mara sura ya fuvu, mara anakuwa sauti ya chura au sauti ya mfu, pia anageuka na kuwa mchwa, maitikwenenda na vile vile kuwa binadamu halisi.

Mzuka pia ana uwezo wa kujibizana na K. Wakati K anamuuliza haja yake ni gani kwake, Mzuka anamjibu:

> Nilivyokwisha kwambia mimi na 'we tumegandamana kama ngozi na nyama, sibanduki mimi mpaka nimalize kazi yangu... Nimeshakwambia nimekuja kukuasa, kukuonya na kukuonyesha yanayokuelekeeni, kama nyinyi ni waja wa kuonyeka na kusikia... Pimeni m'nayofanya (uk. 49).

Babu Mzuka ni mwenye hekima ya hali ya juu. Anaelewa kuwa maovu yanayotendwa na viongozi lazima yatakuwa na hukumu na nyundo zitakuja kuwaangukia vizazi vyao (uk.49). Anaonya kuwa lugha inayozungumzwa ya '*globalization*' ni tamu lakini uhuru wa kibiashara umo katika mshawasha wa vyombo vinavyomilikiwa na kudhibitiwa na mataifa ya Ulaya na hivyo ubora na uzuri wa bidhaa hutegemea kama zimefinyangwa na mataifa yaliyoendelea, jambo ambalo si kweli. Anaghadhibika kuwa wanaotarajiwa kuwaamsha wenyeji wanacheza ngoma moja na wanyanyasaji.

Mzuka anaelewa historia ya nchi za Afrika vizuri. Anamkubusha K kuwa, zamani ulikuwako utumwa na dhiki na kuonya mbele itakuwa na dhiki na utumwa zaidi. Anamweleza K tofauti ya kutawaliwa na kununuliwa ni kuwa ukitawaliwa unaweza kupigana ukapata uhuru wako lakini ukinunuliwa huwezi kujikomboa kama huna pesa za kulipa kujikomboa. Analalamika kuwa heshima ya mwafrika iliondoshwa na watu kutoka bara zingine tokea zamani lakini sasa heshima ya

mwafrika inaondoshwa na mwafrika mwenyewe na kuwa kesho mwafrika ndiye mtu pekee atakayebakia hana heshima duniani (uk. 94).

Ili kudhihirisha mtindo wa kiuhalisiajabu, mtunzi anamtumia Mzuka kuonyesha jinsi ulipizaji kisasi utakavyofanyika. Anazungumza kwa mtindo wa kishairi ambapo maneno yanakatwa na kuwa silabi na yanajidhihirisha akilini mwa Bi. Nyakanga na Zuhura. Mvunjiko huu unasisitiza umuhimu wa yanayosemwa na huyu Mzuka.Mzuka anasema:

> Ni-me-o-na… kwa ma-ndiga ya-ngu ki-su ki-na-ke-ke-ta shi-ngo… da-mu mbi-chi i-na-mwa-i-ka… na m-ke-ke-ta-ji ni su-ru-ru … hu-yu Su-ru-ru - a-li-ye- ku-wa mu-me we-nu… Ha-ja-ku-wa-che-ni yu-no, nyingi n'do m-me – mwa-cha a-na-ngo-ja ku-li-pa ki-sa-si yu-no (uk. 52)

Mzuka anamsomea K mashtaka yake yote na hivyo yeye ni hakimu. Anampeleka K katika safari ili aelimike. Ni mvumilivu na ni mwenye msimamo mkali. Anamuahidi K hatamtoka mpaka akamilishe kazi yake. Anambadilisha K akawa mchwa na kumpeleka alimokulia akiwa kiumbe wa kiajabu. Mwishowe anampeleka kwenye mahakimu wakati ili ahukumiwe kwa maovu aliyoyatenda, kisha anamwambia amemaliza kazi yake, kwani anajua kuwa sasa haki itatendeka. K analishwa kiapo cha Wamasai na Kikamba na anapoachwa na Mzuka, anaona maovu aliyoyatenda na anajinyonga.

### 3.3.2 **Wahusika Wadogo**

Hawa ni wahusika ambao hawachukui nafasi kubwa katika kazi ya kifasihi, bali huwa mhimili au nguzo ya kujenga au kukaza dhamira na kusaidia katika ujenzi wa wahusika wakuu.

#### 3.3.2.1 **Delpiero**

Delpiero ni rafiki mpya wa K, baada ya kupata mamlaka. Ni mfisadi kwani ananyakua eneo zima la ardhi la pahali fulani. Anatetewa na K baada ya wavuvi kulalamika kuhusu unyakuzi wa ardhi. Anasemekana ni mhusika wa kiajabu, kwani wavuvi wanahadithia kuwa walimwona akitoa mabawa na kuruka, akitokomea pahala fulani na kisha kurudi na kuondosha magunia ya unga. Hii inamaanisha kuwa ni mlanguzi wa dawa za kulevya. Mara anageuka mweupe badala ya rangi yake ya zeruzeru (uk.13).

#### 3.3.2.2 **Miyawaza**

Miyawaza ni mgeni kutoka Ujapani. Haonekani kuwa na kazi ya maana nchini lakini ana sifa za mkonowazi. Anampa gari kila ofisa mkubwa ili awafumbe macho aweze kuendelea na shughuli ambazo hazieleweki. Anafuga kucha zenye urefu wa meli nzima na kupita maeneo mbalimbali akinukiliza harufu fulani kama mbwa. Anachimba kwa kucha zake mwaka mzima mfululizo akigundua kitu, jambo ambalo linawafanya wenyeji kucheka na kuridhika na upumbavu wake. Kwa hivyo, yeye anatafuta madini na akiyapata, anayapeleka nchi yake jambo ambalo wenyeji hawalielewi na kuliona kama upumbavu (uk 9, 14).

3.2.2.3 **Von Heim**

Von Heim ni mgeni kutoka Ujerumani anayefanya mambo ya kiajabuajabu. Anasemekana kuwa ana nia kubwa ya kusaidia kumfufua maiti kwa kummiminia bia kutokana na tangi lake kubwa. Anatisha watoto wa watu weusi na hivyo ni mbaguzi wa rangi. Baadaye, anafanya kazi za siri ambazo hazikujulikana na yeyote. Ni katili kwani, akishirikiana na wenzake, wanafanya majaribio ya kisayansi na miili ya binadamu. Anawadharau watu weusi na kuwaona kama chombo cha kufanyia utafiti wa kisayansi. Anawaona waafrika kama watu walio nyuma na kuunga mkono mradi wa FKK kama upeo wa utamaduni ambapo mambo ya anasa yatafanyika (uk 14).

3.2.2.4 **Di livio**

Ni Mwitaliano na mcheza kamari. Anasemekana halali mchana na usiku, kwani yumo mbioni vilabuni, mabasini, bandarini na hotelini na kila mahali akicheza kamari. Anapenda uasherati sana na alifumaniwa akifurahia mchezo wa mbwa wake na msichana mmoja na wengine walisema kwamba raha ya kutazama inapomnogea anajigeuza mbwa na kugawana tija na mbwa wake. (uk.14). Anaeneza virusi vya unajisi wake katika miili ya wasichana na vilevile anawachezesha wavulana mchezo huo aliouzoea kwa muda mrefu. Kufumaniwa sio chochote kwani, anatetewa na viongozi wenyeji walio mamlakani. Kwa sababu ya kupenda anasa, anamshawishi K wafuje mali ya umma na kuanzisha mradi wa FKK, klabu ambapo watu watastarehe kwa kucheza, kula, kuogelea,

kujianika jua na lazima watakaokuwa wakiingia klabu hicho wote wawe wanavua nguo zao (uk. 43).

#### 3.2.2.5 **Mzula**

Mzula ni dereva wake K. Ni mwaminifu na mtiifu kwa mkubwa wake. Anatumiwa na Mzuka ili aweze kumkaribia K na kwa hivyo anabadilikabadilika kila mara; mara yu Mzula na wakati mwingine Mzuka. Mzula anashtushwa na mambo ya kiajabu yanayomtokea mkubwa wake kwani yeye hawaoni mahasimu wanaowafuata na kutoboa magurudumu ya Limonsi (uk. 23-27). Anabadilika na kuwa mhusika wa ndotoni tu.

#### 3.2.2.6 **Maajuza**

Maajuza ni mkewe babu Mzuka na K ni mjukuu wake. Ni ajuza anayeugua na hivyo anahudumiwa na watoto na wajukuu wake. Ni mwenye hekima na msimulizi hodari. Ana uwezo wa kuzungumza na mzuka wa bwanake, babuye K, kwani marehemu bwanake humzuru na kumwambia mwisho u karibu na hivyo atazame dhiki akingojea faraja. Ni mvumilivu na mwenye imani kuwa jamii ikiwajibika,furaha itapatikana. Ana uwezo wa kusoma akili za watoto na wajukuu wake na kutambua hawaamini mizuka. Anaamini kuwa mizuka inaweza kuwasiliana na walio hai katika ndoto au ndoto macho na wanaweza kuleta balaa kwa jamii inapokosa mwelekeo. Ana uwezo wa kuwaona mizuka katika maumbo mengi kama vile paka, nyoka, mijusi na vinyonga.

Maajuza ni mwenye hekima nyingi na anapenda kuelekeza jamii yake. Alimpenda mumewe na kila wakati anayakumbuka maneno yake ya hekima. Anasema mambo kwa uwazi na hivyo kumshtua K. Kwa mfano, anasema kuwa jamii zetu zinapuuza vitu vingi na ndio maana sasa zinalaaniwa. Hata akiwa mtu ni mkwasi vipi, hawezi kutulia na kustarehea ukwasi wake katika dhuluma na visasi vitamfuata. Anawaeleza watoto wake kuwa, makungu wapo na ndio wanaopanga sababu na matokeo yetu, na wakighadhibika, huamsha taharuki za woga. (uk.119). Kwa hivyo anaelimisha, anaonya na kuelekeza jamii.

### 3.2.2.7 **Mahasimu wa K.**

Hawa ni wahusika wa kiajabu na mahasimu wa K wasioonekana. Wahusika hawa wamo akilini mwa K. Mahasimu hawa wanaongezeka kutoka watu wawili hadi kufika maelfu. Ni watu ambao K aliwakosea na nia yao ni kulipiza kisasi. Wanamzunguka K na dereva wake wakiwa katika Limonsin. Miongoni mwao kuna viditia (watoto wasiokua), vimada na wazee. Wanaendelea kumuongeza hofu K kwani wanajitokeza kila mahali, barabarani, ofisini, hotelini na hata kasrini mwake, wakiwa wameghadhibika na kubeba silaha za kumtendea K maovu. Sururu aliyenyang'anywa mke na K ni mmoja wao.

### 3.2.2.8 **Mahakimu Wakati**

Mahakimu hawa ni wa kiajabu. Wao ni wakongwe wenye madevu na hawaonekani binadamu wa kawaida. Wana sauti ya kutisha na kuogofya. Mahakimu hawa wa kiajabu na kwenye mahakama yao, wanamlisha K kiapo cha

Kimaasai na Kikamba, na wanapomaliza kumhukumu kwa maovu aliyoyatenda, K anajinyonga.

### 3.3 HITIMISHO

Katika sura hii, tumechunguza na kubainisha mandhari na matukio na pia wahusika wa uhalisia na uhalisiajabu katika *Babu Alipofufuka*. Tumepata ya kuwa, riwaya hii inachanganya ulimwengu wa ndoto na uhalisia ambapo nia ya mtunzi ni kumbainishia msomaji yanayotendeka hakika ili aielewe dunia kwa uwazi zaidi. Mtunzi Said Ahmed Mohamed anamulika masaibu yaliyomo barani Afrika kabla na baada ya Uhuru. Aidha anadhihirisha historia na siasa za nchi za ulimwengu wa tatu ambazo viongozi ni wenye ubinafsi mwingi na hawajali wanyonge. Riwaya hii imetumia wahusika, mandhari na matukio yanayochanganya uhalisia na uhalisiajabu hivi kwamba, ni vigumu kuweka mipaka dhahiri kati ya uhalisia na uhalisiajabu. Olali (2010:24) anadai kwamba, matumizi ya mtindo huu hulenga kuonyesha kuwa matukio kama haya hutendeka katika ulimwengu na kosmolojia ya Kiswahili. Yaani, uhalisia huu unasawiri jamii ama sayansi kuhusu ulimwengu na hivyo matukio yanayoonekana kama ya kiajabu, kwa hakika ni ya kawaida katika uhalisia wa Kiswahili.

# SURA YA NNE

# UHALISIA NA UHALISIAJABU KATIKA RIWAYA YA *WATU WA GEHENNA*

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunadhamiria kuchunguza na kubainisha vipengele vya uhalisia na uhalisiajabu kama vinavyojitokeza katika riwaya ya *Watu wa Gehenna (2012)* ya Tom Olali. Katika kufanya hivi, tunaangalia uhalisia na uhalisiajabu katika kiwango cha wahusika na katika kiwango cha mandhari ambapo matukio ya kiajabu yanajichimuza katika riwaya.

Katika uchunguzi huu, tumebainisha sifa za kiajabu za wahusika pamoja na matendo yao yanayowafanya waonekane viumbe wasio wa kawaida. Ni bayana kuwa wahusika wa aina yoyote wawe binadamu au viumbe wengine hudhihirisha wasifu wa binadamu katika hali halisi kwa kuwa wanawakilisha binadamu wa kawaida. Wahusika huwa nguzo kuu ya kusukuma hadithi mbele. Kupitia kwa migogoro yao wanapotagusana na wahusika wengine, tumebainisha upekee na umuhimu wao katika kuendeleza riwaya hii kwa kuonyesha sifa bainifu za kiuhalisiajabu, kama zinavyojitokeza. Uhusika wa jadi ulijengeka kwenye uhalisi wa kijamii ambapo wahusika kama vile majitu, mizimu na hata wanyama waliaminika kuwa walikaribiana na wanadamu katika ulimwengu halisi. Hivyo basi, tumetoa mchango wetu kutoka fasihi simulizi za jamii zetu.

Katika kipengele cha mandhari, tumebainisha mahali kama panapojengwa na mtunzi na mnamotukia matukio ya aina yoyote yawe halisi au ya kiajabu. Katika kuchunguza mandhari, tumeangazia ndoto kama mandhari ambayo yamechukua nafasi kubwa katika riwaya ya *Watu wa Gehenna.* Akieleza ndoto, Malcolm (1959:940) anasema kuwa ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu ambaye yuko macho au amelala na yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikra za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, malengo, matarajio na matamanio. Hivyo basi ndoto husafirisha tabia na sifa za mtu kwa sababu huambatana na matukio kadha wa kadha katika maisha ya anayeota na vilevile picha halisi ya mambo anayowaza. Katika sura ya tatu, tumeeleza maana ya mandhari na wahusika pamoja na aina zake. Hivyo tutarejelea sura hii inapobidi.

## 4.1 MANDHARI NA MATUKIO YA UHALISIA NA UHALISIAJABU

Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina yoyote ya fasihi. Mwandishi wa riwaya ya *Watu wa Gehenna* amechanganya mandhari ya kiuhalisia na ya kiuhalisiajabu hivi kwamba ni vigumu kuweka mipaka ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa ndoto. Mwandishi anaanza hadithi kwa kutuchorea taswira ya kiajabu ya Gehenna (jehanamu) ambapo moto mkali wa kutesa watu milele na ambavyo joto linalotoka huko linasababisha watu wasio wakaaji wa Gehenna kubadilika na kuwa miale ya moto (uk.1-3).

Kwa kutumia maandishi ya kiajabu na yasiyozoeleka, anaorodhesha matendo kama vile *Korappzion, Traibbolizim, Chhaldabius* na *Burnt for Rest* yanayowafanya watu wawe wa Gehenna. Mtunzi ametumia mandhari haya ya kiajabu yenye matanuri yenye moto mkali wa kutesa watu milele kama njia ya kuwaonya wanaotenda maovu na kuwahakikishia kuwa mwishowe watapata adhabu kali kwa kutowajibika. Mandhari kama haya yanapatikana katika biblia takatifu ambapo wenye dhambi wanaahidiwa kutupwa kwenye moto na kilio cha milele na milele huko jehanamu.

Eks kama mhusika mkuu anajadiliana na nafsi yake kwenye ndoto. Nafsi yake inamhoji na kumuuliza binadamu ni nani. Anaposhindwa kujibu nafsi yake inamcheka halafu inamjibu. Matukio haya yote ya kiajabu yanafanyika akilini mwa Eks akiwa ndotoni. Eks anajicheka mwenyewe bila kujua, kuonyesha jinsi binadamu analemewa kuyatawala maisha yake apendavyo. Kuna nguvu au uwezo zaidi unaotawala maisha yake (uk 10-13). Hivyo ni wazi kuwa katika akili za binadamu, matukio mengi hutokea ambapo mengine mtu hana majibu yake.

Tunapata mandhari ya kihalisia ya kampuni ya *THE WORLD CEMENTERS INC* ambapo Eks amefanya kazi kwa zaidi ya miaka 40. Akiwa mwaka wa 20 katika kampuni hii, anapatwa na ugonjwa wa mapafu na vilevile kusahau matukio maalum na tarehe maalum. Ubongo wake pia unaathirika baada ya kupata ugonjwa wa moyo na baadaye anaanza kujiendea haja ndogo. Badala ya kampuni kuwajibika na kumsaidia apate matibabu, anafurushwa hata baada ya kupatikana

kuwa ugonjwa huu unatokana na athari ya saruji. Pia kampuni haikumlipa fidia na hivyo Eks anashindwa kulipa gharama za juu za matibabu (uk.14-17).

Kutokana na maelezo haya, mtunzi anatumia mhusika na mandhari halisi kuangaza jinsi wafanyikazi wanateswa na baadhi ya makampuni punde tu wanapopata matatizo ya kiafya wakiwa kazini.

Katika mandhari ya ndotoni, nafsi ya Eks inamshurutisha na kumuamuru afe. Kabla ya kufa, nafsi yake inamuuliza kwa nini alipokea maelezo maovu kuhusu mchezo wa sataranji. Baada ya kuulizwa swali, Eks anakufa na baadaye anafufuka. Baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kunachukua miaka saba. Katika miaka hii saba, MKUU na Eks wanaulizana na kujibizana maswali. Kwake Eks anaona kama alikuwa amelala na MKUU anamuuliza aliona nini huko kondeni. Eks anamjibu kuwa aliona mizaituni, vitunguu, parachichi, balungi, tini, viazi vitamu, maharagwe, figili, karoti, zabibu, nyanya na jozi (uk. 30-31).

Kutokana na maelezo haya, tunaona uduara wa wakati kama mhimili wa uhalisiajabu ukijitokeza. Dhana ya wakati na mwanda au mahali katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (na pia katika *Babu Alipofufuka*), huakisi wakati wa kidhahania usioeleweka na huwa na athari ya kisaikolojia kwa wahusika. Wahusika kama hawa wanafanya matendo yao kwa kipindi kirefu na wanabaki katika hali zao (Wamitila: 2003:156). Katika uhalisiajabu, wakati si wa kistari bali ni wa kiduara. Tunamuona Eks akifa na kufufuka baada ya miaka saba, lakini

bado yuko katika hali ile ya kwanza na kuendelea kuchangia katika riwaya. Katika wakati wa kistari, binadamu anazaliwa, anakua kijana, anaoa au kuolewa, anazeeka halafu anakufa. Katika uhalisiajabu, mhusika anaweza kufa na kufufuka baadaye kama huyu Eks ama babu Mzuka katika *Babu Alipofufuka*. Pengine ndio maana mwandishi Danow (1995:94) anapendekeza kwamba, hatupaswi kufikiria wakati kama kitu kinachofululiza moja kwa moja.

Katika mandhari haya ya kiuhalisiajabu, tunaona mhusika kwa jina MKUU akimweleza Eks umuhimu wa matunda ambayo Mungu aliyaumba pale mwanzoni kabla ya kumuumba Eks kwa maana ya binadamu. (uk. 30-34). Mtunzi kwa kutumia mandhari ya kiuhalisiajabu amefanikiwa kumuelimisha hata msomaji kuhusu umuhimu wa kula matunda kama ilivyokuwa mapenzi ya Mungu alipoumba miti na matunda kabla ya kumuumba binadamu. Eks na mkewe Takosani wamezoea mapishi mazitomazito na kuyaita '*Real Typical English Breakfast*' ambayo ni mchanganyiko wa nyama, na mkate uliopakwa siagi kila upande na chupa ya mvinyo mkali chapa *martel.* Wanachukia kwa nyoyo zao maboga na matunda na kuyaona kama chakula cha sungura. Ukweli ni kuwa magonjwa mengi yanatokana na kutokula vizuri kwani, watu wanaiga hata vyakula wasivyojua asili na hata umuhimu wake.

Katika mandhari ya mjadala kati ya Eks na MKUU, Eks anapewa amri saba. Hizi ni kama zile amri kumi za Mungu katika Biblia ambazo ni sharti zitimizwe ingawa vigumu. Katika mandhari haya, matukio ya kiajabu yanafanyika. EKS

anaamrishwa kubadilisha jina lake na umri wake upunguzwe kutoka **70** hadi **23**. (uk. 36).

Baada ya MKUU kumpa EKS amri hizi, anafyatuka na kufifia angani na anaporudi anawatolea binadamu wote wa Kiafra ushauri. Tunapata hotuba ya kiajabu ambapo MKUU anajua matatizo ya ulimwengu wote ambapo tatizo la afya ni changamoto kila pahali na wanaoteseka zaidi ni Wakiafra kwani kuna uchache wa hospitali, madaktari na dawa. Mandhari haya yanadhihirisha nguvu za ajabu ambazo ni za kiungu na kuna marejeleo mengi ya biblia takatifu kama mahubiri. Mkuu anasema:

> Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu
> watajinyenyekeza watubu dhambi zao na kuniomba, mimi
> nitasikia kutoka POPOTE na kuiponya Kiafra (uk. 37).

Sikujua ni rafikiye mkubwa wa Mwalimu Baya na anafunga safari kwenda kumtafuta. Anapitia katika mtaa wa *Reciful Meadows* na katika mandhari haya, anagongana na msichana maridadi kwa jina Takosani binti Inatesh. Kama jina lake linavyoashiria, Sikujua anamtamani awe mchumba wake wa ndoa bila kujua mienendo yake. Wanajadiliana na ajabu ni kuwa, msichana huyu wa kiajabu ana mambo ya kiajabu. Takosani anaeleza kuwa, anapenda kutembelea makaburini na kuombea kaburi la mama yake, huku akilipigia magoti na kuweka sarafu juu ya kaburi kama salamu. Anaeleza kuwa anazungumza na mizimu ya mama yake na vile vile uraibu wake ni kuogelea baharini (uk. 41-43).

Sikujua anashtuka anavyosikia haya lakini kwa sababu ya urembo wa msichana huyu wa kiajabu, wanapanga vyumba nambari 15 na 18 kila mtu chumba chake bila woga. Takosani anaomba chumba nambari 18 kibadilishwe wachukue chumba nambari 13. Kulingana na imani na itikadi za baadhi ya jamii, kuna nambari ambazo zinahusishwa na imani fulani. Katika imani na itikadi za jamii nyingi za Ulaya, nambari 13 inahusishwa na nuksi au mikosi. Katika jamii hizi, ni vigumu kupata chumba au ghorofa ya 13. Vilevile katika mchezo wa kandanda, ni vigumu kupata mchezaji nambari 13 au gari nambari 13 katika mbio za magari maarufu kama *Safari Rally*. Vilevile, nambari **7** ina umuhimu sana katika biblia takatifu, ilhali nambari 666 inahusishwa na shetani. Katika mila na desturi za jamii ya Wakikuyu, watoto hawakuwa wakihesabiwa na ilikuwa hatia kutaja watoto wote wa mtu kwani, waliamini kufanya hivi kungeleta maafa. Kwa hivyo, uhalisiajabu wa nambari 13 katika riwaya hii, ni mfano wa jinsi mila na tamaduni nyingi duniani zinavyochukulia nambari.

Katika mandhari haya ya kiajabu ya chumba nambari 13, matukio ya kiajabu yanapatikana. Baada ya Sikujua na Takosani kufanya mahaba, Takosani anaondoka kupitia ukutani lakini Sikujua hafahamu. Takosani anamwahidi Sikujua utajiri jambo ambalo linamshangaza Sikujua na kumuuliza kama yeye ni jini. Takosani anakataa na kumhakikishia yeye si jini na hadithi za majini haziamini.

Takosani anamwamuru Sikujua afumbe macho na anapofumba macho anapoteza fahamu. Anapozinduka, anajikuta kwenye mandhari ya kiajabu eneo linalozungukwa na mipapindi mingi na mchanga tifutifu huku Takosani akimtaka wafunge ndoa. Kwake Sikujua haelewi kama anaota ndoto au ni hali halisi na anamwambia Takosani anaona kama yeye ni jini lakini anamjibu yeye ni binadamu halisi. Takosani anamfahamisha wako *Anneheg Xpress*, mtaa wa *Resiful Meadows* na kuwa nyumbani kwao ni chini ya bahari na duniani yeye hufika kwa shughuli maalum. Kadiri saa zinavyoendelea ndivyo Takosani anavyozidi kuwa mrembo. Katika mandhari haya ya ndotoni, wanajipata tena chumbani kwa Sikujua na Takosani anaomba awekewe wimbo wa *MWAKA WA SHETANI* lakini Sikujua anasema hana santuri inayoitwa hivyo. Takosani anazidadisi santuri zile na mara anaibuka na santuri iliyoandikwa kwa rangi nyekundu tena nzito *Inatesh aw akawm*. Hii ni santuri yenye michoro ya kiajabu na wimbo unapaswa kuanza mwisho kwenda mwanzo ili mtu apate maneno kinyumenyume. Wimbo huo wa *mwaka wa shetani* ukiwa unaendelea Sikujua anaona gari pale kando na haelewi kama anaota ama ni hali halisi na anajisemea kuwa hali halisi na ndoto ni kitu kimoja (uk. 48-52).

Kutokana na kisa hiki, tunaelewa wazi jinsi watu wengi wanavyojipata katika sakata za kutisha na hata kunaswa kwenye nguvu za giza bila kujua. Wanafunzi wengi hasa katika vyuo vikuu wanajipata tayari wamenaswa katika matumizi ya dawa za kulevya, imani za nguvu za giza na pia katika anasa bila kujua. Nyimbo nyingi zinazoimbwa kwenye magari, klabu na hata mtaani hazieleweki lakini

wasiojua hununua kanda hizi na kuzifurahia huku wakijitia mashakani. Matukio ya aina hii pia yamo katika sehemu za kuabudia na kufanyia kazi na hata kama wengi wanadai hayapo, ni mambo halisi yanayopatikana kila siku. Hivyo, mtunzi amejaribu kumulika visa vya aina hii na kutahadharisha wasomaji na jamii yote kwa jumla.

Mtunzi wa riwaya ya *Watu wa Gehenna* amefanikiwa kuvunja mipaka ya kijamii, kitaifa na hata kimataifa. Hii ni kwa sababu wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja. Katika kisa kimoja, mhusika Akilimali Van Krockoff kutoka Tasmania anajadiliana na Siyawezi kuhusu Kiafra. Krockoff amehitimu shahada ya uzamifu katika Chuo Kikuu cha *The End of the World* huko Magharibi mwa Tasmania. Majadiliano yenyewe ni kuhusu wanasiasa wa nchi za Kiafra na jinsi wanavyowapa wananchi matumaini wakati wa uchaguzi na mwishowe raia huishia mtoni kwani chama kinajengwa juu ya mtu mmoja ambaye anakuwa yeye ndiye chama, katiba, sera, kila kitu ndani ya yote, na rais akifa siasa zinayumbayumba kwani madaraka yote yamo mabegani mwake (uk. 54-55). Akieleza kuhusu siasa huko Tasmania, Krockoff anasimulia matukio ya kiajabu yanayotokea. Anasema kuwa siasa na ushirikina huandamana, na wanasiasa wanaamini mambo ya ndumba. Akifafanua, anaeleza kuwa ndumba ni jina pana linalojumuisha siri ya mizungu, mazingaombwe, nguvu na maombi na imani potofu, ufundi wa kuwasiliana na mizimu, dawa za kushirikiana na jicho la

pili. Anaeleza kuwa huko Tasmania, wanasiasa wanatumia nguvu za kichawi kupata ushindi katika uchaguzi (uk. 54-55).

Akichangia mjadala, Siyawezi anaeleza kuwa kwa kipindi kirefu Kisiwa cha Pate kimekuwa na mafundi mahiri wa sayansi ya mazingaombwe. Katika miaka ya 2070, Malkia Bi. Kirembwe, aliheshimika na kukimbiliwa na wengi ambao upigaji ramli sio tatizo. Katika simulizi za Pate, Krockoff anaeleza kuwa picha ya fundi wa ndumba ni ya aina ile inayoelezwa na William Shakespeare katika tamthilia yake ya *Macbeth*, kuwa ni viumbe waliochakaa, wenye muonekano wa mnyama mwitu na hawaonyeshi kama wakaaji wa dunia hii ingawa wako juu yake (uk. 56). Wabunge na mawaziri katika suti zao nzuri hukalishwa chini na fundi wa aina ya Karumanzira na kutakiwa kuruka damu ya mnyama aliyechinjiwa njia panda saa mbaya ya usiku au anashuhudia mbuzi akizikwa hai huku macho, masikio na midomo ya mnyama huyo imeshonwa kwa jina la kifo cha demokrasia, ili kuzika nguvu za wapinzani wao. Kisha usiku unaofuata unamwona akitema cheche bungeni kama mtu wa watu wakati ukweli ni mtu wa Gehenna (uk. 57).

Kisiwani Pate, tunaelezwa kuwa wanasiasa hutumia popobawa kuwadhulumu wapinzani wao. Katika vyombo vya usafiri, wanaosafiri kwa jahazi usiku kutoka Pate kwenda Lamu hawafungi macho kwa muda wao wa usafiri kwa kuhofia kujeruhiwa na popobawa, kwani inaaminika kuwa wanatumiwa na mwanasiasa mmoja kushambulia watu huku akieneza ugonjwa wa ukimwi kwa lengo la

kodhoofisha ngome ya Chama cha Mwananchi. Siyawezi anasema kuwa, imani ya ushirikina na maswala ya majini, mazimwi na wanga yana historia ndefu kisiwani Pate. Matukio ya kiajabu yanafanyika hivi kwamba mtu anaondolewa nyumbani kwake usiku bila mwenyewe kujua na kwenda kufanyishwa kazi ya kuvunja mawe usiku kucha au kuchimba kisima na kurudishwa alfajiri akiwa amechoka (uk.58-59). Hata hivyo, kuna baadhi ya jamii au watu wanaoamini mambo ya aina hii na ukweli ni kwamba, mtu huona anachotaka kuona na kusikia anachotaka kusikia na imani za majini au nguvu za giza humuathiri mwenye imani hizo.

Tunapatana na ndoto ya kiajabu ambapo Sikujua analiona gari wanamosafiria likizama baharini. Anajikuta akiwa yupo kwenye mji mzuri uliokuwa na ghorofa za kupendeza. Anajisemea kuwa, hiyo haikuwa ndoto, fikra wala hali halisi, bali yote matatu kwa pamoja (uk. 60).

Kutokana na usemi huu wa Sikujua, tunaona jinsi uhalisi na ndoto vinavyochanganyika hivi kwamba hakuna mipaka ya uhalisi na jinamizi katika uhalisiajabu. Mara Sikujua analetewa chakula na wapambe wa Takosani. Mara mandhari haya yanageuka mahakama na wapambe hawa wanamshtaki kuwa alipokuwa duniani alizoea kukata maelfu ya miti na aliposhutumiwa kutoendelea aliwalaani wale aliodai ni wapinzani wake. Pia anashtakiwa kuwa alipokuwa mamlakani kama mbunge, alishiriki katika vita vya kikabila na kusababisha umwagikaji wa damu wakati na baada ya uchaguzi. Vilevile, anashtakiwa kwa

kutumia nguvu za giza kupata cheo cha ubunge na kutumia dawa ya kuongeza nguvu za kiume zinazotokana na wachawi ili kumwezesha kufanya mapenzi kwa muda mrefu na mtu asiye mke wake. Alimhimiza mwanamke kutumia dawa ya kutengeneza ubikira bandia ili amfurahishe katika uzinzi na mwisho anashtakiwa kwa mazoea ya kusoma *The Codex Gigas.* Wapambe hawa wanamfunga kitandani na kumtandika bila huruma (uk. 60-62).

Mtunzi anatumia uhalisiajabu huu kumulika dunia na mambo yanayofanyika kisirisiri katika ulimwengu tunamoishi. Watu wengi hasa viongozi hushiriki maovu ya aina yote kisirisiri, lakini ukweli ni kwamba kuna wakati haya yote yatafichuka na adhabu kali kutolewa kwao.

Kuna mandhari ambapo mchezo wa kiajabu unachezwa na wahusika wakuu watatu ambao ni Sikujua, *The Codex Gigas* na Daktari Majini Tisa na unasemekana ni mchezo wa ukweli. Pazia jekundu linaanguka na linaporudishwa mara moja linafuatwa na pazia jeusi. Katika mandhari haya ya kiajabu, Sikujua ni mbunge aliyewaua watu 666 na kwa kufanya hivi anavishwa *Knight in the National Order of the Legion of Honour* na kuapa kwa *The Codex Gigas* mara 666 huku amefungua ukurasa 290. Usiku wa manane Sikujua anakutana na Daktari Majini Tisa huko mahame ya Ndagoni na wanaelekea bandari kubwa ya Wete ambayo ingaliwawezesha kusafirisha miili ya albino wakitumia merikebu za kuelekea Tanga zilizokuwa zimepakia mashehena ya saruji, mbao, karafuu, mapakacha ya *minazi* na ndizi. Kuna stoo kubwa ya kuhifadhi miili ya albino

Katika mandhari ya safarini, tukio la kiajabu na la kushtua linafanyika wakati Mwalimu Baya anampeleka msichana Mishi huko Chumbageni. Wakiendelea na safari yao kwa vokswageni ya Sikujua, treni inapiga honi inayoashiria kuwa iko karibu na hivyo Mwalimu Baya anaamua kuongeza mwendo ili apite kabla ya treni kufika kwani hakutaka kuzidi kuchelewa. Ghafla, gari lake linazimika katikati ya reli na anapojaribu kuwasha bila mafanikio, kwani betri ilikuwa imekwisha kawi; anaona taa ile kubwa mbele ya kichwa cha treni. Anamuamuru Mishi afungue mlango atoke nje lakini anaendelea kukaa kama amepigwa na bumbuazi na haonyeshi dalili ya kufahamu hatari inayowakabili. Anapojaribu kufungua mlango wake atoke, nao unakataa na kuhisi akili inamruka. Anapojaribu kuvunja vioo kwa ngumi navyo vinakataa amri na kumfanya ajilaumu kwa nini akampa lifti binti huyo mwenye mkosi (uk. 102-107).

Mara Mishi anamgeukia kwa haraka na kukunjua mikono yake kwa kasi ya mwanga na kumkumbatia Mwalimu Baya kabla tu treni haijagonga gari (uk. 107). Mishi anatamka jina *Shemhamforash!* Kwa haraka kwenye sikio la Mwalimu Baya na mara treni inaligonga gari lao kwa kishindo kama sauti ya radi ikipasua matlai lakini Mwalimu Baya hasikii sauti yoyote na kimya kinatanda akiwa mikononi mwa Mishi. Anapofumbua macho, anaona mabehewa ya treni yakipita ndani yao kama waliokuwa mizuka. Anaweza kuona viti, watu na kila kitu ndani ya treni huku treni ikiendelea kwa kasi. Baya haamini jinsi treni imepita ndani yao, bila kuwadhuru na anaendelea kushuhudia behewa la mwisho bado wakiwa katikati ya reli huku treni inaendelea mbele. Mishi anamwachilia na anarudi

kitini kujaribu kuwasha gari ambalo linawaka mara moja. Anaegesha gari pembeni aweze kuvuta pumzi alizokosa kwa muda ule wote. Anashtuka kwani hajui kama bado yu hai, ndotoni, au ndio ashakufa na roho yake bado inatangatanga (uk. 107-108).

Wakiwa garini, tukio lingine linatokea wakati Mishi anafungua mlango na kutoka kuelekea nyumbani. Mwalimu Baya anasikia mlio wa 'Ko Ko Ko' kama vile mtu aliyevaa viatu vya mchuchumio. Ana hakika moyoni mwake kuwa Mishi hakuwa amevaa viatu vya mchuchumio kwani alikuwaamevaa viatu vya wazi. Anapotazama miguu yake aone ni viatu gani hivyo vyenye kutoa mlio ungedhani mbao ikigonga sakafu, moyo unampasuka kwani hakuyaamini macho yake. Miguu ya Mishi imegeuka kwato za ng'ombe. Baya hataki ushahidi wa ziada. Lo! Mishi alikuwa jini (uk. 109-110). Tukio hili la kiajabu linatahadharisha watu dhidi ya kushirikiana na watu ambao hawawajui vyema. Wakati mwingine madereva wanawapa wasichana warembo au akina mama wajawazito lifti na baadaye wanawageuka kuwa majambazi na hivyo kuhatarisha maisha yao. Katika nadharia ya uhalisiajabu, mazingira ni sehemu muhimu sana na majitu na mazimwi hurejelewa na Mishi ni mfano wa wahusika wa kiajabu katika riwaya hii.

Mwalimu Baya anaendelea na safari huku akikanyaga mafuta kama aliyepagawa na mara anajihisi kibaridi kikimpuliza shingoni mwake na kudhania ameacha mojawapo ya madirisha ya gari wazi. Anapoangalia madirisha yamefungwa lakini

nywele zinamsimama na kujua kuna tatizo. Sauti ndogo ya kike inamshutua ungedhani ameuona mzimu wa Babu yake K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ukimuita. Anapoangalia kiti cha nyuma, anamwona binti mdogo Saida akiwa amekaa upande ule ule wa gari kama alivyokuwa ameketi wakitoka Maweni. Ana uhakika alimshusha Saida Masiwani kwa mama yake na kuondoka yeye na Mishi tu. Kufumba na kufumbua, anaangalia nyuma na Saida ametoweka jinsi ile ile alivyoingia ndani ya gari. Mwalimu Baya anaanza kujua kuwa ameanza kurukwa na akili (uk. 113).

Katika mandhari ya kiajabu, Mishi na Mwalimu Baya wanajikuta kwenye ghorofa ndefu pembeni mwa bahari ya Hindi, huku wamekumbatiana kimapenzi kwenye kitanda cha sufi chenye mashuka ya hariri. Baada ya kufanya mapenzi, Baya anaendelea kumpapasa na kugundua binti huyo ana magamba mgongoni na mara mwili wake unapoteza joto na kuwa baridi kama barafu jambo ambalo linamshtua sana.

Anajisemea kuwa maajabu kama haya hayapaswi kuonekana na mwanadamu na baadaye kusimulia. Mishi anatamka tena neno *"Shemhamforash!"* na mara chumba kizima kinajazwa mwanga wenye rangi ya mbalamwezi angavu unaotoka ndani ya mwili wa binti huyo.Mwalimu Baya anamtazama na anajikuta roho inamtoka. Ajabu ni kwamba, Mishi ana jicho moja kwenye paji la uso wake, huku mwili wake ukiwa nusu toka juu hadi chini, titi moja, mkono mmoja, mguu

mmoja, nusu kila kitu. Anamsukuma kutoka kifuani mwake na kupiga ukelele kuomba msaada (uk. 117).

Anapozinduka usingizini, Mwalimu Baya anauhisi mwili wake wote ukipigwa na upepo mkali. Anapoangalia vizuri, anagundua hayumo chumbani mwake, wala ndani ya nyumba, wala ndani ya hoteli. Anajikuta juu ya mbuyu huku nguo zake zinaning'inia kwenye matawi yake (uk.117-118). Baada ya muda mfupi wasamaria wema wanamsaidia kuteremka na kumpa shuka ajisitiri. Anamueleza mzee mmoja kisa chote kutoka mwanzo hadi mwisho na mzee anamwambia kinachomsibu ni shetani wa mahaba kutoka Gehenna aliyewahi kuwa mke wa Shemhamforash! na kuwa hakuwa wa kwanza kupatwa na masaibu kama hayo. Anapomuuliza mzee huyo kama kuna dawa au madhara yaliyompata baada ya kukutana na mke wa Shemhamforash, mzee anamueleza kuwa kama amefanya mapenzi naye kwenye ndoto, ameshateuliwa na hivyo hatamuacha alale na mwanamke mwingine yeyote hadi kifo. Anamuelezea kuwa njia ya pekee ni kwenda Mabokweni kwa Sheikh Hamza Hamdani ili ampe dawa na kumuagua, Baya anauliza kama Sheikh huyo ni jini lakini mzee anamhakikishia si jini wala ndoto lakini ni mambo halisia. Baya anafunga safari ya kwenda kwa Sheikh anayempa masharti yanayomchukua karibu miaka saba kutimiza na mwishowe ile laana inavunjwa baada ya Mwalimu Baya kumtafuta mtu mgeni huko Chamada na kumtupia laana hiyo. Mwalimu Baya anaamka kutoka kitandani na kupata kuwa matukio haya yote yametendeka akilini mwake (uk. 112-120).

Kutokana na kisa hiki cha kiajabu, ni wazi kuwa matukio mengi hutokea akilini mwa binadamu kama ndoto anapolala ama wakati yu macho lakini yu mawazoni. Wakati mwingine matukio haya yanaonekana kama mazingaombwe lakini kuna wale wanaodai kuwa ni matukio ambayo yashawahi kutokea kwa binadamu halisi na ulimwengu halisi. Ni matukio ya kutisha na kuogofya na kawaida yanaathiri maisha ya binadamu hata mchana anapokumbuka yaliyotokea kwenye ndoto. Mtunzi anataka kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hutokea katika ulimwengu halisi.

Katika mandhari halisi ya Chuo Kikuu cha Kuhisika, wanafunzi wanagoma wakiungwa mkono na wazazi pamoja na baadhi ya walimu kwa kutoridhishwa na utawala wa kidhuluma. Wanabeba mabango huku mojawapo likiwa limeandikwa: *THE CORRUPT POLITICIAN'S CREED (uk. 122).* Mwanafunzi anayelibeba bango hili anapigwa risasi na polisi na kuumizwa vibaya. Wanafunzi wanasisitiza maktaba ichomwe wakidai inahifadhi nakala ya *The Codex Gigas* na makala ya *Hydropolitics around the Nile.* Maandamano ya aina hii pia yanafanyika katika nchi nyingi za Kiafra ambapo ujumbe kutoka kwa *Anonymous* katika nchi ya Mafirauni unaenezwa kupitia kwa *facebook* na *twitter.*

Maandamano ya aina hii yamewekea msingi nadharia ya uhalisiajabu kuwa, wakati na mahali vina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Kwa hivyo tunaona jambo linapotokea mahali fulani linajirudia kwa sura nyingine mahali pengine. Migomo ya wanafunzi wa shule za upili, vyuo na raia kutoka nchi tofauti za

Kiafra hutokea mara kwa mara na mwishowe tunaona nchi nyingi zinaanguka moja baada ya nyingine. Pia tunaona athari ya utandawazi kwa vile jumbe zinasambazwa haraka nchini na hata katika kiwango cha kimataifa.

Katika mandhari ya *Gehenna Systems Centre* (GMC), mhusika Yunasi anapofanya kazi huko Newyork, tunaona uhalisi na ndoto zinachanganyika. Yunasi haelewi kama yu ndotoni au ni ukweli na anamwandikia rafiki yake akimueleza sauti inavyomwambia jinsi alivyofuja pesa za washiriki na kulala na wake zao alipokuwa kasisi. Pia anajipata akisoma kitabu kinachoitwa *Encyclopaedia of Haunted Places* badala ya biblia takatifu chenye wimbo wa *Gehenna.* Yunasi kama mhusika halisi ana imani kuwa, kuna nguvu za ajabu katika jina la Yesu na wote wanaloliita wanaokolewa. Anaona amezungukwa na maiti za watu wengi huku akiongozwa na mtu asiyemjua mwenye koti lenye maandishi MKOMBOZI akiwa na tochi. Anahofia bibi yake (Saida) amekufa lakini anapompigia simu anamkubali Yesu na kuokoka. Mara anaposema amina, anashtuka na kuamka huku uso wake umelowa jasho lakini aliyoshuhudia hayakutokea kwani ilikuwa jinamizi na anaonelea labda yatatokea siku zijazo (uk.149-154).

Kuna mjadala unaotokea mawazoni mwa mhusika Hikmat. Hikmat mtazamaji halisi wa kipindi cha *The Night of the Living Dead* anachangia mjadala kuhusu matatizo yanayokumba Kiafra. Runingani, mjadala una wahusika watatu Ikmat, Kmat na Mat na ghafla kitendo cha kiajabu kinatokea. Hikmat anatoa maoni yake

na wale watangazaji wanakubaliana naye na kumhimiza aendelee na hivyo mtazamaji akawa mtangazaji na watangazaji wakawa watazamaji (uk.171). Ikmat anaeleza jinsi wananchi wamejawa na huzuni wakiona jinsi wanavyodharauliwa na kunyimwa matunda ya uhuru. Anasema tuepuke marejeo ya kitabu cha Maombolezo (4:8-9) yanayosema:

> Nyuso zao ni nyeusi kuliko makaa, hawajulikani katika njia kuu; ngozi yao yagandamana na mifupa yao imekauka, imekuwa kama mti. Heri wale waliouawa kwa upanga kuliko waliouawa kwa njaa maana hao husinyaa, wakichomwa kwa kukosa matunda ya mashamba (uk.172)

Tunaona jinsi uhalisiajabu unavyojitokeza hata katika Biblia takatifu. Ni ajabu kuona binadamu mweusi kuliko makaa mwenye mifupa iliyokauka. Mara nyingi ndoto hubadilika na kuwa ukweli wa mambo. Ndoto hii ya Hikmat inampeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio yasiyowezekana katika hali halisi. Pia tunaona jinsi mtunzi anavyomgeuza mhusika mmoja, na kuchukua nafasi ya wahusika watatu au wanne. Badala ya kutumia wahusika wengi, mhusika mmoja anachukua nafsi ya wahusika tofauti jambo ambalo linawezekana tu katika mtindo huu wa uhalisiajabu.

Matukio ya kiajabu yanafanyika nyumbani mwa Lakeisha. Anamuona rafiki yake Bi. Saeeda Khan akimkata mwanawe Baingama miguu yote miwili na kunyofowa nywele za utosini na kisogoni. Lakeisha anawaona watu wasiofahamika wakimkata mwanawe mkono wa kulia na kuacha wa kushoto ukining'inia. Wanamfukua alikozikwa na wanaunyonga mwili wake hadi kufa halafu kukata

kichwa na ulimi huku mwanawe akilia kwa huzuni. Lakeisha anaona kitendo hiki cha ajabu cha mfu kunyongwa na mara sauti ya mama inasika ikisema: "AMEKUFA MARA MBILI" huku paka mkubwa akitokea na kukimbia. Mara Baingama anamuita na kumuuliza kwa nini analia na ajabu ni kuwa anapokataa kumjibu, mwanawe anamuuliza kama ametumwa na watu wanaotafuta zeruzeru kama yeye (uk.182-185).

Katika mahakama ya kiajabu, Baingama anaona jaji wa Gehenna akiwahukumu Bi. Saeeda Khan kwa kushiriki katika kuua zeruzeru na kunyofoa viwiliwili vyao kwa ajili ya biashara. Kwake Bi. Saeeda haoni mahakama hii ya Gehenna ikiwa na uwezo wa kuhukumu mtu kifo kwa ajili ya zeruzeru kwani ni baraka kupata zeruzeru, kumuua na kuuza sehemu za mwili wake kwa wapiga ramli, na anadai kuwa hata hospitali yake inatokana na mauzo ya viwiliwili vya zeruzeru (uk.187-188).

Katika mahakama hii, Bi. Saeeda na Bi. Rebecca Balira wanasukumwa pembeni mwa rusu ya *Chhaldabius* huku Mwanahamisi Mruke na Methodia waliowatesa wakiwa wafanyikazi wa nyumbani wanaendelea kupiga soga pahali pa starehe. Mara Baingama anasikia sauti ya mamake Lakeisha ikimuita na anashtuka anapogundua alikuwa amelala usingizi mzito ulioambatana na jinamizi kali. Mtunzi anamshirikisha msomaji anapouliza kama anafikiri ilikuwa ni ndoto (uk.189). Mtunzi kwa kutumia uhalisiajabu katika ndoto ya aina hii anamulika uovu unaotekelezwa na watu mashuhuri kufanya mazingaombwe. Wanasiasa,

wafanyibiashara na watu waovu wanatumia viwiliwili vya zeruzeru kupigia ramli ili watajirike huku wakipuuza haki za zeruzeru na kuwaona kama sio binadamu. Katika mahakama hii, mavazi mekundu kama damu yanayovaliwa na mahakimu pamoja na machozi ya damu ya washukiwa yanadhihirisha hatari.

Katika mandhari ya hospitali, tukio lingine la kiajabu linafanyika. Madaktari, wachungaji na wahudumu wa chumba cha kuhifadhia maiti wanashirikiana na wafanyibiashara haramu kukata viwiliwili vya maiti. Wanaelewa wazi kuwa binadamu wanaogopa binadamu wenzao wanapokufa, na hivyo hawana nafasi ya kuangalia sehemu zote za mwili kabla ya maiti kuwekwa kwenye jeneza. Baada ya kupanga ajali, kasisi Taabu anakimbia kuwaambia manusura kuwa binadamu anapowaumiza, Yesu atawaponya (uk.199). Waovu hawa wanatoa ulimi, masikio, macho na sehemu nyeti na kuweka katika friji na baadaye kuuza. Mara tunapata vichwa vya hadithi magazetini vikisema "BODY PART THIEVES HIT MORTUARY" na wahubiri kuendelea kuombea jambo hili. Ajabu ni kuwa zeruzeru wanauawa ili watu wajitajirishe huku wanasiasa wakitaka kujipatia kura na sasa wamemaliza zeruzeru wanavamia vyumba vya kuhifadhi maiti kutafuta nyeti za watu (uk 200).

Mauaji haya yanatokea wakati watu wanapata maagizo kutoka kwa waganga washirikina, tena matapeli wanaotumia nguvu za giza (uk.208). Mtunzi anaonyesha kuwa ushirikina ni ushirikina tu, uwe ni wa utabiri wa nyota, matumizi ya damu na viungo vya albino, kupiga ramli na kadhalika. Nafsi ya

Baingama inawaomba wananchi wapuuze ushirikina na kule kuamini katika sehemu za miili ya wafu ama albino. Anaendelea kusema kuwa kifo ni kazi ya Mungu na ndiye aliyetoa uhai kwa binadamu na atauchukua siku atakayopenda kwani kifo ni siri ya Mungu (uk.210).

Katika mandhari ya Mahakama, Takosani na Sikujua wanashtakiwa kwa makosa ya kumuua Yunasi na familia yake. Takosani anakiri kuwa yeye ni mtumishi wa shetani na amekuwa akiwasiliana naye tangu akiwa na umri wa miaka miwili na pia anatawaliwa na nadharia za ajabu na kuweka imani yake kwa msingi wa kitabu kimoja cha *The Codex Gigas.* Katika mandhari haya, tunaona wakili wake akimtetea kwa sheria zinazowalinda wenye matatizo ya kiakili lakini kwake Takosani anasisitiza kuwa yeye si mwendawazimu lakini ni mwenye imani ya dini ya kishetani (uk.212-218). Hapa, mtunzi anatoa mwanga jinsi mawakili hutetea washukiwa hata kama wametanda maovu bora tu walipwe na wajinufaishe.

Mahakama ya Gehenna inaendelea kuhukumu wahusika waliotenda mambo maovu. Kuna mchezo baina ya wahusika wawili wakubwa (Munkari na Nyamaume) na wahusika wengine wa Gehenna. Bi Saeeda Khan ni mhusika hewa asiyekuwepo ila jukumu kubwa ni kuwa mchezo unachezewa fikrani mwake. Anapuliza parari kubwa kuwaita watu wa Gehenna waje wahudhurie hotuba. Munkari anawahutubia halaiki hii kubwa akiwa amebeba hinzirani kubwa na kibogoshi chenye mafuvu ya watu. Wanaohutubiwa wanalia na kutoa sauti za

popobawa, lakini ni wakati wa kupewa mhadhara kwa dhambi walizotenda duniani (uk.221). Munkari anawaeleza kuwa wako pale kwa hiari yao wala hawakuletwa na yeyote na anawahoji kwa sababu ingawa wamekufa wao ni T*he living dead* (uk.221). Anawaeleza kuwa wameshiriki uongozi mbaya unaosababisha kutikisika kwa Kiafra huku akisisitiza ufisadi ung'olewe kwani *mafamba* ni hatari na ufisadi ni ugonjwa (uk.222). Mhusika huyu wa kiajabu anaeleza kuhusu athari za utandawazi ambapo mafisadi huhamisha utajiri wa Kiafra kwenda kutajirisha nchi nyingine (uk. 224).

Kwa kutumia mchezo huu wa *The Matrix of the corruption in Kiafra* ambao unafanyika fikrani mwa Bi. Saeeda na ambao ni tukio la kiajabu, mtunzi anatumia mhusika wa kiajabu anayeangazia maovu yanayotendeka katika nchi za Kiafra. Munkari anasema kuwa, anaohutubia ni wanaoshiriki ufisadi na anamwamuru Nyamaume avuvie moto (uk. 242). Nyamaume anavuvia moto maradufu na kilio kikali, mayowe na sokomoko kutoka kwa wanaohutubiwa zinaongezeka. Mchezo huu wote unafanyika fikrani mwa Bi Saeeda Khan ambaye ni mmojawapo wa watu wa Gehenna.

Kuna safari ya kuelekea Nahegen na kondakta amejaza gari kupita kiasi na pia gari linaendeshwa kasi ya kilomita 666 kwa saa. Gari linagonga shimo kubwa na dereva anashindwa kulidhibiti kwani linaenda kasi, mafuta yanavuja na moto kuwaka na ghafla mlipuko mkubwa kusikika huku moto ukisambaa kwa kasi na kuangamiza abiria wote wakawa majivu. Ajabu ni kuwa abiria mmoja kwa jina

Angamizamtuwewe II hakufariki. Tukio hili linafanyika huko NdaRwa na mara watu wa Gehenna wanafika katika mandhari ya ajali huku wakisherehekea na kuihesabu mifupa na kutoa hukumu (uk. 243-250).

Matukio mengi yanafanyika katika mandhari ya ndotoni hata ingawa katika hali halisi yaliwahi kutendeka katika nchi fulani. Mfano ni ndoto hii ya kondakta ambayo hata kama mtunzi hajasema nchi hiyo ni gani, inaonekana ni nchi ya Rwanda ambapo maelfu ya watu waliuawa katika vita vya kikabila na ilivyobaki ni watu kwenda kuhesabu mafuvu na mifupa iliyohifadhiwa.

Naye Faki Nahodha anazindushwa na mlio wa arafa ya ujumbe mfupi unaotoka parokia anayohudumu kasisi Taabu akitakikana huko kwa mipango ya mazishi kwani kasisi Taabu amepatikana kwenye madhabahu ya kanisa akiwa amejitia kitanzi. Anapofika huko parokia, haamini anachokiona na hivyo anapigwa na mshangao wa ajabu. Anampata kasisi akinywa chai, huku anasoma gazeti la *The Tombstone Epitaph* ambapo kasisi mmoja anashtakiwa kwa kumnajisi msichana wa umri wa miaka 13 kwenye madhabahu ya kanisa. Hii ni sadfa kwani kasisi Taabu alikuwa amefumaniwa na kibiritingoma mwingine wakiwa katika mahaba mazito kwenye madhabahu huku wanakunywa divai chapa *Blasted Church.* Ghafla, kasisi Taabu anamuuliza Faki Nahodha kama amuongeze chai. Faki anashtuka kwani kadhia hiyo yote inafanyika akilini mwake kwa kipindi cha sekunde sita pekee, pale pale anapokaa na kasisi Taabu (uk.253-257).

Mtunzi anatumia mandhari ya uhalisiajabu kwenye fikra za mhusika wake ili aonyeshe jinsi uovu umekithiri hata makanisani. Wachungaji wenye jukumu la kuchunga kondoo wako kwenye mstari wa mbele kunajisi wasichana wadogo huku wakijihusisha na vibiritingoma. Pia wanafuja pesa za kanisa na kunywa divai na wapenzi wao.

Nafsi ya Hikmat inachipuka tena na inaongea na Hikmat. Ni ajabu kuona mhusika anajadiliana na nafsi yake na kutoa uamuzi. Katika mandhari haya, uamuzi unapatikana kuwa, ukosefu wa vifaa muhimu hospitalini na shuleni, barabara mbovu, kiu na njaa inayowakabili Wakiafra inatokana na jinsi taasisi zinavyoongozwa kwa njia mbaya. Kuna hurafa mbalimbali ambazo zimetolewa kuhusu chanzo cha ufisadi. Hurafa moja ni kuwa, wakati wa enzi ya kiongozi fulani wa Kiafra, falsafa iliyoeleza ufisadi ilikuwa "kanyoni *gakwa wihithahithe na wonwo nduri wakwa"* yaani ndege wangu mdogo, endelea kujificha na utakapopatikana, hutakuwa wangu (uk. 263). Hivyo huu ndio ulikuwa msingi wa ufisadi lakini wakati kiongozi wa pili anapochukua hatamu za uongozi, falsafa ile inabadilika na kuwa "*Kanyoni gakwa oya kiria giothe uroya onawonwo turi o hamwe"* yaani ndege wangu mdogo chukua chochote utakacho na hata utakapopatikana sote tungali pamoja. Hivyo wanaume na wanawake wanaendelea kuharibu raslimali za nchi na kutumia hazina ya uzeeni kujinufaisha bila kuwajali wakongwe waliostaafu. Nafsi ya Hikmat inaendelea kumueleza kuwa hii ndiyo sababu historia ya taifa itakayosimuliwa na kuandikwa sura kama vile G.berg,

Mol Ashes, A. leasing, F.P.E.P, Makaburi na nyinginezo kutengeneza historia (uk. 264-266).

Mara mkewe, Takosani binti Abadalla mkewe anamwamsha Eks huku amelowa jasho na kuonekana kama alikuwa kwenye jinamizi. Anapofumbua macho, anajiona na kuiona dunia halisi. Ni tukio la kiuhalisiajabu jinsi mhusika huyu anavyobadilika na kuchukua maumbile ya wahusika wengi tofauti tofauti. Anakumbuka vema kuwa huko (ndotoni), alikuwa anazinduka, mara analala, mara anaamka, mara anafariki, mara anafufuka, mara yumo Gehenna, mara anateketea, mara yu baharini. Anachotaka kujua ni; nini kilitokea, mbona kilitokea, lini kilitokea, vipi kilitokea, wapi kilitokea na nani alifanya kitokee. Anapatwa na woga huku akifikiri matukio yote yaliyotokea ndotoni na anajaribu kuyasukuma nyuma. Anachokumbuka ni kuwa kabla ya kuupata usingizi ule mzito na kuzama katika jinamizi alikuwa ameusoma ukurasa wa mwisho wa riwaya ile yenye picha ya jalada na mifano ya watu wengi wakiwa katika bahari kubwa ya moto mkali wakiwa wanalia huku wamesimama kwa maumivu makali na kutoa machozi ya damu- riwaya ya *Watu wa Gehenna.* Asipojua hakika ni ikiwa yeye yu hai au mfu. Tunaona jinsi mitindo ya mbinu rejeshi na ukumbukaji inavyotumika katika mtiririko wa riwaya nzima.

### 4.2 WAHUSIKA WAKUU

Katika riwaya hii ya *Watu wa Gehenna,* mtunzi ametumia wahusika halisi na wahusika wa kiajabu katika kuendeleza dhami ra na maudhui ya kazi husika.

Kutokana na kushiriki katika matendo na migogoro muhimu katika kazi hii, tumetambua wahusika wakuu wawili ambao mtunzi amewapa uwezo wa kubadilisha nafsi na maumbile yao na kuchukua maumbile ya wahusika wengine tofautitofauti. Wahusika hawa ni Eks Ngwenyama na Takosani Binti Abdalla. Aidha, haya yote yanafanyika mawazoni mwa wahusika hawa wawili wakuu. Mtunzi amewaumba wahusika hawa kwa ustadi mkubwa hivi kwamba, ni vigumu kutambua wakati wanabadilika kutoka nafsi moja hadi nyingine ama kutoka mhusika mmoja na kuchukua maumbile ya mhusika mwingine ( uk 266-267).

### 4.2.1 Mhusika Eks

Eks ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* na jina lake kamili ni Eks Ngwenyama. Ni mhusika wa kiajabu sana kwani nafsi yake inabadilikabadilika. Kawaida nafsi yake haikuwa inalala lakini ajabu ni kuwa siku moja inaamua kulala. Sauti ya mbali sana inamwambia nafsi yake imelala, lakini yeye hajui ataiamsha namna gani na ndiyo inayompa mwelekeo.

Ni mhusika ambaye pia anabadilika na kuwa mhusika tofauti. Eks anabadilika na kuchukua nafsi ya wahusika halisi. Mwanzoni mwa riwaya (uk 10), tunampata Eks akizungumza na nafsi yake kama mhusika tofauti. Kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi, anaendelea kubadilikabadilika. Mara, anageuka na kuwa Sikujua, mara Mwalimu Baya, mara Yunasi, kasisi John, Baingama na mara Hikmat.

Ni katika fikra au akilini mwa Eks tunapopata mandhari ya kufanyika hadithi hii akiwa ndotoni. Eks anazungumza na nafsi yake ambayo inamhoji na kumuuliza binadamu ni nani. Anaposhindwa kujibu nafsi yake inamcheka. Kicheko hiki cha ajabu cha nafsi yake ni ishara ya kujicheka kwa binadamu kutokana na kushindwa kudhibiti maisha yake.

Eks ameifanyia kazi kampuni ya THE WORLD CEMENTES INC. kwa muda wa miaka 40 na wakati anapopatwa na matatizo ya kiafya anafurushwa (uk 10-17). Kwa hivyo, hapa Eks anawakilisha binadamu halisi na jinsi wanavyodhulumiwa na waajiri wasio na utu. Pia, hajafanikiwa kupata mtoto kwani shahawa zake zinapatikana na kasoro kulingana na madaktari. Eks na mkewe wanaishi maisha ya starehe na kula chakula kizuri kama vile nyama choma na mvinyo kinachomfanya awe na kitambi kinachomzuia kuvaa nguo anazotamani, kutembea, kufanya kazi za nyumbani, kuendesha gari, kuinama kuchukua ufunguo na pia kutekeleza kitendo muhimu cha ndoa (uk.18-19).

Eks anakalia kiti cha jeuri na kuendelea kumlaumu Mzee Afisul kwa kumpa ugonjwa na vilevile kumchukua mkewe. Kwake Eks haoni kama ni ndoto lakini anasikia sauti ya mzee Afisul ambayo haikumtisha. Ni mhusika shupavu na anamuuliza kama yeye ni shetani, Mzee Afisul anakana na kuendelea kumpa fomula ya akili ya binadamu, na kuwa Gehenna imo akilini mwa binadamu.

Eks kama mhusika wa kiajabu ana nafsi mbili. Nafsi yake ina uwezo wa kumuamuru afe na vilevile afufuke. Tunaambiwa ya kuwa baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kulichukua miaka saba. Katika miaka hiyo saba MKUU na EKS wanaulizana na kujibizana maswali. Katika nadharia ya uhalisiajabu, tunapata wahusika wakiajabu wakifanya matukio ya kiajabu.

Eks Ngwenyama ni mhusika ambaye ana uwezo wa kubadilikabadilika na kuchukua maumbile ya wahusika wengi tofauti tofauti. Mara anazinduka mara analala, mara anaamka, mara anafariki, mara anafufuka, mara yumo Gehenna, mara anateketea, na mara yu baharini. Ni mhusika aliyekata tamaa na kutaka kujua nini kilitokea, mbona kilitokea, lini kilitokea, vipi kilitokea, wapi kilitokea na nani alifanya kitokee. Anapatwa na woga kwa yale yote amepitia na kile ambacho hajui ni ikiwa yeye yu hai au mfu (uk. 266-268).

Mtunzi ametumia mhusika EKS na kufinyanga fikra zake akachukua maumbile ya wahusika wengi huku akidhihirisha uovu katika jamii. Ingawa kuna wahusika wengi, katika riwaya hii ya watu wa Gehenna, wahusika ni wawili tu ambao ni Eks kama alivyo mhusika K katika *Babu Alipofufuka* na Takosani binti Abdalla. Hawa wawili wametumiwa na mtunzi kuwakilisha wahusika wengine katika nafsi zao.

### 4.2.2 **Takosani binti Abdalla**

Takosani ni mhusika wa kiajabu ambaye mtunzi amemuumba kama mhusika anayebadilikabadilika na kuchukua nafsi za wahusika wengine. Kama mhusika halisia, anapenda kuona mumewe Eks anakula chakula kizuri. Pia hajafanikiwa kupata mtoto. Anatembelewa na ziraili magharibi ya siku ya kwanza ya mfungo sita na anaenda zake jongomeo na kumuacha Eks.

Tunamuona Takosani akibadilika na kuchukua nafsi na maumbile ya wahusika tofauti. Anabadilika na kuwa Takosani binti Inatesh (yaani binti shetani), mhusika wa kiajabu. Ni mwenye nia mbaya na anataka kumteka mhusika kwa jina Sikujua na kufanya mapenzi naye na hivyo kumnasa awe mfuasi wake. Ni mdanganyifu kwani anasema kuwa wanaume ni waongo ilhali anamnasa Sikujua. Ni mwenye uchu wa mapenzi na anasema angependa mwanamume mwenye mapenzi ya kweli. Kwa ustadi mkubwa anamuonya Sikujua kuwa akimjua kabisa hatamuweza kwani hajui jinsi anavyoishi, anachokula na kunywa na starehe zake. Aliwahi kufunga ndoa na Mwarabu lakini ndoa ile ikavunjika baada ya siku saba na hivyo anaamini wanaume ni wakorofi na anaonelea vyema kubaki peke yake (uk. 41-42).

Takosani binti Inatesh ni msiri na mlaghai kwani analia kwa uchungu akimwomba Sikujua asimuoe kwa maana hangeweza kuyatii masharti yake lakini haya ni machozi ya mamba. Anafanya matendo ya kushtua na kuogofya lakini kwake Sikujua anashindwa kudhibiti hisia zake juu yake kwa sababu ya urembo

wake huku akisahau sio vyote ving'aavyo ni dhahabu. Ana mazoea ya kuombea kaburi la mama yake lililoko Kizingitini kisiwani Pate, huku akilipigia magoti na kuliwekea sarafu na lazima kila usiku aamke na kwenda makaburini. Anaposafiri, lazima aombe ruhusa mizimu yake iridhike na sarafu yake ambayo kwao ni salamu. Uraibu wake ni kuogelea baharini na macho yake yanabadilikabadilika na kwa hivyo anavaa miwani (uk. 42-43).

Katika mandhari ya hoteli ya *Anneheg Xpress* katika mtaa wa *Reciful Meadows,* Sikujua analipia vyumba viwili, chumba nambari 15 na chumba nambari 18 lakini Takosani anataka chumba nambari 13 na hivyo kumtaka Sikujua abadilishiwe chumba kile. Chumba kinapatikana ambacho kimeandikwa "*Room Thirteen*" kwa rangi nyekundu tena nzito sana kama rangi ya damu. Ni mwenye kupenda mahaba na anateta anahisi joto kali na kuomba apunguze nguo huku Sikujua akifarikija moyoni akimuona akiendelea kutoa nguo zote kwani kwake huu ulikuwa ushindi mkubwa. Kwake chumba nambari 13 ni cha maana sana cha kumwezesha kutekeleza shughuli zake lakini Sikujua mhusika wa kiuhalisia hang'amui chochote (uk. 44-45).

Anapenda kujipulizia manukato makali aina ya chapa *poison* yanayomfanya Sikujua apate tabu kupumua ilhali haonyeshi kukerwa na harufu hiyo. Ajabu nyingine ni kuwa Takosani anaondoka kwa kupitia ukutani na anaporudi chumbani harufu ya manukato inamtanguliza. Anamwambia Sikujua kuwa angetaka kumpa utajiri jambo linalomfanya Sikujua amuulize kama yeye ni jini.

Anaseme yeye si jini na hadithi za majini haziamini lakini hangethubutu kumpa utajiri ingawa ana uwezo kwani akiwa tajiri atamsahau Mungu.

Pia ana uwezo wa kumfanya Sikujua apoteze fahamu na pia kumpeleka makazi yake chini ya bahari jambo ambalo linamfanya Sikujua ashindwe kama anaota ndoto au ni hali halisi kwani haoni jinsi mandhari yanavyobadilika. Anamueleza Sikujua kuwa makazi yake ni chini ya bahari na kuwa duniani anafika kutekeleza shughuli maalum. Anapenda nyimbo na anataka Santuri ya MWAKA WA SHETANI. Ajabu ni kuwa Sikujua haelewi kuwa katika dunia ya akina Takosani maneno huandikwa kinyumenyume na hivyo basi ni vigumu binadamu halisi ambaye sio wa dunia yao kung'amua maana yake. Anapodadisi santuri zile anapata santuri iliyoandikwa kwa rangi nyekundu tena nzito *inatesh aw akawn* na mchoro mkubwa wa ngorombwe upande mmoja na upande wa pili umechorwa picha ya parari. Anaeleza kuwa mwaka fulani unaweza ukawa wa shetani hivi kwamba kila unachotaka kufanya hakitimii na kila mpango unavurugika. Mambo haya yanamfanya Sikujua asijue kama anaota ama ni hali halisi lakini ukweli ni kuwa hali halisi na ndoto ni kitu kimoja (uk. 48-52).

Mtunzi anatumia mhusika huyu wa kiajabu kudhihirisha kuwa katika maisha ya binadamu, matukio haya ya kiajabu hutokea hata kama ni ndotoni na kuwa mara nyingi mambo haya yanaonekana kama ya kiajabu lakini yanakuwa halisi kwani baadhi ya watu wanaabudu shetani na nguvu zingine za giza na wakati tunapotagusana nao katika maisha halisi, matukio ya aina hii yana uwezekano wa

kutokea. Pia anataka msomaji aelewe kuwa, ni vigumu kuwatambua wahusika wa kiajabu miongoni mwa binadamu halisi.

Katika fasihi simulizi za jamii nyingi za Afrika, watoto walikuwa wamefunzwa kuhifadhi siri kwa wageni na pia kutowafuata kwa vile hawakuelewa nia zao. Katika hadithi moja kutoka jamii ya Wakikuyu, wasichana walienda kucheza densi kama ilivyokuwa kawaida baada ya mavuno. Wasichana wale walipatana na kijana mmoja mtanashati na wote wakapendezwa naye. Sherehe ilipokwisha, wasichana kumi walimfuata kwani kila mmoja alitamani kuolewa naye. Njiani, yule kijana alikuwa akiwashika nzi na kuwaweka kisogoni mlimokuwa na kinywa kilichokuwa kimefunikwa na nywele. Msichana aliyekuwa nyuma yake aliona kitendo kile cha ajabu na kugundua kijana huyo alikuwa jini na hivyo akawaambia wenzake kuwa hataendelea na safari kwani alikuwa ametumwa na mzazi wake kwenda kuteka maji. Kila mmoja alipata nafasi ya kuona kitendo cha kumega nzi na wasichana tisa wakajipatia sababu za kutoendelea na safari akabaki mmoja ambaye hakutaka kumuacha. Walipofika nyumbani kwa yule kijana, ajuza mmoja alishtuka kumuona na akamueleza kuwa yule ni jini na alikuwa amemnasa kule ili awe akimpikia wasichana warembo. Yule ajuza alimnusuru na kumuonya kuwa, sio chote king'aacho ni dhahabu.

Kutokana na hadithi hii, tumebainisha kuwa uhalisiajabu ulitumika sana katika fasihi simulizi za jamii nyingi na hutumika kuwaelimisha, kutahadharisha na kuwaonya watu kuhusu dunia wanamoishi. Kisa hiki kinafanana na kisa katika

riwaya hii ambapo Sikujua anaona bahati ya kupata msichana mrembo, na hata baada ya kuona matukio ya kiajabu anayoyafanya, yeye amenaswa na urembo na mapenzi kwa mtu asiyemjua hakika.Vilevile, mtunzi, anaonya jamii kutojihusisha na watu ambao hawaeleweki vyema mienendo na nia zao.

Takosani ni muuaji kwani anasababisha kifo cha Yunasi na familia yake. Takosani na Sikujua wanaonekana watumiaji wa dawa za kulevya, wamejichora picha za kutisha katika miili yao, kujitoboa toga masikioni, puani, kwenye ulimi, kidevuni, midomoni, kwenye nyusi na kujivika vipuli na kukata nywele zao kwa mtindo wa kiajabu. Anavaa mavazi meusi yenye michoro ya mafuvu ya watu na joka kubwa na pia yenye maandishi ya kiajabu yaliyoandikwa kwa rangi nyekundu *Oxyuranus mirolepidotus.* Mikononi amejichora *Dragon yin yang* wa Uchina na fomula ya nishati ya $E=MC^2$. Fulana yake imeandikwa swali na jibu; *"Do we not possess superior intelligence? We Simply do" (uk. 215).*

Ana nguvu za kiajabu kwani anaiba bunduki aina ya metal storm na makasha mawili ya risasi kutoka kwa afisa mmoja wa kitengo cha udhibiti wa silaha. (uk. 214-215). Anapopelekwa mahakamani anakiri kuwa yeye ni mtumishi wa shetani na kuwa amekuwa akiwasiliana naye tangu akiwa na umri wa miaka miwili, pia ni mpinzani wa masihi Yesu Kristu na ni binti wa shetani hivyo Takosani binti Inatesh. Ameweka imani yake kwenye *The Codex Gigas* biblia ya shetani. Wakili wake anapomtetea kuwa ana matatizo ya kiakili kwani watu wa aina hii wanalindwa kisheria, anaamini kuwa yeye sio mwendawazimu na anaongezea

kuwa ana mpango unaoratibiwa na baba yake shetani wa kuwaandaa vijana wote duniani waasi (uk.216-218).

## 4.3 WAHUSIKA WADOGO

Wahusika wadogo katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* wamechukua nafasi kubwa katika kujenga dhamira na vilevile katika ujenzi wa wahusika wakuu ambao ni Takosani binti Abdalla na Eks Ngwenyama. Aidha wahusika hawa wadogo ni wengi mno lakini kwetu tunaangalia wahusika wa kiajabu watakaotusaidia kuwekea misingi nadharia hii ya uhalisiajabu.

### 4.3.1. Mishi

Mishi ni mhusika wa kiajabu anayeonekana na mara kutoweka kiajabuajabu. Kutoka fasihi ya Ugiriki wa kale, kuna mhusika wa kiajabu kwa jina Muse mwenye nguvu za kiajabu na tunaweza kumlinganisha na Mishi katika *Watu wa Gehenna.* Ni mhusika muhimu sana katika kuendeleza riwaya na kudhihirisha uhalisiajabu katika hadithi. Tunapata Mize mhusika muhimu katika riwaya ya *Dunia Yao*, mwenye sifa za kiajabu kama Mishi. Mishi ni mhusika wa kiajabu anayeingia riwayani akiwa kama dhana kwenye akili ya mhusika Mwalimu Baya. Ana uwezo wa kujipa mwili wa kumvutia Mwalimu Baya, kama mwanamke wa kutamanisha. Mwalimu Baya anatamani sana kufanya mapenzi naye.

Mishi kama mhusika wa kiajabu ana uwezo pia wa kukwamisha gari la Mwalimu Baya katikati mwa reli treni inapokuwa inakuja kwa mwendo wa kasi. Mara kwa

mara, analitamka jina *Shemhamforash!* kila wakati tukio la kiajabu liko karibu kutokea. Haonyeshi dalili ya kufahamu hatari inayowakabili ya kugongwa na treni na wala hana hofu. Anamkumbatia Mwalimu Baya mikononi mwake na hivyo ana uwezo wa kiajabu wa kumuokoa binadamu halisi na kumfumba macho asing'amue kinachotokea. Mabehewa ya treni yanapita ndani yao kama waliokuwa mizuka huku wakiona viti, watu na kila kitu ndani ya treni huku treni inakwenda kwa kasi. Lakini kwake Mishi hili ni jambo ambalo si ajabu. Anaashiria nguvu za giza zinapompiga Mwalimu Baya kwenye kisogo na kumfanya aanguke chini kama gunia la mchanga.

Ni mhusika anayejibadilishabadilisha kiajabu kwani wakati mmoja mwalimu Baya anamuona na viatu vya wazi na mara miguu yake inabadilika na kuwa kwato za ng'ombe huku Baya akimuona jini lakini asiweze kujinasua kwake. Pia ana uwezo wa kuingia popote wakati wowote na kupitia popote hata ukutani bila binadamu halisi kufahamu. Ana uwezo pia wa kutawala nafsi ya binadamu halisi (Baya) kwa kumfanya alale usingizi mzito na kuota ndoto huku akiendelea kufanya mapenzi naye. Anajibadilisha mwili na mgongo wake kuwa na magamba na mara mwili unakuwa baridi kama barafu.

Mwili wa mhusika huyu wa kiajabu una uwezo wa kutoa mwanga wenye rangi ya mbalamwezi angavu. Mara mwili wake unageuka na kuwa kila kitu nusu toka juu hadi chini yaani jicho moja kwenye paji la uso wake, titi moja, mkono mmoja, mguu mmoja, nusu ya kila kitu.

Ajabu ni kuwa Mishi alikuwa mke wa Shehamforash na hivyo ni shetani wa mahaba na pindi tu mwanamume analala naye katika ndoto, anateuliwa na kupata laana kuwa hatalala na mke mwingine hadi kifo. Hivyo, amemteua Mwalimu Baya na kumning'iniza juu ya mti wa mbuyu akiwa uchi wa mnyama.

### 4.3.2 **Shamsa Muhashamy (Baadayadhiki)**

Mhusika Shamsa ni mhusika wa kiajabu na anaishi makaburini. Ni mpweke kwani anaishi peke yake kwa muda wa miaka miwili na chakula chake kikiwa maji ya marashi. Ni rafikiye Takosani anayependelea kumuita Baadayadhiki. Shamsa ni mpiga ramli na anasema alianza kupiga ramli kule Mbwajumwali na kuhamia Mombasa baadaye. Ni msimulizi hodari na kupitia kwake, tunapata kisa cha mwanasiasa mmoja kwa jina Vuai Nahodha alivyopewa wadhifa wa Waziri wa Afya na kushindwa kutekeleza wajibu wake. Anaeleza kuwa, mwanasiasa huyu aliweza kuwasiliana na madaktari wa vituo vya afya vya Tandauwa, Ndagoni, Wingwi, Makangale na Bogoa kupata kuchukua sampuli za damu za wagonjwa na baadaye kupanga njama ya kufyonza damu mbichi chupa 40 na kutupa miili ya wagonjwa. (uk.70). Anaelewa mambo halisi jinsi haki za wanyonge zinavyokiukwa, ufisadi na kuondolewa jamii fulani katika eneo fulani na kupiganisha makabila ni mambo yanayorudisha maendeleo nyuma katika Kiafra. Mtunzi anamtumia kufichua siri za wanaotenda maovu.

4.3.3. **MKUU**

MKUU ni mhusika wa kiajabu na ambaye anapatikana akilini mwa mhusika Eks. Ni mhusika mwenye uwezo wa kumhoji na kumuelimisha Eks. Akiwa kama nafsi ya Eks, anamuamuru Eks afe halafu afufuke. MKUU anamlaumu Eks kwa kupokea maelezo maovu kuhusu mchezo wa Sataranji kutoka kwa Mzee Asiful na ndio maana anamwamuru afe. Baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kunakochukua miaka saba, na ni katika miaka hii ambapo MKUU na Eks wanaulizana na kujibizana maswali.

Ana uwezo wa kujua yanayotendeka na vilevile anayoyaona Eks akiwa amelala. Mkuu anaelewa wazi kuhusu dunia ilivyoumbwa na kuwa Mungu mwanzo aliumba ardhi kavu, akafinyanga konde, akawaumba wanyama na samaki… kabla ya kumuumba Eks, kwa maana ya binadamu. Ni mwanasayansi anayeelewa umuhimu wa majani na matunda katika kuimarisha afya ya binadamu. Ni mwalimu na ana utaratibu wa kuuliza na kujibu maswali kwani anamuelimisha Eks kuhusu lishe bora. Anamwamuru Eks asiukaribie mlango wa Gehenna. Ana uwezo wa kufyatuka na kufifia angani.

MKUU anaelewa vyema matatizo ya watu duniani hasa matatizo ya kiafya. Anaelewa kuwa mataifa ya Kiafra yana uchache wa hospitali, madaktari na dawa na hii imechangiwa na kutotilia maanani dawa za asili huku wakizikumbatia zile za nchi za magharibi ambazo ni wachache tu wanaoweza kuzigharamia. Kwake, dawa hizi ni zile ambazo muda wake wa kutumia umeisha au zile zinazofanyiwa

majaribio kwa mara ya kwanza na ni zenye athari ambayo haijafahamika. Hivyo wanatumika kama vipanya vya maabara.

Ni mwenye hekima na anapoulizwa na Eks kama ana ushahidi kuhusu madai yake, anatoa majibu kuyatetea maoni yake kuwa katika enzi za mababu wa akina Eks, kila ugonjwa ulitibiwa na aina fulani ya miti shamba na kulikuwepo na watu wa kufanyia utafiti dawa hizo. Anapendekeza kuwa watafiti hao wangeendelea, kungepatikana dawa ya ukimwi.

MKUU ana uwezo na nguvu za kiungu. Anamrejelea Mungu pamoja na maandiko matakatifu kwa ustadi. Anasema kuwa Mungu alipomuumba mwanadamu, alimwekea duniani kila aina ya miti kwa matumizi mbalimbali na moja ya matumizi hayo ilikuwa ni dawa. Kwa hivyo, tatizo la kuendelea kuumwa wakati kuna dawa silo tatizo la Mungu ila ni la binadamu. Anasema:

> Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu
> watajinyenyekeza watubu dhambi zao na kuniomba, mimi
> nitasikia kutoka POPOTE na kuiponya Kiafra. Nadhari
> njia ya peponi (uk 37).

Mtunzi anamtumia MKUU kudhihirisha nguvu za kiungu. MKUU anajua kuwa tatizo la Wakiafra ni kufikiri kuwa utaalamu wa bara jingine ni bora kuliko ule wa kwao. MKUU anatahadharisha maendeleo kama adui mkubwa wa binadamu huku akijiita '*INTELLIGENT!*' Binadamu anapotengeneza ndege, basi anahitaji utaalamu wa kutengeneza mahali pa kuegesha hewani ili irekebishwe

inapoharibika. Kwake Mungu amempa binadamu uhuru wa kufanya atakavyo na kwa hivyo akitengeneza umeme halafu umchome, asimlaumu Mungu kwa maana umeme sio moja ya vitu alivyoweka ulimwenguni pale mwanzo, na YEYE hajui umeme ni kitu gani. MKUU anawalaumu madaktari ambao wamepewa hekima na Mungu na badala yake wanawatoza wagonjwa pesa nyingi ili wajinufaishe.

### 4.3.4 **Munkari**

Munkari ni mhusika wa kiajabu na ambaye ni hakimu wa Gehenna. Ni mlinzi mkali na tunamwona akimzuia Yunasi kumwokoa mkewe Saida kwani yeye si mtu wa Gehenna (uk.219). Akisaidiana na Nyamaume, wanawazuia Bi Saeeda Khan na Bi. Rebecca Balira wasitoroke Gehenna ili wapate adhabu ya maovu waliotenda – huku wakitumia neno Nobe! Anajua maovu yote ambayo kila mshukiwa ameyatenda na hivyo yuko tayari kuwasomea mashtaka na kuwapa adhabu kali (uk. 226-227).

Anapendelea michezo ya kuigiza wakati anapotoa hukumu huku akishirikisha wahusika wa Gehenna kama vile Bi Saeeda ambaye mchezo umo fikrani mwake. Munkari ana jukumu la kuwakaribisha watu Gehenna (uk. 248-252). Pia ana uwezo wa kuchipuka ardhini kiajabu huku amevaa sare nyekundu kama damu na kuanza kucheza na kasisi Taabu aliyemdhalilisha kijinsia binti mmoja kwa jina Kinaya katika madhabahu ya kanisa wakati alikuwa padre. Anaielekeza bunduki kichwani na kujifyatulia lakini hakuna risasi inayotoka na anapomwambia kasisi Taabu ajifyatulie, risasi inatoka kwa hakika na kuufumua nje ubongo wake huku

watu wa Gehenna wakiukimbilia. Anaeleza sababu ya kasisi kupata adhabu hiyo ni kwa kutokuwa mwaminifu katika kiapo chake cha useja (uk. 255).

Munkari anaonya kuwa watenda dhambi wote watahukumiwa na kupewa adhabu kali siku moja baada ya maisha ya duniani.

### 4.3.5 **Hikmat**

Hikmat anatokea kama mhusika halisi ambaye anazindua rasmi kampeni za ubunge pale Ndotoni. Ni mwenye maarifa na anapongezwa na wananchi kwa kuzindua manifesto yake yenye ushawishi mkubwa na ahadi zenye kupigania uhuru wa nchi za Kiafra hata ingawa uhusiano wao na nchi za kigeni utadhoofika (uk. 159). Ni mhusika mwenye nafsi mbili. Moja ya Hikmat yeye anayetimiza ndoto zake kikweli na Hikmat mwingine mwanasiasa anayetimiza ndoto zake kibahati.

Ni mfuasi wa kipindi cha *The Night of the Living Dead* kwenye runinga kwani kinaleta mjadala kuhusu changamoto katika nchi za kiafra. Ana uwezo wa kuchangia mjadala huu moja kwa moja na ajabu ni kuwa anageuka kuwa mtangazaji nao watangazaji watatu ambao ni Ikmat, Kmat na mat wanakuwa watazamaji. Nafsi yake ndiyo yenye wahusika Ikmat, Kmat na Mat na mjadala unafanyika akilini mwake lakini unaonekana kama mjadala halisi. Nafsi yake na yeye wana mazoea ya kufanya dayalojia pamoja hasa kuhusu uongozi mbaya unaosababisha kusambaratika kwa nchi za Kiafra (uk. 263-266).

Ni mtetezi wa wanyonge na anakashifu jinsi wabunge kama wawakilishi wa watu wanavyosimama bungeni kudai nyongeza ya posho zao badala ya kuomba sehemu ya mishahara yao ikatwe kwa ajili ya kugharimia operesheni kwenye kaunti zao ili kuonyesha upendo wao kwa wananchi (uk. 176).

### 4.3.6 **Watu wa Gehenna**

Watu wa Gehenna ni wale walioshiriki matendo maovu wakiwa duniani. Wana walinzi wao na mahakimu wao. Wakazi wa Gehenna wana tabia za ajabu sana na kila mmoja wao anajiona afadhali kuliko mwenzake lakini uovu ni uovu na watendao maovu wote ni watu wa Gehenna. Ni wakazi wanaoonekana wakiwa kwenye bahari ya luja au biwi la simanzi na wako kwenye lindi la fikra nyingi.

Ni wabinafsi na kila mkazi wa Gehenna anafuata ajenda yake na kwa hivyo hawana ushirikiano. Hawa ni watu wanaojuta kwa sababu walishiriki katika ukataji misitu, kuwanajisi wasichana, kuiba dawa za hospitali, kupokea rushwa, kupiga ramli, kuua, na kuuza viwiliwili vya albino, kueneza ukabila, kuwapunja wafanyakazi wao, kushiriki ufisadi baadhi ya maovu mengine.Hapa Gehenna, wanawekewa muziki unaoitwa *walijuta* ambao unachezwa kuwakumbusha maovu waliyoyatenda (uk. 8).

Wakaazi wa Gehenna ni wengi na ingawa wanaweza kufanya kazi kwa ushirikiano, azimio lao hasa ni kujitosheleza kibinafsi. Ni watu ambao hawajali kinachofikiriwa na wenzao wanapojitosheleza. Vilevile ni watu wajanja, wenye

akili na kuzidi yote, watu hatari. Siri yao kubwa ni kujitia katika ndoto ya utendaji huria yaani hakuna chochote ila hiari ya mwenye nguvu na hiari ya mnyonge na kila mkazi ana ajenda yake ambayo hamfichulii mwenzake (uk. 9).

Bi Saeeda Khan na Bi Rebecca Balira ni baadhi ya wakazi wa Gehenna wanaohukumiwa kwa kuwatesa wafanyikazi wa nyumba na kuwaua zeruzeru na kuuza viwiliwili vyao (uk. 187). Wote walioangamia kwenye ajali ya barabara huko Nahegen pia ni wakazi wa huku.

Wakazi waliotangulia Gehenna ni watu wanaofurahia wakati kuna tukio la kiajabu litakalowawezesha kuongezeka kama vile mauaji ya kikabila na ajali za barabarani. Baada ya muda fulani, wanakuwa na sherehe za kuihesabu mifupa na kutoa hukumu wakiongozwa na Munkari (uk. 250-252). Watu wa Gehenna ni wahusika wa kiajabu kwani wakati kasisi Taabu anapojifyatulia risasi na kuufumua nje ubongo wake, watu wa Gehenna wanaukimbilia ubongo huo na kumkaribisha awe mtu wa Gehenna. (uk. 255)

Wengine wao ni wauaji na wengine walevi. Wakili Angamizamtuwewe II aliyepanga njama za mauaji ya kimbari nchini NdaRwa mnamo 2064 na mlevi aliyeshiriki kufanya mapenzi ya jinsia moja nchini na mwanamume mwenzake pia ni watu wa Gehenna wenye kilio kikali chenye machozi ya damu huku wakitoa mayowe na kusononeka (uk. 220-242).

## 4.4 **HITIMISHO**

Katika sura hii tumechunguza na kubainisha mandhari na matukio chungu nzima ya uhalisia na uhalisiajabu kama yanavyojitokeza katika riwaya hii ya *Watu wa Gehenna.* Mandhari haya hasa yanapatikana akilini mwa wahusika kwenye ndoto na wakati mwingine yanaonekana halisi kabisa kwa msomaji, ilhali wakati mwingine yanabadilika na kuwa yenye kushtua na kuogofya.

Pia tumechunguza na kubainisha wahusika wa kiuhalisia na wale wa kiajabu katika riwaya hii. Wahusika halisia wanabadilika na kuwa wa kiajabu na kupata maumbile ya kutisha pamoja na kufanya vitendo vya kuogofya kwa mfano mhusika Mishi. Aidha, kwa kutumia mandhari, matukio na wahusika wanaochanganya uhalisia na uhalisiajabu, mwandishi Tom Olali ameweza kudhihirisha, kumulika na kueleza kwa ustadi zaidi baadhi ya mambo ambayo hayangeweza kuelezwa kwa mtindo wa kawaida. Wamitila (2003:274) anaeleza uhalisiajabu kama sifa ya kuyaeleza matukio ya kifantasia, ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja inayoyafanya yaonekane ya kawaida tu, na hivyo kufanya mpaka uliopo kati ya yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana kuwa mdogo sana. Kwa hivyo, mwandishi Tom Olali ameweza kusimulia chimbuko la ufisadi na maswala mengine ibuka kama vile athari za utandawazi na biashara haramu ya kuuza viwiliwili vya zeruzeru na baadhi ya maswala mengine kwa kutumia mbinu hii ya uhalisiajabu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ambayo ni ya mwisho katika utafiti wetu, tumetoa muhtasari wa matokeo kutokana na uchunguzi wetu. Tunakusudia kubainisha iwapo madhumuni ya utafiti wetu yameafikiwa. Pia tumepima nadharia tete za utafiti wetu pamoja na kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu.

## 5.1 KUHUSU MADHUMUNI YETU

Katika utafiti wetu, tumeshughulikia riwaya mbili za waandishi wawili, Said A. Mohamed (*Babu Alipofufuka)* na Tom Olali (*Watu wa Gehenna*). Tumetumia nadharia ya uhalisiajabu kuchunguza na kubainisha dhana za uhalisia na uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari katika riwaya hizi. Tumepata ya kuwa, waandishi hawa wawili wametumia wahusika wakiajabu na mandhari yenye matukio mengi ya kiajabu. Tumebainisha kuwa dhana ya uhalisiajabu imejijitokeza katika viwango vya wahusika na mandhari.

Pia tumetumia tajriba yetu kama wanafasihi kutoa maoni yetu ambayo yametusaidia kupanua mawazo yetu katika kuikamilisha tasnifu yetu. Tumeweza kugusia jinsi uhalisiajabu unavyojitokeza katika fasihi simulizi za jamii zetu na hivyo kudhihirisha kuwa uhalisiajabu sio mtindo mpya lakini umekuwepo katika tamaduni za kila jamii.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia hatua ambazo uhalisiajabu umepiga kwa kuangalia vipindi vya uhalisia hakiki na uhalisia wa kijamaa na kubainisha kuwa kipindi cha uhalisiajabu kiliibuka ili kuweza kuzungumzia masuala ambayo hayangeweza kuzungumziwa kwa njia ya kawaida au kwa mtindo wa kiuhalisia. Kwa kutumia uhalisiajabu, riwaya hizi zimefanikiwa kujadili masuala ibuka na kumulika uozo katika jamii; jambo ambalo mtindo wa kiuhalisia haungeweza. Katika *Babu Alipofufuka*, Babu Mzuka ameyaingilia maisha ya mjukuu wake K na kuyaathiri maisha yake na anavyoendelea kusaka furaha na maana ya maisha ndivyo anapata kinyume chake.

Kutokana na maelezo haya tunapata ya kuwa binadamu anaonekana kutokuwa na uwezo wa kuyadhibiti maisha na maisha yamebaki kitendawili kisichoweza kuteguka. Hivyo tumebainisha ya kuwa binadamu yumo mbioni kupata furaha bila mafanikio. Pia, tumepata ya kuwa, waliokufa bado wangalipo katika hali tofauti na wanaendelea kuathiri maisha ya walio hai.

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*, mwandishi amesimulia chimbuko la ufisadi na kupiga msasa masuala ibuka mathalan biashara haramu ya viwiliwili vya zeruzeru, kuteswa kwa wafanyikazi wa nyumbani katika mataifa ya ng'ambo na vilevile athari za utandawazi katika mitandao ya kijamii maarufu kama '*facebook.*' Kwa mfano, tunampata Lakeisha mamake Baingama ambaye ni zeruzeru amepata mwanamume tajiri wa kumuoa kupitia kwa mtandao na kuwaacha watoto wake wakiteseka na hivyo kuingilia maisha ya ulanguzi wa

dawa za kulevya pamoja na uasherati ili kukidhi mahitaji yao. Mwandishi anakashifu uigaji wa tamaduni za jamii za ulaya na kuacha mila na tamaduni asilia za Kiafrika. Hii ni mifano tu ya masuala ambayo yamezungumziwa kwa ustadi mkubwa kwa kutumia mtindo huu wa kiuhalisiajabu katika riwaya tulizoshughulikia yakaweza kuteka hisia za msomaji.

Katika sura ya tatu na ya nne, tumechunguza riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* mtawalia. Tumebainisha uhalisia na uhalisiajabu katika vipengele vya mandhari na wahusika na kupata ya kuwa, uhalisi na ndoto vinachanganyika na hivyo ni vigumu kuweka mipaka kati ya uhalisia na uhalisiajabu. Hivyo tumewekea msingi nadharia yetu kuwa labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

Katika utafiti wetu, tumepata mandhari yenye matukio na wahusika wa kiajabuajabu kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya zetu teule. Wahusika wanabadilikabadilika na kuchukua nafsi tofauti na kutenda mambo ya kushtua na kuogofya. Kutokana na madhumuni yetu, tumebainisha kwamba riwaya hizi mbili zinaingiliana na kuchangiana kwa kiasi kikubwa. Aidha vipengele vya uhalisiajabu ni vingi mno katika riwaya hizi lakini tumebainisha tu uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari na tumepata uhalisiajabu unajibainisha kwa kiwango kikubwa katika riwaya hizi.

## 5.2 UPIMAJI WA NADHARIA TETE

Dhana ya uhalisiajabu imechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Tumedhihirisha kuwa uhalisia na uhalisiajabu zinaingiliana sana.

Visa vya kimazingaombwe ni vingi mno katika riwaya hizi mbili. Kuna wahusika wengi wa kiajabuajabu ambao hulka yao inaweza kusemekana inatokana na kutokuwa binadamu kamili. Vilevile, kuna wahusika wengine wa kawaida kwenye riwaya hizi walio na uwezo usiokuwa wa kawaida kama tulivyobainisha katika sura ya tatu na ya nne.

Suala la ndoto katika riwaya hizi mbili limechukua nafasi kubwa kama mojawapo wa mihimili ya uhalisiajabu. Jambo hili la kuchanganyika kwa ndoto na uhalisia limeweka ugumu wa kubainisha mipaka ya uhalisi na uhalisiajabu na ndipo tukaweka msingi mhimili wa uhalisiajabu kuwa labda wakati mtu anapoota ndipo yumo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

Matukio mengi katika riwaya hizi yametokea mawazoni mwa wahusika wanapolala ama wako macho na kuota ndoto za kiajabu. Ndoto hizi zinaonekana kama matukio halisi kabisa kwa wahusika hawa na zinaathiri maisha yao hivi kwamba, wanafikia maoni kuwa kama hazijatokea, zitaweza kutokea katika hali halisi wakati mmoja.

Tumebainisha kuwa riwaya hizi kuandikiwa katika pahala na nyakati tofauti sio kizuizi kwa dayalojia kati ya riwaya hizi zinazoitika mwangwi wa riwaya nyingine zenye kutumia mtindo kama huu. Hili ni dhihirisho kuwa mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa imevunjwa kwa maana wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.

Kwa kujitenga na mtindo wa kiuhalisia, riwaya hizi zimo katika tapo la sanaa za kimajaribio zinazojaribu kufaulu pale ambapo uhalisia umelemewa katika kuelezea matukio ya kiajabu kwani, wanauhalisia wanadai kuwa lazima yanayozungumziwa yawiane na ukweli na yawe akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Huenda sababu mojawapo ya waandishi Mohamed A. Said na Olali Tom kutumia uhalisiamazingaombwe katika kazi zao ni kutokana na misukosuko na mawimbi ya mabadiliko na ukosefu wa uthabiti wa kijamii, kisiasa, kiuchumi pamoja na masuala ibuka mathalan biashara haramu ya kuuza viwiliwili vya zeruzeru, kuteswa kwa wafanyakazi wa nyumbani katika mataifa ya ng'ambo na athari za utandawazi katika mitandao ya kijamii.

Kutokana na vipengele ambavyo tumevishughulikia, twaweza kusema kwamba, njia mwafaka ya kufasiri utafiti huu ni kuwa riwaya hizi zimeandikwa katika kuzingatia kaida na kunga za uhalisiajabu ambao umejenga jumuiya pana na inayoendelea kupanuka kote duniani kila uchao. Matumizi ya mtindo huu wa uhalisiajabu umeweza kuangaza uovu na adhabu yake katika jamii kwa ustadi

unaovuta makini ya wasomaji na kuathiri hisia zao. Kuna uwezekano mkubwa wa kuyakumbuka matukio yanayotoa mafunzo kwa wanajamii kama yanavyojitokeza katika riwaya hizi.

Riwaya hizi mbili zina uhusiano mkubwa na kwa kujua au kwa kutojua, waandishi hawa wawili wamo katika dayalojia au mazungumzo yanayoonekana kuigana na kuathiriana kimtindo na kimaudhui. Kimsingi, tunaweza kusema kuwa fasihi moja inasema au inajibizana na nyingine au kutoa mwangwi wa mambo yanayofanana au kulingana na yale ya fasihi nyingine.

Kazi hizi mbili zimetumia sifa bainifu za uhalisiajabu kama nyenzo za kuakisi na kuangaza hali halisi ya udhaifu, kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumifu katika Afrika na ulimwengu wote. Kwa jumla, utafiti huu unatilia mkazo kwamba, uhalisiajabu ndio nguzo kuu ya uendelezaji wa riwaya hizi katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui. Dhamira kuu ya kuangaza uozo katika jamii na adhabu yake imefanikishwa kupitia uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari ambapo maudhui mbalimbali yamebainika.

Kwa hivyo, tumepata nadharia tete zetu kuwa kweli kwani, vipengele vya uhalisia na uhalisiajabu vimejitokeza kwa kiasi kikubwa na pia dhana ya uhalisiajabu imejitokeza kama mhimili mkuu wa dhamira katika riwaya mbili tulizoshughulikia.

## 5.3 **MAPENDEKEZO**

Matumaini yetu ni kuwa, utafiti huu utakuwa msingi bora wa uchanganuzi wa uhalisiajabu wa riwaya za kimajaribio au riwaya mpya. Kwa kuwa utafiti wetu umeshughulikia uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna,* bado tafiti zaidi zinahitajika kwa kuzingatia mielekeo mingine ya kuzihakiki riwaya hizi. Kwa sababu hiyo, tumependekeza utafiti zaidi kuhusu mambo yafuatayo:

1. Watafiti wengine waweze kutumia nadharia zingine kutafiti vipengele tofatutitofauti kwani utafiti wetu umejikita katika vipengele vya wahusika na mandhari katika mwanda mpana wa uhalisiajabu.
2. Uchunguzi wa dhana ya uchimuzi katika riwaya ya *Watu wa Gehenna.*

## MAREJELEO


Alexander, M. (1990). *Flights from Realism.* London. Edward Anold.

Allende, I. (1985). *The House of the Spirits.* London. Anchor Brendon Ltd.

Baldic, C. (2001). *Oxford Concise Dictionary of Literacy Terms*. Oxford. Oxford University Press.

Cooper, B. (1988). *Magical Realism in West African Fiction.* New York: Routledge.

__________ (1998). *Magical Realism in West African Literature*: Seeing *with a Third Eye*. New York: Routledge.

Crystal, D. (1997). *Dictionary of Linguistics and Phonetics.* 4th edition Oxford: Blackwell.

D' Haen, Theo L. (2005). *Magic Realism and Post modernism.* Decentering Priviledged Centers. Zamora Lois Parkison and Wendy Faris (Eds) Magic Realism: Theory, History Community. Durham & London: Duke University Press. PP. 191-208.

Danow, K.D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque.* Kentucky University of Kentucky Press.

Drouwart,L. (1993). *Journal of the South Pacific Association for Commonwealth, Literature and Language Studies*. London. No.36

Encarta Encyclopaedia (2002). New York. Microsoft Company Limited.

Green, J.A (2009). *Dreams of Freedom: Magic Realism and Visionary Materialism in Okri and Blake*. Romanticism 15/1:18-32.

Gromov, M. (2002). *Post Modernistic Elements in Recent Swahili Novels.* Nairobi. (Haijachapishwa).

Hough, G. (1969). *Style and Stylistics*. London. Routledge & Kegan Paul.

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

_____________ (1991). *Mzingile.* Dar es Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Khaemba S.S (1999). *Ulinganishi wa Maudhui ya Mapinduzi katika Dunia Mti Mkavu na Kiza katika Nuru.* Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Khamis, S. A.M (2005). *Signs of New Features in the Swahili Novel*. Research in African Literature 36/1: 92-108.

Magaju, J. (2004). *Uhalisiajabu kati ya Riwaya ya Babu Alipofufuka* (2001) ya S.A Mohamed na *Bina-Adamu!(*2002) ya K.W Wamitila. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Malcolm, N. (1959*). Dreaming U.S.A*. London. Routledge and Kegan Paul Ltd.

Marquez, G.C. (1980). *One Hundred Years of Solitude*. London. Pan Books Ltd.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics & Publishers.

Mdee, J. S., Shafi, A., Kiango, J.G. & Njogu, K. (2009). *Kamusi Kamili ya Kiswahili.* Nairobi. Longhorn Publishers

Mkangi, K. (1984). *Mafuta. Nairobi.* East African Educational Publications.

Mugwika, F. (2012). *Dhana ya Uchimuzi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kimajaribio ya Mafamba.* Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K & Wafula,R.M (2007*). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Nyabunga, A. (2005). *Uhakiki wa Bina- Adamu! (2002) na Musaleo*! (2004) za K.W Wamitila. (Haijachapishwa)

Okri, B. (1992). *The Famished Road.* New York: N.A Talese.

Olali, T. (2008). *Mafamba.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

__________(2010). *Structure and Anti-structure of a Swahili New Novel: A Stylistic Analysis of Babu Alipofufuka.* The Nairobi Journal of Literature, UoN 82-98.

____________(2012). *Watu wa Gehenna.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Robert, S. (1951). *Kusadikika*, London, Nelson.

____________(1967). *Kufikirika*. London: Nelson.

Roh, F. (1925) Nach-Expressionismus-Magischer Realismus. Leipzig. Krinkhardt & Biermann.

Said, A. M. (2001). *Babu Alipofufuka.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

___________ (2006). *Dunia Yao.* Nairobi. Oxford University Press.

Thiong'o, N. (2004). *Murogi wa Kagogo.* Nairobi. East African Educational Publishers Ltd.

___________ (2005). *Wizard of the Crow.* New York: Pantheon.

TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi. Oxford University Press.

_________(2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Toleo la Tatu: Dar es salaam. Institute of Kiswahili Research.

Wafula, R.M & Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (1989). *A Dictionary of Stylistics.* London: Longman Group.

Walibora, K. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17(2010): 143-157.

Wamitila, K.W (1991) *Nagona and Mzingile:* Kezilahabi's Metaphysics. Kiswahili 60: 62-67.

________ K.W. (1999). *Unlocking Katana Mkangi's Walenisi. A Case of parabolic narrative?* Kiswahili 61:83-93.

___________ (2001). *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

___________(2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

____________(2002) *Uhakiki wa Fasihi; Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi Phoenix Publishers Ltd.

___________ (2003). *Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo's *Pedro Paramo*. Kiswahili 66:49-58.

___________ (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publications Ltd.

___________ (2004). *Musaleo!* Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

_____________(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Warnes, C. (2006). *Magic Realism and German Idealism. Modern Language Review.* 101/2:488-498.

Williams, R. (1995). *The Postmodern Novel in Latin America: Politics, Culture, and the Crisis of Truth.* New York: St. Martin's.

Williams, R. (1999). *Marxism and Literature.* New York. New York University Press.

Zamora P.L. & Faris B.W. (1995). *Margical Realism: Theory, History and Community.* London. Duke University Press.